Rosa Mistika—waridi lenye fumbo; uwili wa maisha. Rosa Mistika—wapo wanaomwita malaya, mzinzi mkuu, mvunja nyumba za watu; na wapo wengine wanaomwona kama msichana mwenye nafsi isiyo na hatia, msichana aliyekuwa amezingwa na kutekwa nyara na shinikizo hasi za mazingira, yakamghilibu bila ya kujitambua. Rosa Mistika—wachache wenye malezi makali wamemwita asherati, na kukataa katakata asisomwe kwa hofu ya kupotosha wengine; lakini baadhi wakasema: Hata! Asomwe, ulimwengu upate kioo cha kujitazama na kuona utata wa malezi ya wasichana kwa wazazi: "ubora" wa maisha ya "kifungo" cha "kufuli" na macho kisichoweza kuhimili silika za mwili unaotawaliwa na msukumo wa wakati; na faida ya uhuru usio na mipaka.

Rosa Mistika—waridi lenye fumbo, fumbo la utata, utata unaobeba shtaka mpaka mbele ya Mungu—nani hasa mwenye hatia katika angamizo la Rosa Mistika? Baada ya kutafakari, Mungu anaturudishia walimwengu—wewe na mimi—shtaka hilo: tulisome kwa makini, tujiite wenyewe sisi mashahidi, halafu ndio tutoe hukumu.

Profesa E. Kezilahabi ni mwandishi mashuhuri katika fasihi ya Kiswahili. Yeye ni mzaliwa wa Ukerewe, Mwanza, Tanzania; na ana shahada ya Ph.D. ya Chuo Kikuu cha Wisconsin, Madison cha Marekani.

*Rosa Mistika* ni mojawapo ya riwaya nyingi alizoandika, ikiwa ni pamoja na *Nagona* na *Mzingile* vitakavyotolewa hivi karibuni na DUP. Diwani yake ya pili ya ushairi ya *Karibu Ndani* ilitolewa na DUP mwaka 1988.

HEKIMA NI UHURU

DAR ES SALAAM UNIVERSITY PRESS

ISBN 9976 60 065 8

# Rosa Mistika



86
586
05

E. Kezilahabi

# I

Katika ziwa Victoria—kama liitwavyo mpaka sasa—kuna kisiwa kijulikanacho kwa jina la Ukerewe, maili thelathini hivi kutoka Mwanza, na kama hakuna ukungu, unaweza kukiona kutoka Usukumani. Katikati ya kisiwa hiki kuna jengo kubwa la Wajerumani lililosalia mpaka sasa. Karibu na jengo mpaka leo hii kuna mti uliokuwa ukitumika kunyongea watu—watu weusi nafikiri. Jengo hili liko katikati ya kijiji cha Namagondo. Si mbali na jengo hilo alikuwa akiishi Regina.

Regina alikuwa akijulikana kijiji kizima. Ukimwona anatembea utafikiri anaogopa kutoboa ardhi ya Mungu; lakini yeye ukimwuliza husema, "Ninaogopa kukanyaga viumbe vya Mungu." Wakati akila alizoea kulamba vidole vyake. Watoto wake wakimcheka huwambia, "Wanangu, ninyi hamkuona wakati ule wa njaa; wakati tulipokula mizizi ya miti, wakati mtu aliweza kununuliwa kwa debe moja la mawele." Lakini Regina tangu aolewe hakuwa na raha: alikuwa akisumbuliwa na kuteswa na mumewe kwa kosa lisilo lake.

Katika kijiji chote cha Namagondo hapakuwa na mwanamke aliyekuwa akipigwa karibu kila juma kama Regina. Wanawake wengi kijijini walijiuliza kwa nini hakutaka kumwacha bwana wake. Wengine walimwonea huruma; wengi lakini, walimwona mjinga.

Regina, alikuwa na watoto watano wasichana; wote wazuri kama yeye. Matumaini yake ya kukaa pamoja na watoto hao—kama alivyoambiwa na bwanake—yalikaa katika mimba ya miezi mitano aliyokuwa nayo sasa. Hayo yote Regina hakuwa na haja ya kuambiwa—wala kukumbushwa. Alifahamu. Regina alifahamu: alikuwa halali kifudifudi, alikuwa hali samaki wenye miba mingimingi, alikuwa habebi vitu vizito. Aliogopa kuharibu mimba. Siyo mimba peke yake iliyomfanya Regina asimwache bwanake: ilikuwa pia na moyo aliokuwa nao juu ya watoto wake. Hakutaka kuachana na watoto hao; bila yeye, mumewe alikuwa hawezi kuwatunza. Mawazo yake yote yalikuwa juu ya furaha ya watoto wake katika maisha yao ya baadaye.

**Mawazo haya yalikuwa yakimzunguka kichwani mwake aliposikia sauti kwa mbali: "Hoi! Hoi! Hoi!" Alifahamu. Alifahamu huyo mtu alikuwa nani na alikuwa katika hali gani: sauti hiyo alikuwa amekwishaizoea. Mara moja aliwahimiza watoto wale upesi wakalale. Sauti ilikaribia, na sasa aliweza kusikia maneno yaliyokuwa yakisemwa.**

**"Kila siku ninawakuta hapo—kila siku! Nimekwishawambia kwamba wachawi wote wa Namagondo hawaniwezi lakini wao hawasikii." Sauti sasa ilifika karibu na mlango wa nyumba. Watoto walijikunja kitandani, kimya!**

"Regina! Fungua mlango."

Regina aliamka polepole na kwenda kufungua.

"Wachawi walikuwa wanataka kuniua papa hapa karibu na barabara, lakini nimewatawanya wote! Wotee! Hukusikia wanakimbia?"

Regina hakujibu.

"Wako wapi watoto wangu?" Zakaria aliuliza.

"Wamelala". Regina alijibu kwa unyenyekevu.

"Mke gani wewe! Kunijibu vikali namna hiyo. Waamshe nataka kuwaona."

Bila kuguna, Regina alikwenda kwa huzuni katika chumba cha watoto. Aliogopa kupigwa. Kati ya watoto wake, Rosa Mistika ndiye alikuwa kifungua mimba, naye alijulikana kwa kifupi kama Rosa. Rosa alikuwa msichana mzuri, mrefu kiasi, mnyenyekevu na mnyamavu. Kama akienda kuoga kisimani utamwona kabla ya kuvua nguo anaanza kuangalia huku na huko, huvua huoga upesiupesi, huvaa, huchukua maji na kurudi nyumbani. Akifika nyumbani hujikuta bado ana povu la sabuni sikioni. Alikuwa hapendi kuangaliwa kwa muda mrefu. Ukimwangalia machoni huinamisha kichwa. Rosa akiwa na umri wa miaka kumi na mitano alikuwa darasa la saba.

Flora akienda kuoga, hujiangaliangalia kwa muda mrefu kabla ya kuoga. Hutazania matiti yake ambayo sasa yalikuwa yanaanza kuwa makubwa; hujipapasapapasa kwa mikono kutoka mgongoni mpaka pale matako yanapotelemkia; halafu huanzia kifuani mpaka pale tumbo linapotelemkia; halafu tena hujiangaliangalia. Hata kama amemaliza kuoga hungoja mpaka jua limkaushe ndipo avae. Akienda saa nane kisimani atarudi saa kumi na moja na jiwe lake mkononi, ingawa kisima kilikuwa maili moja tu kutoka nyumbani. Kila mara alitukanwa na mama yake kwamba alikuwa mvivu. Regina akisema kwenda kulima, yeye hubeba mtoto ubavuni. Akiambiwa kuweka moto jikoni yeye huchukua majani kutoka paa la jiko.



Honorata ndiye alimfuata Flora. Honorata alikuwa na shamba lake la pamba. Alipenda sana kufanya kazi. Mara nyingi utamsikia analilia jembe. Ingawa alikuwa mzuri, ilikuwa kama kwamba yeye hakujitambua: alikuwa hajali nguo gani alivaa wala kuweka mafuta nyweleni."Maji yanatosha" alizoea kusema. Honorata akiwa na umri wa miaka tisa alikuwa darasa la tatu.

Stella alimfuata Honorata. Ukifika nyumbani utamwona amekaa mguu mmoja huku mwingine huko; mama yake akisema, "A, a, Stella"! utamwona Stella anaweka pamoja miguu yake akicheka lakini hufungua tena kama mama yake akitega mgongo. Wageni wakija nyumbani yeye huwapanda migongoni. Siku moja alitumia fimbo ya mgeni kukokotea mavi ya kuku chini ya mguu wake. Lakini kama mama yake akifanya kosa la kumpiga atakataa kula siku nzima mpaka abembelezwe. Mara mbili alikuwa amekwishaanguka kutoka mtini. Nguo zake zilizoea kupasuka tumboni na utamwona Stella anakimbia ameshikilia nguo yake ili tumbo lisionekane. Huyu ndiye alikuwa Stella; kipenzi cha baba yake.

Sperantia alikuwa bado hajafahamu kuzungumza. Ukimwambia "Unataka pipi?" Hujibu "Ndiyo." "Unataka kupigwa?" Hujibu "Ndiyo." Siku moja aliumwa na nge na Regina hakuweza kujua mahali pa kuchanja kuweka dawa yake. Sperantia alishika kichwa, mikono na miguu.

Zakaria alipoingia ndani ya nyumba wasichana hawa walijifanya kulala; lakini walisikia kila neno alilosema baba yao. Kwa kuwa Rosa alikuwa amekwishavunja ungo hakuamshwa. Flora akiwa darasa la tano aliamshwa. Flora, Honorata na Stella waliletwa mbele ya baba yao. Mara moja Zakaria alianza mchezo wake wa kawaida.

"Haya ondoeni usingizi! Jipaa–ngeni! Nyuma–geu–keni! Nyuma–geu–keni! Nyuma–geu–keni! Jii–ka–zeni! Jii–legezeni! Maaark–taim! Shoto kulia! shoto kulia!. Mikono juu! Chini! Juu! Chini!"

"Mimi nimechoka," alisema Stella; wengine walimcheka. "Haya imbeni sasa! *Siku moja wawinda* ... aliwaanzia.

Nao hawakuchelewa kuanza:

*Siku moja wawinda, porini walikwenda*
*Wakamkuta Sungura, wakamfukuza na mbwa*
*Sungura kakimbia, mwenye shimo kafika*
*Ndipo katunga wimbo, wimbo wa sikitiko*
*Shambani sikufika na maboga sikula*
*Mnieleze kosa la kunifukuza na mbwa.*

"Tena!" Zakaria aliamrisha. Watoto walianza tena tangu mwanzo.

Zamani Zakaria alikuwa mwalimu lakini alifutwa kazi kwa sababu ya ulevi. Jirani zake walisema alijali pombe kuliko watoto: alikuwa hajatoa hata chapa kuwalipia watoto ada ya shule. Kama sasa watoto walikuwa shuleni, heko kwa mama yao. Regina alilima pamba kwa bidii, na pesa alizopata aliwavika watoto wake. Kitu kimoja kilimsaidia sana Regina katika kuelimisha watoto wake—ng'ombe. Baba yake alipokufa alirithi ng'ombe wanne. Kwa wakati huo wawili walikuwa wamekwishauzwa. Zakaria alikuwa ameshindwa hata kujenga nyumba ya maana. Katika nyumba alimokuwa akilala sasa pamoja na watoto wake, nyota zilikuwa zikiwashangilia kila siku usiku. Tangu Ijumaa mpaka Jumapili Zakaria alikuwa anakwenda kunywa, na siku nyingine za juma alijifanya mgonjwa kitandani. Mke wake hakupata kufahamu mumewe alikuwa na shilingi ngapi benki kwani alimwona akinywa kila juma.

Wakati watoto walipokuwa wakiimba, Zakaria alikuwa akicheza—alikuwa akirukaruka. Labda mambo yote yangalikwenda sawasawa kama Stella asingaliropoka. Stella alikuwa hawezi kuficha siri; labda kwa kuwa alikuwa bado mtoto mdogo. Mara mbili Regina alikuwa amekwishapigwa kwa sababu ya mropoko wa Stella. Stella alisema kwamba wanaume fulani walikuja kumwita mama yake, kumbe walikuwa wachuuzi wa nguo. Kwa Zakaria Stella ndiye alikuwa msemakweli, na alimpenda kwa sababu hii.

"Baba, Baba," Stella aliita.

"Mm," aliitikia.

"Leeo! Leeo! Rosa ali–alipata barua; barua pamoja na shilingi ishirini. Ametuonyesha."

Zakaria alichafuka, Rosa aliitwa mara moja. Rosa alikuja hali shuka ikitelemka chini. Kabla hajasema lolote alipigwa na kuanguka chini. Alijaribu kuamka na kukimbia lakini shuka ilimtegatega na kumwangusha chini tena. Alikuwa sasa mikononi mwa babake.

"Lete hiyo barua, iko wapi? Pamoja na shilingi ulizopewa. Unafikiri sisi hapa maskini!"

Rosa alipigwa tena na tena, makofi yalikwenda mfululizo hata damu ikamtoka puani na mdomoni. Alilia, "Baba nihurumie, sitarudia tena, nimekoma." Rosa alinyang'ganywa shuka. Chupi ilimwokoa lakini matiti yalikuwa nje. Ole wao watakaoyaona matiti ya binti zao! Regina machozi yalimtelemka mashavuni. Alilia kwa sauti. Watoto walipomwona analia nao pia walianza kulia; hapo ikawa kelele moja kwa moja. Hata Stella



alilia. Zakaria hakujali; alichukua fimbo na kuongozana na bintiye mpaka chumba cha watoto hali akinguruma.

"Lazima unionyeshe barua hiyo! Unataka kuniletea umalaya wa mama yako hapa!"

Rosa—akiwa na haya nyingi alichukua mfuko wake wa madaftari, na katika daftari la jiografia alitoa barua hiyo pamoja na shilingi tano. Alimpa babake shilingi hizo; lakini ile barua aliikunjakunja na kuitupia mdomoni. Alijaribu kuitafuna lakini babake alimkaba koo. Rosa hakuitema. Zakaria alikaza mkono. Macho ya Rosa yalianza kuwa mekundu, ulimi ulimtoka na barua ilianguka chini. Ilikuwa na utelezi kama kuku aliyetapikwa na chatu. Zakaria aliiokota mara moja.

"Sema nani amekupa barua hii!"

"Charles,"Rosa alitamka kwa shida.

Charles alikuwa kijana mwembamba na mrefu kidogo, mweupe na mwenye sura nzuri. Wakati huu alikuwa akilelewa na mjomba wake Ndalo kwa ajili ya kusoma shule. Alipofaulu mtihani wake wa darasa la nne, alichaguliwa kwenda kusoma Murutunguru Upper Primary School. Kwa kuwa yeye alikuwa mwenyeji wa Itira—umbali wa maili saba hivi—ilimpasa kuja kukaa karibu na shule. Siku ya kwanza kufika kwa mjomba wake alimkuta Rosa amekaa akiongea na Bigeyo, mke wa Ndalo. Charles alijulishwa kwa Rosa, na Rosa alijulishwa kwake. Ndipo walipofahamu kwamba watakuwa wakisoma shule moja na darasa moja. Kwa kuwa Ndalo alikuwa hajajaliwa mtoto alimtunza Charles kama mtoto wake.

Kila siku asubuhi Charles alizoea kumngojea Rosa na kwenda pamoja shuleni. Jioni pia hurudi pamoja. Zakaria hakusema lolote kwa sababu alimwona bintiye bado mbichi. Miaka miwili sasa ilikuwa imekwishapita, na huu mwaka wa tatu uliwafikisha darasa la saba. Njia iliwafanya wapendane lakini kati yao hakuna aliyekuwa na ujasiri wa kuweza kumwambia mwenziwe. Mwishowe Charles alitambua kwamba siku zake za kukaa pale zilikuwa zikikata kamba, ndipo alipopata ujasiri wakuweza kuandika barua hiyo.

Kama upepo usingalikuwa unavuma kuelekea magharibi siku hiyo, wangaliweza kusikia kelele kwani ulikuwa umbali wa robo maili tu kutoka kwa Ndalo mpaka kwa Zakaria. Charles alikuwa amekwishajiwekea kijumba kidogo cha majani kisichokuwa na chumba. Alikuwa bado anasoma gazeti la *Kiongozi* aliposikia mtu anabisha hodi. Alifungua mlango na kutoka nje pamoja na shuka yake. Katikati ya mji alisimama Zakaria pamoja na bintiye, mkuki mkononi. Bintiye alikuwa

bado analia. Ndalo pamoja na mkewe pia walitoka nje wakiwa katika shuka zao. Loo! Mwezi uliwang'aria na nyota ziliwamulika. Wakiwa katika shuka zao nyeupe walionekana kama malaika waliotumwa kuja kushuhudia ukatili uliokuwa ukitendeka: siyo tu kati ya mwanadamu na mwanadamu, lakini pia kati ya baba na bintiye. Zakaria alianza kusema kwa sauti kubwa:

"Charles! Tangu leo ukome kutembea na binti yangu. Chukua vishilingi vyako (alimtumpia shilingi tano). Unafikiri sisi masikini tusio na mikono!"

Alimshika Rosa shingoni kwa ukosi wa gauni lake akamsukuma kuelekea nyumbani kwake. Rosa alipofika nyumbani alikuta Regina amekwishamchemshia maji ya kumkandia usoni, kunywa na kuondoa damu mdomoni na puani. Baada ya kuoshwa alikwenda kulala. Alilia karibu usiku kucha.

Zakaria alipofika chumbani mwake alifunguafungua ile barua na kuisoma. Alisoma kwa shida sana.

*Namagondo,*
*P. O. Box Mpenzi,*
*Ukerewe.*

*Mpenzi Rosa Mistika*

*Ewe ua waridi lenye fumbo! Ewe dada wa makao yangu uliye kitulizo changu! Funua macho uione makala hii fupi ya mapenzi. Nakuota kila siku wakati wa usiku; sipati usingizi kwa ajili yako. Kuvumilia nimeshindwa. Tafadhali unijibu upesi. Nakutakia ushindi mzuri katika mtihani wako.*

*Wako katika-mapenzi na matumaini.*

*Charles Lusato.*

Alizima taa na usingizi ulimchukua. Upepo ulivuma polepole kupitia dirishani; uliingia ndani ya nyumba na Zakaria alisikia ukiingia masikioni mwake. Alijifunika. Ilikuwa kana kwamba uliingia kusema, "AMANI DUNIANI KWA WATU WENYE MALEZI MEMA!"



# II

Hivyo ndivyo Rosa alivyolelewa; hivyo ndivyo alivyotunzwa; hivyo ndivyo alivyochungwa na babake. Tangu siku hiyo alikoma kutembea na mvulana yeyote. Na Zakaria alipojua hayo alifurahi sana. Alijidai kwamba yeye alifahamu jinsi ya kulea binti zake— hasa alipokuwa amekunywa kidogo. Hakufahamu kwamba Rosa alikuwa katika rika baya, na kwamba ukali ulikuwa haufai; hakufahamu kwamba mabinti wanahitaji uhuru fulani kutoka kwa baba zao; hakufahamu kwamba kwa kumpiga bintiye alikuwa akiingilia utawala usio wake, na kwamba kuhusu maoni ya ndoa yeye alifaa kidogo sana; na hakufahamu kwamba Rosa alihitaji kuwafahamu wavulana. Kwa hiyo, kutokana na malezi ya namna hii, Rosa alianza kuwaangalia wavulana kama watu asiopaswa kuandamana nao, au hata kuzungumza nao. Alianza kufikiri kwamba alitakiwa kujitosheleza. Alizidi kuwa mnyamavu.

Wakati Rosa alipokuwa akijenga fikara hizi moyoni mwake, Charles alikuwa amekwisha kwenda kwao na wala hakupata kumwona tena. Alipata fununu kwamba majibu yao ya mtihani yalikuwa yamekwishawadia shuleni. Alisikia kwamba Charles alikuwa ameshinda na angekwenda Mkwawa, na kwamba yeye mwenyewe alichaguliwa kwenda shule ya wasichana ya Rosary. Kwa kuwa ada katika shule zote za sekondari ilikuwa ikilipwa na serikali, Rosa aliona kwamba atawezá kuendelea. Lakini mambo hayakuwa rahisi kama alivyotegemea. Baada ya muda wa siku chache alipata barua kutoka Rosary ikimjulisha juu ya kuchaguliwa kwake. Barua haikutaja ushindi tu: ilimwomba afike shuleni pamoja na shilingi themanini za nguo, shuka mbili, viatu na sanduku zuri. Pesa za marashi je? Rosa alianza kuona kwamba hataendelea.

Zakaria alisema kwamba hakuwa na pesa. Kwa hiyo mpango ulifanywa wa kuuza ng'ombe mmoja. Regina—alivyokuwa na nia ya kuendeleza binti zake katika masomo—hakupinga. Zakaria alipokwenda kunywa pombe aliwatangazia watu kwamba alikuwa na ng'ombe jike wa kuuza.

Baada ya siku mbili walifika vijana wawili kutoka mjini Nansio. Kwa bahati nzuri waliwakuta Zakaria na Regina wote nyumbani. Bei ya kwanza ilikuwa shilingi 250/– lakini baada ya wale vijana kubisha na kunung'unika kwamba ng'ombe alionekana kuwa na tegu tumboni, bei ya mwisho ilikuwa shilingi 180. Huyo ng'ombe alikwenda na ng'ombe mmoja alibaki. Stella aliamka na kupiga kelele.

"Wanyang'anyi! Acheni ng'ombe wangu." Alivuta kamba iliyokuwa imefungwa kuzunguka pembe, na ng'ombe aligeuka kumfuata. Regina alimshika Stella; wale vijana walichukua ng'ombe. Stella alijigaragaza chini hali akilia; kazi bure.

Rosa alipewa shilingi sabini kununua sanduku, shuka na viatu. Shilingi mia moja na kumi Regina alimtunzia sandukuni mpaka siku ya safari. Rosa alifurahi sana.

Siku hiyo jioni, kama saa kumi hivi, Regina alikuwa amekwishachimba viazi wakati Zakaria alipokusanya nguo kuukuu za kaniki. Nguo hizi mke wake alikuwa hazihitaji tena. Zakaria alikuwa mtu mwenye mizaha mingi; lakini mara nyingine mizaha yake ilizidi kiasi. Ingawa alikuwa mkali sana katika mambo ya malezi, aliweza pia kucheka na kufurahi pamoja na familia yake. Alianza kuzipasua kaniki hizo katika vipande virefu na kusokota kamba moja kubwa.

Alikuwa karibu kumaliza wakati Stella alipojongea karibu na kuanza kuuliza maswali.

"Unataka kufanya nini na kamba hiyo?" Aliuliza mkono wake ameweka kwenye kidevu.

"Oo, ninataka kwenda kumchukua yule ng'ombe."

"Utarudi lini?"

"Leo usiku."

"Lakini kwa nini unasokota kamba ya nguo? Kwa nini hutumii nyuzi za kitani?"

Zakaria alitabasamu kidogo kuona mtoto anataka kuvumbua ujanja wake.

"Oo ninataka kumwiba ng'ombe usiku; kamba nyeusi haiwezi kuonekana usiku.... Ebu shika mwisho wa kamba, haya vuta!" Stella alivuta lakini baba yake karibu amwangushe.

"Vuta kwa nguvu," alivuta tena.

"Basi."

Kamba ilikuwa tayari na Zakaria aliondoka pamoja na fimbo kuelekea Nansio hali moyoni akicheka. Regina aliporudi nyumbani jioni kabisa



Stella alimwambia mamake kwamba Zakaria alikwenda kumchukua ng'ombe. Regina alielewa kwamba alikwenda kunywa pombe. Kwa kawaida Zakaria alikuwa hasemi nyumbani kwamba anakwenda kunywa pombe.

Jua lilitua, giza likatanda. Wasichana walianza kuingiza kuni ndani ya jiko tayari kwa mapishi ya chakula cha usiku. Siku hiyo ilikuwa ni zamu ya Flora kusonga ugali. Maji yalipochemka tayari kuweka unga, Honorata alianza kumsukumasukuma Flora atoke juu ya kiti ili yeye apike. Regina alimsukuma Honorata kwa nguvu akaanguka chini. Honorata asingekarisika sana kama Stella asingalitoa macho na kumzomea "Woo" hali amekunja vidole vya mkono. Honorata alimrukia Stella na kumpiga teke. Stella alilia.

Regina alichukua kijifimbo kumpiga Honorata lakini alikimbia nje. Mama hakuweza kukimbia. Wakati mambo hayo yalipokuwa yakitendeka, Flora alikuwa amekwishapakua ugali. Regina alimsifu na kumwambia kwamba bwana atakayemwoa atapata bahati. Zakaria aliwekewa sehemu yake pembeni. Wakati ulipowadia wa kula Regina alimwita Honorata aingie jikoni asahau yote aliyoyatenda. Alivunjavunja ile fimbo na kuitupa nje. Honorata aliingia. Walikaa katika duara miguu miwili imewekwa pamoja na imekunjwa kurudi nyuma. Regina alikaa akiangalia ugali kwa bega. Miguu yake aliielekeza mbele na Sperantia bila kuambiwa alikaa juu ya miguu hiyo.

Kama kawaida Regina alikuwa akitumia muda huu kuwaonya binti zake. Siku hiyo alianza kumwonya Stella. "Usipoachia uwongo huo nitakukata ulimi, nitakukata masikio!" Wengine walicheka. Stella alinuna. Regina aliendelea kumwonya kwamba lazima apige magoti kila mara akimpatia babake kitu fulani. Honorata alionywa kwamba akimwona mgeni anakuja nyumbani lazima ampokee fimbo yake na kuleta kiti mara moja. Flora alionywa juu ya uvivu wake katika kulima: juzijuzi Honorata alimaliza matuta mawili yeye akiwa bado na tuta moja.

Kwa kuwa Rosa alikuwa amekwishavunja ungo alipewa maoni kama haya: "Mwanangu, wewe sasa umekuwa mtu mzima. Karibu utakwenda huko ng'ambo Usukumani. Usitusahau sisi wazee wako—tuandikie barua mara kwa mara. Jambo moja hasa ningependa kukuhadharisha: wavulana wakorofi. Huenda wakakutaka mapenzi, nia yao ikiwa tu kukupa mimba itakayokukatisha masomo yako. Daima wakwepe hao. Na iwapo utakuwa mpumbavu ukapata mimba usiitoe. Tunasikia kwamba siku hizi wasichana wengi wanaosoma wanafanya hivyo ili wapate kuendelea na masomo yao. Wanapenda masomo zaidi kuliko watoto. Hata hivyo ni wauaji."

Alinyamaza kwa muda kitambo na kunywa maji. Aliendelea; "Mtoto ni majaliwa ya Mungu, na siyo kila mtu anapata. Mwone Bigeyo anavyosumbuka. Kwa hiyo—kama mimi nilivyokuzaa—ukipata mimba afadhali uache shule; kaa na mimba yako. Kama unaogopa kutunza mtoto mimi nitakusaidia kumtunza. Wasichana wote wanaotoa mimba sasa watasikitika baadaye; watashangaa kuona kwamba hawapati mimba katika maisha yao ya siku zijazo. Wanapokuwa bado wasichana hawaoni faida ya mtoto, watakapokuwa wazee kutembelea fimbo watawalilia watoto wao walioua wakingali wasichana! Wanasema kwamba nchi imejaa watu. Sioni hiyo inawezaje kuwa sababu ya kuweza kuua mtoto ambaye amekwishaingia tumboni."

Regina alikuwa mwanamke mwenye busara ingawa hakuwa na kisomo chochote. Alipomaliza kusema maneno hayo alimwona Sperantia akiyumbayumba kwa usingizi. Aliwaambia watoto wale upesi wakalale. Wote walikula haraka na kunawa mikono ndani ya sufuria. Walipomaliza kunawa mikono waliacha vyombo ili wavioshe kesho yake asubuhi. Regina alichukua ugali na Honorata alichukua mboga kwa ajili ya Zakaria. Flora alibeba mtoto, kichwa begani. Rosa alichukua koroboi kwa mkono mmoja juu ya kichwa chake wapate kuona vizuri. Walitoka jikoni kwenda nyumba ya kulala. Walipofika nje Stella alisema.

"Hicho nini!" alikuwa akiangalia juu angani.

"Ni nyota inahama," Honorata alisema.

Rosa aliwambia kwamba ni roketi ilikuwa ikizunguka dunia. Aliwambia kwamba Marekani walitarajia kufika mwezini. Stella aliongezea kwamba mwezini kuna sungura; alisoma kitabuni juzi.

Waliingia ndani ya nyumba. Wasichana walikwenda katika chumba chao. Walianza kutegeana na kutegua vitendawili. Walipochoka na vitendawili walianza kusimuliana hadithi. Saa zilikuwa zimekwenda mbali. Honorata alikuwa akisimulia hadithi yake; lakini alipoona kwamba hapakuwa na mtu aliyekuwa akisikiliza aliacha. Alikwenda kuzima koroboi. Loo!! Aliona nyoka mkubwa mweusi akitembea kuelekea chumbani mwao kutokea mlango wa nyuma. Alipiga kelele kwa sauti ya juu, "Waayi!" Wengine waliamka na kukimbia bila kuona hatari ilikokuwa. Walipiga kelele wote, walibanana mlangoni, lakini mwishowe walipita. Stella alikuwa wa mwisho kupita, nyoka alimgusa mguuni lakini hakuweza kumwuma. Regina ambaye alikuwa amekwishalala aliamshwa na kelele za watoto. Binti zake wote walikuwa sasa katika chumba chake.

"Nyoka, nyoka!" Stella alipiga kelele.



"Ameniuma mguuni," aliendela kusema.

Kwa kuwa hapakuwa na mwanamume yeyote ndani ya nyumba, Regina aliona afadhali kufa pamoja na watoto wake. Alichukua fimbo kubwa sana na kuelekea mlangoni. Nyoka alikuwa bado anagaagaa chini; alionekana kana kwamba alikuwa amebanwa na mlango: hakuweza kuingia ndani kabisa. Regina alimpiga fimbo mara mbili–tatu. Stella alikuwa akishangilia: "Piga! piga!" Nyoka alionekana kuruka juu. Regina alitupa fimbo na kukimbia. Alichukua mkuki sasa; alimchoma kichwani. Stella alisema, "kumi na mbili," ilionekana kana kwamba nyoka huyu wa ajabu alikufa.

Regina alikuwa amekwishatoka jasho. Alikuwa bado akijipangusa jasho Zakaria aliposukuma mlango na kuingia. Stella alimwambia, "Nyoka! Angalia usikanyage nyoka!" Zakaria alicheka. Alimchukua yule nyoka kwa mikono yake na kumwonyesha Stella kwanza. Stella alicheka machozi yakamtoka. Wengine pia walipotambua walicheka mpaka mbavu zikawauma.

Walimletea chakula akala. Baada ya kula alitoa chupa moja ya moshi mfukoni mwake. Alianza kunywa. Hata watoto aliwaonjesha kidogo kidogo. Alikunywa nusu tu na kulala.

Usiku huo mvua ilinyesha kwa wingi sana. Lo! Nyumba ilikuwa kama mti. Ilivuja kustaajabisha. Kulikuwa na ngozi za ng'ombe mle ndani ya nyumba. Regina alizichukua na kuwafunika watoto wake, na matone ya mvua yalicheza patapata juu yao.

# III

Siku zilikwenda polepole sana kwa Rosa. Alikuwa akiangalia kalenda kila siku. Moyo ulikuwa ukimdunda: alikuwa hajasafiri kwa njia ya meli, alikuwa hajaona mji wa Mwanza, alikuwa hajaona majumba yenye orofa nne au tano, na alikuwa hajaona gari moshi. Alipoambiwa kwamba motokaa zinaweza kupita juu ya reli kwenda upande mwingine hakuweza kuamini. Hatimaye siku zilikaribia na kalenda ilimwambia kwamba lazima aondoke Jumatatu kwenda shuleni.

Siku ya Jumamosi, Rosa alikwenda kununua vitu vilivyokuwa vikihitajika. Flora aliandamana naye. Walikwenda kwa miguu—umbali wa maili sita hivi. Njiani walikutana na vijana waliojaribu kuwasimamisha. Walikimbia. Miluzi ilipigwa kuwafanya waangalie nyuma lakini wao hawakuangalia nyuma kamwe; waliendelea kukimbia kama ndege walionusurika. Mwishowe walifika mjini Nansio. Waliingia duka moja la BATA alimokuwa akifanya kazi bwana Ndalo. Walitumainia kwamba atawasaidia kuchagua viatu vizuri kwa bei nafuu. Waliviona viatu. Rosa alijipima, akaona vinamkaa.

"Bei?" aliuliza.

"Shilingi ishirini na saba," Ndalo alijibu kwa sauti ili Mhindi pia asikie.

"Sisi hizo hatuna."

"Mnazo shilingi ngapi?"

"Sisi tunazo kumi na nane."

"Hamna kabisa!"

"Hatunazo," wote wawili walijibu pamoja.

"Ngoja nikamwulize mwenye duka."

Alikwenda kumwuliza Mhindi aliyekuwa amekaa akitafuna kitu fulani. Alirudi.

"Amesema shilingi ishirini na tano bei ya mwisho."

"Sisi hizo hatuna!"

"Eti hawana."

"Kumi na tisa haidhuru," alijibu Mhindi.



"Hatuńa hizo tumesema."

"Hawana," Ndalo alirudia tena.

"Ambiye yeye iko tembea duka yotee iko rudi."

Ndalo aliwambia wasichana katika lugha ya Kikerewe waende duka lililokuwa mbele yao upande mwingine wa barabara. Aliwambia kwamba humo wataweza kupata kwa bei ya shilingi kumi na sita.

"Tejama wewe iko haribu biashara yangu! Mimi fikiri wewe iko fanya kaji majuri, kumbe danganya." Baniani alifoka. Alimsukuma mmatumbi nje na alimtupia shilingi tano.

"Haya! Chukua. Kwenda nyumbani! Kwenda nyumbani! Pana rudi! Kwenda nyumbani! Kwenda lima ndani ya tope!"

Ndalo kuona kwamba katukanwa hali nchi yake imeshapata uhuru, alianza kuvua shati.

"Wewe Baniani nitakuharibu sura sasa hivi usahau pilipili!" Shati lilimbana mabegani. Alipovua Baniani alikuwa amekwishafunga duka. Umati wa watu ulikuwa umekwishakusanyika.

"Mwoga huyu!" Mtu mmoja alisema, "Wewe kupiga mtu mpaka uvue shati! Ulishaona wapi?" Ndalo hakuwasikiliza watu tena. Alivaa shati lake na kutembea akielekea nyumbani.

Rosa na Flora walikwenda mle dukani. Walivipata kwa bei ileile waliyoambiwa na Ndalo. Pesa zilizobaki walinunua shuka na sanduku. Kwa kuwa walikuwa na mizigo walipanda basi kurudi nyumbani. Walipofika nyumbani walimkuta Bigeyo akiwangojea, kwani Rosa alikuwa amemwambia aje amnyoe.

Walikuwa wamekaa kivulini chini ya mchungwa. Regina alikuwa akifua nguo za Rosa. Mkasi ulilia "kacha kacha, kachu" juu ya kichwa cha Rosa. Rosa alikuwa akijitazama ndani ya kioo kila wakati akimwongoza Bigeyo asijekata sana nywele zake za mbele karibu na uso. Stella aliona kitu fulani kinashuka kasi sana. Alipiga kelele hali akitupa mikono juu.

"Swa! Swa! Swa!"

Wengine pia waliamka na kupiga kelele. Kazi bure. Kifaranga kimoja kilikwenda kinaning'inia kati ya kucha za mwewe. Walibakia kuhesabu vilivyosalia.

"Vilikuwa kumi: Sasa vimebaki vitatu!" Flora alishangaa. Rosa alikaa chini tena kunyolewa. Muda si mrefu mwewe alirudi. Safari hii Honorata ndiye alikuwa wa kwanza kumwona.

"Swa! Swa! Swa!" alitupa mikono juu, "Swa!" Mwewe alikuwa amekwishachukua kifaranga kingine. Zamu hii hakuenda mbali. Alitua juu ya

mti karibu na mji. Wasichana walianza kumtupia mawe lakini hayakumfikia. Mwewe alikula kifaranga bila kujali. Alipomaliza aliruka kwa raha ya shibe. Vifaranga vilibaki viwili. Ilionekana kana kwamba hata mwewe alifahamu kwamba huu ulikuwa mji wa wanawake.

Kesho yake asubuhi Rosa, Flora na Honorata walikwenda Murutunguru kusali misa ya kwanza. Rosa alivaa viatu vyake vipya. Alirudi nyumbani amevishikilia mkononi. Walipofika nyumbani walikuta Regina anamenya viazi. Alionekana kutokuwa na raha. Walimsaidia upesiupesi. Waliviosha na kuviweka ndani ya sufuria. Zakaria alikuwa amekwenda kusali kwenye pombe. Wanasema aliponunua pombe alizoea kuinua bakuli juu kuwapatia watu akisema, "Kunyweni hii ndiyo damu yangu." Labda kwa kuwa alikuwa mtu mwenye mizaha mingi.

Siku hiyo Zakaria alimpitia Ndalo kwenda kilabuni. Rosa na Flora waliporudi nyumbani kutoka kusali hawakumkuta, lakini waliweza kuona kwamba mama yao hakuwa na raha.

Siku hiyo saa zilikwenda polepole sana kwa Rosa. Baada ya chakula cha mchana alianza kunyoosha nguo zake. Alipomaliza alipanga vitu vyake sandukuni. Rosa alikuwa akijaribu kufunga kufuli lake jipya aliposikia mama yake akifoka na kumtukana Stella.

"Wizi wa baba yako huo lazima uukomeshe!" Stella alipiga chenga mbili–tatu huyoo! kwa Bigeyo. Stella alikutwa akichukua samaki chunguni. Jua lilipotua, Bigeyo alimleta Stella nyumbani. Alimwombea toba kwa mama yake. Jioni hiyo maneno ya Stella yalikuwa machache. Hata wakati wa kula hakusema lolote. Regina alimwangalia Rosa kwa muda mrefu. Alitaka kumwambia kilichotokea. Alisita: alimhurumia.

Usiku Rosa hakulala. Aliamka kuangalia dirishani. Aliona bado giza. Alijaribu kufumba macho apate usingizi. Kazi bure; usingizi hauwezi kushurutishwa. Baada ya muda mfupi aliamka tena. Aliona bado giza. Usingizi ulimpata karibu kucha. Alipoamka mara ya tatu ndege walikuwa wamekwishaanza kuimba. Alipoangalia dirishani hakuweza kuamini macho yake. Aliona watu wawili—hapana, watu watatu. Mmoja wao alikuwa amebebwa katikati, miguu yake ikikwea chini. Alikwenda kumwamsha mama yake alipomtambua baba yake.

"Hodi, hodi."

Regina alifungua mlango.

"Kitanda chake kiko wapi?" Ndalo aliuliza. Zakaria alilazwa juu ya kitanda. Ndalo aliwaeleza kwamba alikunywa chupa moja na nusu. Alipoonyesha kwa mkono ile nusu, ilionekana kwamba alikunywa karibu



chupa mbili za moshi. Zakaria alimwagiwa maji na aliletewa maziwa. Alinyweshwa maji ya limau. Saa nne asubuhi Zakaria alikuwa bado hajafunua macho yake.

Safari ya Rosa ilivunjika. Hakuweza kwenda siku hiyo na kumwacha baba yake katika hali hii. Mchana kutwa binti zake walikuwa wamemzunguka. Hata chakula cha mchana walikula karibu na kitanda chake. Saa kumi na mbili jioni Zakaria alianza kujitingisha. Alifumbua macho. Ndalo alimwona ni mzima na akaondoka kwenda nyumbani kwake. Zakaria alipofumbua macho tena Regina alimwuliza.

"Unataka nini?" Zakaria alinyamaza tu.

"Unataka kula nini?" Regina aliuliza tena kwa sauti.

"Ombe, ombe," Zakaria alijibu kwa sauti hafifu sana.

Waliogopa kumpatia "Ombe." Badala yake walimtayarishia uji. Baada ya kunywa uji Zakaria aliweza kukaa kitandani. Ndalo alipokuja usiku kumjulia hali alimkuta amekaa kitandani.

"Aaa! Aaa! pombe jana ilikuwa ya kutuua. Hivi tulikunywa chupa ngapi?" Zakaria aliuliza.

"Mimi nakumbuka tulikunywa chupa kumi."

"U, u, u. Hata Christmas hatukunywa namna hii!"

Usiku Zakaria alilala kama kawaida. Ilionekana wazi kwamba amepona. Kesho yake asubuhi—Jumanne—Regina alikwenda nyumbani kwa Ndalo kufanya upelelezi zaidi. Alipoukaribia mji wa Ndalo alishangaa kuona matendo yaliyokuwa yakitendeka pale nyumbani. Ndalo pamoja na Bigeyo walikuwa wanakula nyama ya kuku hali wanakimbia kuzunguka nyumba.

Ndalo na mkewe walikuwa wakisumbuliwa na jambo moja—uzazi. Walikuwa wamekwishapoteza pesa nyingi sana kutafuta dawa ya uzazi. Mwaka mmoja walikwenda nchi za mbali kuitafuta. Walirudi na nusu debe la mizizi ya miti. Mizizi ilikwisha, na wala hapakuwa na alama yoyote ya Bigeyo kupata mimba. Mwaka uliofuata walikwenda pengine. Huko walimkuta mganga mmoja wa kienyeji aliyewaambia kwamba Bigeyo alikuwa hazai kwa sababu alipokuwa bado msichana alikataa kuwabeba wadogo zake mgongoni. Dawa ya uzazi sasa ilikuwa lazima kupata mkojo wa wadogo zake ajimwagilie mgongoni. Lakini jambo hili halikuwa rahisi: wadogo zake sasa walikuwa watu wazima.

Waliporudi nyumbani, haukupita muda mrefu mdogo wake akamtembelea. Bigeyo alifurahi sana. Wakati wa kulala ulipofika alimpelekea mdogo wake kopo. Alimwambia kwamba katika kijiji hicho kulikuwa na

wachawi wengi na ilikuwa hatari kutoka nje wakati wa usiku. Alimwambia akojoe ndani ya kopo. Asubuhi na mapema Bigeyo alichukua lile kopo na kwenda kujimwagia mgongoni. Mwaka ulipita. Bigeyo alipokuwa anashiba sana mumewe alimwuliza kama amepata mimba. Miaka miwili ilipita: hapakuwa na alama yoyote kwamba Bigeyo alichukua mimba.

Mwaka uliofuata walijaribu hospitalini. Daktari alimwambia wazi kwamba hawatapata mtoto lakini wao hawakuamini. Mwishowe walikata shauri kwenda kaskazini, huko walimkuta mganga mwingine aliyewaambia wale nyama ya kuku mweupe wakikimbia kuzunguka nyumba ili kutakasa mji. Regina aliwakuta wakila nyama hii. Bigeyo alipokuwa akiambiwa kwamba wasichana wengi hutoa mimba siku hizi hakuamini. Alizoea kusema:

"Yuuu! Yuuu! Sisi wengine tulilaaniwa umhuuu!" Alizoea kuweka mkono kwenye shavu. Hapo ndipo Regina humwambia: "Wasichana wa siku hizi wanatoa mimba kama mtu aliyeumwa na kunguni. Mtu aliyeumwa na kunguni huamka, humtafuta chini ya godoro, chini ya mto, ndani ya shuka, na kwenye pembe za kitanda mpaka ampate amwue. Hivyo ndivyo wasichana wa siku hizi wanavyojitahidi kuua watoto. Wanapopata mimba wanafikiri ni kunguni aliyeingia tumboni kuwanyonya damu. Wanajaribu wawezavyo kumtoa. Wasichana wanatoa mimba kama mwanamke ambaye amefanya mpango na bwana mwingine arudishavyo mtoto nyumbani. "Rudi nyumbani! Ukija huku utaliwa na jini!" Na mtoto hurudi nyumbani anakimbia. Wanawafukuza watoto kutoka tumboni wapate kuendelea na mipango na vijana wengine."

Kwa hiyo, Regina alipowakuta wanakula nyama wanakimbia alifahamu nia yao. Alisimama kwa muda kuwangoja wamalize matendo yao. Walipomaliza alibisha hodi nyumbani. Bigeyo alimweleza juu ya mganga wao mpya. Baada ya kusimulia yote ya kaskazini, Regina aliuliza maswali yake yaliyokuwa yamempeleka. Ndalo alimwambia wazi kwamba Zakaria alikuwa akinunulia watu pombe ovyo, hata watu ambao hawakumfahamu siku hiyo walifaidika. Alitumia karibu shilingi hamsini.

Regina aliporudi nyumbani alikuwa anatembea mikono ameweka nyuma kama mtu aliyefiwa. Ilionekana wazi kwamba Rosa hatakwenda shuleni. Rosa sasa alifahamu. Aliambiwa na mamake. Zakaria alisahau kufunga sanduku alipozichukua.



Ng'ombe mmoja aliyekuwa amebaki hakuuzwa kwa sababu alikuwa hazai tena. Zaidi ya hayo wadogo zake pia walihitaji ada ya shule. Regina alikuwa na shamba kubwa la mihogo, kama eka tatu au nne hivi. Alimwambia Rosa kuchimba eka moja. Dada zake walimsaidia. Kazi hii ilichukua muda mrefu. Kuchimba, kutoa maganda, kukausha na kuuza—hii haikuwa kazi rahisi. Majuma matatu yalipita, udaga ukawa tayari. Udaga ulikaa pale nyumbani muda wa siku mbili: wanunuzi hawakupatikana. Rosa alikata tamaa.

Zakaria alikuwa ametulia tu kama mambo haya yalikuwa hayamuhusu. Aliendelea kunywa pombe kama kawaida. Regina alikuwa akitumainia wanunuzi kila siku. Mwishowe wazo lilimwingia kichwani. Alikusudia kutengeneza pombe ya muhogo—inaitwa mapuya. Alipata mawele kwa mabadilishano na udaga. Alikuwa na nia. Pombe ilitayarishwa. Ilikuwa siku ya Ijumaa pombe ilipokuwa tayari—mapipa matatu.

Rosa mwenyewe ndiye alikuwa akiuza. Dada zake walimsaidia kuosha bakuli za kunywea. Hawakwenda shule siku hiyo. Ilikuwa mara ya kwanza watu wengi kufika katika mji wa Zakaria. Wengi walishangaa walipoona nyumba ya Zakaria. Ilikuwa imelala upande.

Pombe ilikuwa kali sana. Watu walimsifu vikubwa Regina. Saa sita ilipofika watu walikuwa hawasikilizani tena. Hata wale ambao walikuwa hawajanunua pombe walikuwa wamekwishaanza kuzungumza Kiswahili kirefu.

Ilikuwa mara ya kwanza kwa Stella kuona walevi—matendo na maneno yao. Honorata alikuwa akiosha bakuli Stella alipomwambia: "Honorata! Angalia! Angalia a! a! a!"

Honorata aliangalia akatoa macho mara moja: mtu mmoja alikuwa anakojoa karibu nao. Stella mwishowe aliwazoea, kwani aliwaona wakikojolea michungwa, migomba, maua yao—hata nyumba. Palikuwa na mpiga zeze. Watu walichezesha mabega yao utafikiri hayana mifupa. Walipiga mishindo chini utafikiri siafu walikuwa wakiwatambaa miguuni. Mmoja alikuwa amekwishachimba shimo refu kwa mguu wake, lakini bila kuhamisha mguu aliendelea kupiga mumo humo—labda kuonyesha nguvu zake. Wanawake pia waliingia kucheza. Wao walisimama mbele ya mwanamume waliyempenda na kuchezesha mabega yao polepole, bila kupiga miguu chini, shingo zao upande. Walipiga vigelegele pia. Mwanamume aliyechezesha mabega zaidi aliinuliwa mikono juu na mwanamke.

Wakati watu walipokuwa wanacheza zeze, mtu mmoja alimwendea Rosa akamwambia: *"Mai children! we know Anglish Makerere I, Makerere I."* Rosa alicheka. *mabia."*

*"Yes, yes give me mabia."*

Ujanja wake, pombe alipewa na Rosa.

Wanywaji walikuwa wamekaa katika vikundivikundi. Katika kikundi kimoja mtu fulani alikuwa akisukumwa atoke. Stella alisikia walivyokuwa wakimwambia. Alirudia maneno: "Kupe toka! Jitegemée!"

Katika kikundi kingine watu walikuwa wakicheka sana. Stella alikwenda kusikiliza. Mtu mmoja alikuwa akisimulia ubaya wa pombe. Alisema kwamba mlevi mmoja alilewa sana akasahau kujifunika blanketi. Mbu walimnyonya damu yote wakabakiza ngozi tu. Mlevi mwingine alilala nje; kesho yake alikutwa nguo zimekwisha liwa na mchwa. Alipomaliza hadithi zake aliomba pombe anywe.

Katika kikundi kingine watu wawili walikuwa wakigombana juu ya utajiri.

"Una nini wewe matako nje!"

"Ndiyo, matako nje lakini ninaweza kukulisha wewe pamoja na mji wako mzima."

Wazee kabisa walikuwa na kikundi chao. Mzee mmoja alikuwa akisema kwamba atakayemnunulia madebe mawili ya pombe atampatia binti yake aoe. Zakaria—ingawa hakuwa mzee sana—alikuwa katika kikundi hiki. Yeye alikuwa akijidai kwamba anafahamu kutunza binti zake.

Regina alikuwa amempa Zakaria dèbe zima la kunywa, yeye pamoja na rafiki zake. Debe lilipokwisha alidai tena jingine. Alitishia kwamba atamwaga pombe yote kama wakimnyima. Walimpa.

Kama saa kumi na mbili hivi, mapipa yote matatu yalikuwa matumboni mwa watu. Watu waliyumbayumba kwenda majumbani kwao. Wengine walilala hapo. Regina na Rosa walipohesabu pesa walizopata walikuta shilingi mia mbili. Walifurahi sana.



# IV

Rosa alikwenda shule ya wasichana ya Rosary. Shule hii ilikuwa imejengwa kupakana na barabara. Kulikuwa na milima karibu kila upande. Milima hii ilikuwa imejaa mawe makubwamakubwa meusi na mapango ambamo fisi walikuwa wakilala. Usiku utawasikia wakicheka lakini mchana hawaonekani. Shule tano zaidi zilikuwa zimejengwa katika milima hii. Shule hizi zote zilikuwa za wavulana. Lakini shule moja ya wasichana ilitosha kupafanya pawe mahali pazuri pa kusomea. Upande mmoja sauti nyororonyororo za wasichana ziliweza kusikika, nazo zilijibiwa upande mwingine na sauti nzito za wavulana. Mara chachechache sauti hizi ziliweza kusikika pamoja zikiwa na majadiliano au mdahalo au labda dansi. Rosa alikuja katika mazingira haya. Mahali penye furaha, lakini mahali ambapo wasichana walikuwa wakiadimika sana. Msichana ambaye hakuwa na rafiki wa kiume lilikuwa kosa lake mwenyewe.

Shule hii ilikuwa ikiendeshwa na mabikira. Walionekana kufaa sana katika shule iliyokuwa imejengwa kati ya mbwa mwitu. Wasichana walizoea kuwaita masista. Mkuu wa shule hii aliitwa Sista John. Rosa alipofika shuleni Sista John alishangaa. Maafisa wengi walikuwa wamekwishagombania nafasi yake. Afisa mmoja alikuwa amekwishamwambia Sista John kwamba alimfahamu sana Rosa. "Msichana huyo," alisema, "alikufa maji wakati akiogelea ziwani." Rosa alikuwa mzima. Ingawa alichelewa mwezi mmoja aliruhusiwa kuchukua nafasi yake. Baada ya siku mbili Rosa aliandika barua nyumbani kuwajulisha wazazi wake hali yake na taabu aliyoipata safarini. Alikuwa bado akiyakumbuka maneno ya mama yake.

Rosa hakukawia kupata rafiki pale shuleni—aliitwa Thereza. Rosa alipokuwa akimtembelea rafiki yake chumbani kwake, Thereza alizoea kumwonyesha picha za wavulana aliokuwa nao. Rosa alishangaa kuona jinsi rafiki yake alivyokuwa mjinga. "Mimi sipendi kuzungumza na wavulana," alisema. "Hawasemi ukweli wowote—hata sitaki waniguse!"

Kweli Rosa, kwa wakati huu, alikuwa bado hataki kuzungumza na mvulana yeyote. Wavulana walipokuwa wakimsemesha aliwajibu kwa maneno makali ya kukatisha tamaa. Hata hivyo vijana hawakuweza kuvumilia kumwona Rosa bila rafiki wa kiume: alikuwa mzuri. Baada ya mwezi mmoja alikuwa amekwishapata barua zaidi ya ishirini. Zote hizo alizijibu kwa mstari mmoja tu, "Samahani kaka, mwenzio sijiwezi. Jaribu mahali pengine."

Pale shuleni kulikuwa na mpango wa kucheza dansi na wavulana kutoka shule mbalimbali mara tatu katika kipindi. Rosa hakuhudhuria hata mara moja. Wasichana waliruhusiwa kutembea au kukaribisha rafiki zao kwa maongezi siku ya Jumapili. Ni mara chache Rosa alitoka nje ya eneo la shule, na wala hapakuwa na kijana aliyemtembelea siku za Jumapili. Masista walimwita msichana mwema na mwenye bidii. Sista John alimpenda sana Rosa. Baada ya muda si mrefu Rosa alichaguliwa na Sista John kuwa mkubwa wa darasa lake. Wasichana wa darasa la tisa pia walimpenda, hasa kwa sababu alikuwa hajapata kugombania mvulana na msichana yeyote.

Kweli alikuwa msichana mwenye bidii, kwani kipindi kilipokwisha alikuwa wa pili katika mtihani. Hivyo ndivyo Rosa alivyomaliza kipindi chake cha kwanza; hivyo ndivyo alivyoweza kujitunza. Alikuwa amekwishawajulisha nyumbani siku ya kufika. Alipofika nyumbani alikuta mama yake amemngojea kwa hamu sana. Rosa alifurahi sana kuwaona dada zake. Wakati akizungukazunguka mji kuangalia mabadiliko alikuwa amembeba Sperantia ubavuni. Hakuona mabadiliko makubwa sana isipokuwa kwamba nyumba ilionekana kuwa chafu. Baba yake alikuwa amekonda lakini siyo sana.

Watu kijijini walipomwona anakwenda kuteka maji au kusali walimwuliza alikuja lini, na waliendelea kumwuliza hata baada ya juma moja. Walimwambia kwamba alikuwa amekwishanenepa, na kwamba alikuwa mzuri zaidi. Baada ya juma moja na nusu watu walimzoea tena.

Rosa alitumia muda wake kwa kusoma vitabu vya hadithi. Mara nyingi utamwona amekaa chini ya mti akisoma. Mara nyingine alikuwa akiwasaidia dada zake kujibu maswali ya historia au kufanya hesabu. Rosa alikuwa anasoma kitabu cha Shaaban Robert cha *Kusadikika;* mama yake alikuwa amekaa kivulini akisuka mkeka; baba yake alikuwa akichonga mpini wa jembe kwa tezo; Sperantia alikuwa analia kwa sababu mtoto wake aliyekuwa amemtengeneza kwa udongo alivunjika



shingo na sasa alikuwa akimshurutisha Flora aunge tena shingo hiyo wakati aliposikia watu wanabisha hodi. Walikuwa vijana wawili. Mmoja alikuwa na kofia kichwani. Rosa hakuwafahamu.

"Shikamoo mzee!" Zakaria hakusikia.

"Mzee, shikamoo! Tunakusabahi," walipandisha sauti. Zakaria aligeuka nyuma kutazama ni kina nani.

"Marahaba. Karibuni." Alijibu kwa upole. Aliendelea na kazi yake.

"Rosa waletee viti wakae," Regina alisema.

Rosa alileta viti viwili. Wale vijana walikaa wakitazama upande wa Rosa. Walikuwa bado wakifikiri namna ya kuanza kuzungumza Zakaria alipogeuka tena na kuwauliza kwa upole.

"Mnataka nini watoto wangu?"

"Mzee sisi tunatafuta mayai ya kununua."

"Ooo! Kumbe mnatafuta mayai tu. Ninayo machache. Ninaweza kuwaleteeni lakini bei ni senti kumi kila yai; siyo senti tano."

"Lete tu mzee, lete."

Zakaria aliingia ndani ya nyumba. Vijana walibaki nje wakitabasamu. Alitoka na mayai matatu mkononi. Walikuwa wakiyapima yale mayai kwa kuelekeza juani hali jicho moja wamefumba waliposhtukia viboko vinalia juu ya miili yao.

"Mnafikiri mimi mjinga! Ondokeni hapa!" Wale vijana walikimbia bila kuangalia nyuma. Walifikiri bado anawafuata. Zakaria aliwasikia kwa mbali wakimtukana.

"Mshenzi, utaoza na binti zako!"

Zakaria hakuwajibu lolote. Regina na Rosa walikuwa wamenyamaza tu.

"Mshenzi, unanizalia wasichana tu! Unaniletea taabu nyumbani bure tu!" Zakaria alifoka.

Regina hakujibu; aliogopa kumdhihaki. Stella aliokota kofia na kuiweka kichwani. Baba yake alimnyang'anya.

Baada ya muda mfupi Zakaria alitulia. Aliendelea na kazi yake. Stella na Honorata walianza kucheza mchezo wa kujificha. Walijificha mvunguni; walijificha nyuma ya nyumba; walijificha jikoni. Sperantia alikuwa akiwatafuta. Alipokuwa akiwapata walijificha mahali pengine. Haukupita muda mrefu Stella akatoka mafichoni akilia. Macho yalikuwa yamemvimba—na pua pia. Manyigu yalimtandika. Wenziwe walimcheka na kumzomea, na huo ndio ulikuwa mwisho wa mchezo.

Siku zilikwenda haraka sana kwa Rosa—livu ilikaribia kwisha. Rosa

alikuwa akimwosha Sperantia ndani ya karai aliposikia mama yake anamwita. Rosa alimwona mama yake amegeuka sura. Baba yake hakuwako nyumbani. Regina alimwambia aende kumwita Bigeyo. Kwa kuwa Bigeyo alikuwa na mgeni—dada yake—alisema kwamba atakuja baadaye. Rosa alieleza ugonjwa wa mama yake. Bigeyo alifahamu. Alikwenda pamoja na dada yake hali wanakimbia. Walimkuta Regina hajiwezi kabisa. Walimbeba kumpeleka nyuma ya nyumba ambako kulikuwa na ua. Wasichana walifukuzwa; waliambiwa wasikae karibu.

Regina alijifungua mtoto wa kiume. Mtoto alimwagiwa maji, alilia. Bigeyo alikimbia huku na huko akipiga vigelegele kwa ulimi. Alikuwa akitupa mikono juu. Wasichana walikuja kuangalia mtoto. Stella aliuliza kwa nini walitaka kumwua mama yake; Stella alikuwa akichungulia na aliona wakimshika mdomo na pua.

Zakaria alirudi usiku nyumbani siku hiyo. Alikuwa amekwishapata habari hizo njema njiani. Alimbeba mtoto. Alimpa pongezi mke wake.

"Regina! Sasa mji huu umekuwa wako."

"Aksante," Regina alijibu akitabasamu. Alijiona ana uwezo wa kuzungumza.

"Zakaria, inafaa uache ulevi."

"Aa mke wangu, unafikiri ulevi ni ugonjwa?" Alinyamaza kwa muda mfupi. "Mume gani asiyekunywa?" aliendelea. "Mtu asiyekunywa hawezi kujulikana kwa watu. Nani humu kijijini asiyemfahamu Maji–Machafu." Hilo ndilo lilikuwa jina lake la ulevi. "Unafahamu mimi nilianza kunywa pombe wakati nilipozaliwa: maziwa yangu yalikuwa pombe. Nikiacha sasa pombe itakuwa kama kujiua."

"Lakini Zakaria inafaa upunguze ulevi. Wengine wanakunywa lakini bado wanaweza kuwatunza watoto wao vizuri na wao wenyewe wanafanya kazi nyumbani."

Zakaria aliguna tu. Alinyamaza. Aligeuza mazungumzo.

"Sijui huko mjini nyama wanauzaje?" Aliuliza. "Nitakwenda kesho mjini, sijui unahitaji nini zaidi."

"Taulo mbili," Rosa alidakia, "Pea mbili za kanga na pembe tatu tano, pia na nguo za matandiko pamoja na chandalua." Zakaria aliandika juu ya karatasi asije akasahau.

Usiku huo Zakaria aliimba aleluya karibu usiku kucha. Kesho yake alikwenda posta. Mke wake alishangaa kumwona jioni anarudi na vitu vyote alivyokuwa ametaja. Alianza kupata sauti. Alianza kuzungumza



kwa furaha. Hata watu wa kijijini waliona ajabu. Lakini Zakaria hakuacha ulevi. Aliendelea kunywa pombe kama kawaida. Aliendelea pia kuwachunga binti zake kama ng'ombe.

Majuma mawili yaliyofuata wanawake wa kijiji walikuja kumpa pongezi. Kila mmoja alikuwa akija na bakuli la unga kichwani. Majirani walifurahi pamoja na Regina. Walimtakia heri na walitumaini kwamba taabu zake zitapungua.

Wakati siku za Rosa zilipokwisha mtoto alikuwa amekwishabatizwa kwa jina la Emmanuel. Alikuwa mtoto mwenye afya nzuri, na nyumbani dada zake walimpenda. Mara nyingi Stella na Sperantia waligombania kumbeba. Rosa alipotaka kurudi shuleni mama yake alimwombea pesa za matumizi. Zakaria alimpatia shilingi ishirini.

# V

Rosa alirudi shuleni. Safari hii aliendelea na mwenendo wake uleule. Lakini kipindi hiki hakikuwa kizuri sana, hasa kwa Rosa. Wanafunzi wa darasa la tisa walianza kuzoea maisha ya pale shuleni. Ugeni ulikuwa umekwisha. Waliporudi kutoka likizoni walirudi wamekwishakuwa wajanja. Walianza fujo ya kuzungumza darasani wakati wa kujifunza. Waliona "Cambridge" ilikuwa mbali.

Waalimu hawakukawia kutambua. Mara nyingine walizungumza kwa sauti za juu vile kwamba walimu wakiwa nyumbani mwao waliweza kusikia. Siyo kelele tu iliyowafanya watambue. Wanafunzi wengi walianza kuwa wanachelewa kupeleka madaftari yao ya kazi walizokuwa wakipewa. Wanafunzi wa darasa la kumi na mbili pia walikuwa wamekwishapeleka manung'uniko yao mbele ya Sista kuhusu kelele. Walimu walianza kuliangalia sana darasa hili. Kila mwalimu wa zamu alizoea kuingia darasani kuwanyamazisha.

Wanafunzi hawakusikia. Rosa aliitwa na Sista John ofisini.

"Rosa," Sista alimwita.

"Sista."

"Lazima uniambie majina ya wanafunzi wanaofanya fujo darasani."

Rosa alinyamaza.

"Rosa. Kama unaogopa kutaja majina yao, andika juu ya karatasi hii."

"Sista, mimi huwa siwaoni!"

"Kwa nini!"

"Mimi huwa ninajali kusoma vitabu tu."

"Haya toka humu! Toka nje! Kesho darasa lenu halina masomo!"

Rosa alitoka nje haraka. Aliona kwamba ilikuwa afadhali kufanya adhabu wote kuliko watu wachache ambao angewataja yeye.

Kesho yake darasa lao halikuwa na masomo. Darasa lote lilipewa adhabu. Wote waliambiwa kuchukua mafyekeo. Sista aliwambia kufyeka majani yote yaliyokuwa karibu na nyumba. Walifyeka hadi saa sita.



Wakati wa kazi wale ambao walikuwa hawafanyi fujo darasani walianza kunung'unika.

"Hatuwezi kuvumilia kufanya kazi kwa sababu ya watu wachache tu. Siku nyingine tutawasema!"

Mwezi uliofuata darasa lilikuwa tulivu. Rosa asingepata taabu tena kama habari fulani zisingemfikia Sista John. Ilikuwa ikisemekana kwamba wasichana watatu wa darasa la tisa walilala siku moja mjini na kwamba walirudishwa asubuhi kwa motokaa bado wamelewa. Sista John alisikia habari hizi siku mbili baadaye kutoka kwa mtu aliyewaona mjini Mwanza.

Siku chache baadaye Sista John alimwomba Rosa ampelekee madaftari ya wanafunzi ofisini mwake. Alipoweka madaftari juu ya meza Rosa alishangaa kusikia Sista John anamwomba kukaa juu ya kiti kwa muda mfupi.

"Rosa," Sista alisema akitabasamu.

"Sista."

"Unaendeleaje na masomo yako?"

"Nafikiri nafanya vizuri."

"Tunafikiri unaweza kusomea usista."

Rosa alinyamaza.

"Rosa, umesikia nini katika siku hizi zilizopita?"

"Sikusikia lolote Sista."

"Rosa, fahamu kwamba tunakuamini sana. Unaweza kuniambia wasichana waliolala mjini?"

"Sista mimi siwafahamu."

Sista alianza kugeuza sura yake.

"Wasichana wengine wanasema kwamba wewe pia u mmoja wao."

"Ah! Sista siyo mimi ni ..." Rosa alinyamaza.

"Usipowasema utafukuzwa shule wewe mwenyewe."

"Sista mbona ni kina..." Rosa alitaja majina matatu.

"Aksante sana Rosa. Unaweza kwenda."

Rosa alitoka nje, jasho limekwishamtoka.

Wale wasichana waliitwa. Kila mmoja wao alipewa adhabu ya kusomba magari mia ya mchanga. Kwa kuwa walipaswa kupeleka mchanga mbali, mwenye nguvu aliweza kufanya ishirini kwa siku. Kazi hii iliwachukiza sana, kwa sababu shule yenyewe ilikuwa karibu na barabara, na wavulana walipokuwa wakipita walikuwa wakiwaangalia sana. Sista alikataza rafiki zao wasiwasaidie. Vidole vyao vilivimba sana. Wen-

gine walishindwa hata kushika uma wakati wa kula. Baada ya juma moja walimaliza adhabu yao. Sasa ilibakia kazi ya kumsaka yule aliyetaja majina yao.

Rosa alifikiri kwamba hatajulikana. Alishangaa sana siku moja alipoingia darasani jioni wakati wa kujifunza kuona kila msichana anamwangalia. Alifunua deski lake kuchukua kitabu, hakuweza kuamini macho yake. Alianza kulia kwa sauti. Daftari zake zote zilikuwa zimetatuliwa vipandevipande. Alipoangalia vizuri ndani aliona kipande cha karatasi. Alikitoa na kukisoma.

"Kumbe ndiyo maana uko mnyamavu namna hii! Ulifikiri tutafukuzwa! Utakatifu wako uko wapi?"

Rosa alikwenda kuwona Sista John. Alimweleza yote yaliyotokea. Alikuwa hajafahamu kwamba hata shuka zake zilikuwa zimechomwa moto.

Kesho yake wale wasichana waliitwa tena ofisini baada ya Sista John kusikia kwamba walichoma hata shuka za Rosa.

"Nani kati yenu ametenda mambo haya?" Sista John aliuliza akicheka kidogo.

"Mambo gani?" Mmoja kati ya wasichana aliuliza.

"Hatuna habari. Kuna mambo yametokea?" Mwingine aliongezea.

"Bila shaka mmekwishasikia juu ya madaftari yaliyopasuliwa na nguo zilizochomwa."

Wasichana walinyamaza. Walionyesha kila alama ya kushangaa. Sista John aliendelea.

"Si jambo baya. Hata mimi mwenyewe nilizoea kufanya hivyo kama mtu akinichongea. Kama mlimchomea nguo zake sioni ubaya. Ujinga wake mwenyewe; mimi sikumwomba aje kuniambia majina yenu. Alikuja mwenyewe humu ndani kuniambia."

"Ndiyo maana hata sisi tulikusudia kujilipizia kisasi," mmoja wao alisema.

"Kwa hiyo mlimchomea nguo?"

"Ndiyo!"

"Na madaftari mkatatua!"

"Ni wazi!"

"Nilifahamu kwamba ni ninyi maana mlimwandikia hata kijibarua hiki."

Sista alianza kutembeatembea chumbani. Alipofika tena mezani



alipokuwa amekaa mwanzoni, alichukua bahasha tatu kutoka kitabuni akawapa, kila mmoja yake. Alianza kugeuka sura.

"Nafikiri tumechoka na matendo yenu. Na huu nafikiri utakuwa mwisho. Utakuwa mwisho kwa sababu mnapaswa kuondoka hapa kabla ya saa sita. Kuna muda mrefu wa kutosha kuweza kupanga vitu vyenu."

Wasichana walilia. Walijigaragaza juu ya sakafu, *"No, no Sister! Sister No!"* Walikatalia ofisini. Walipotambua kwamba ilikuwa kazi bure kulia walikataa kupanga vitu vyao. Lakini jioni kama saa tisa hivi, polisi walikuja kuwakusanya na kuwapeleka kwenye stesheni ya basi. Walisafirishwa makwao. Na huo ndio ulikuwa mwisho wao.

Sista John alimsaidia Rosa kununua vitu vilivyoharibiwa pamoja na madaftari. Ilikuwa kazi ngumu kuandika tena mambo waliyokuwa wamekwishamaliza. Thereza alimsaidia na kama isingalikuwa yeye, Rosa asingalimaliza. Wasichana walikoma kumsumbua Rosa lakini chuki haikwisha. Rosa alichukiwa sana. Alipojaribu kukaa na kuongea na wenziwe walimkimbia na kumwacha peke yake. Rosa alikonda. Alimaliza darasa la tisa kwa shida sana ingawa aliweza kuwa wa nne katika mtihani wa kumaliza mwaka.

Rosa alipoingia darasa la kumi aliendelea bado na tabia yake ile ya kuogopa na kuchukia wavulana. Alipoingia darasa la kumi na moja Rosa alikuwa bado akijifikiria kwamba yeye aliweza kujitosheleza.

Mara chache Rosa alikwenda kutembea mjini Mwanza. Alizoea kwenda kwa basi na kurudi kwa basi. Rosa alikuwa amesimama kwenye kituo cha basi akingojea basi la kwenda Rosary College lifike, na karibu naye kulikuwa na wavulana wawili wakizungumza kwa sauti ya juu. Rosa aliudhika aliposikia jina lake likitajwa. Wale vijana walikuwa hawajamwona. Rosa alisikiliza kwa makini. Alijificha nyuma ya mtu mwingine aliyekuwa karibu.

"Nasikia kwamba msichana huyo hapendi kuzungumza na wavulana!"

"Sijui anajifikiria yeye nani?"

"Nafikiri anamwogopa baba yake."

"Nasikia baba yake mkali sana?"

"Sana! Alitutandika viboko bwana."

"John alikuwa anasema kwamba msichana huyo ni kilema."

"Kweli bwana inawezekana. Hakuna uzuri usio na dosari."

"Kweli bwana inawezekana. Wewe unafikiri msichana anaweza kufika darasa la kumi na moja bila ..."

Rosa hakusikia vizuri maneno yaliyosemwa mwishoni. Aliwaona wale vijana wakipanda basi kuelekea Bwiru. Aliweza tu kubahatisha kwamba walikuwa wanafunzi kutoka shule ya Bwiru ya wavulana.

Rosa alibaki pale amesimama kimya. Maneno hayo yalimkata ini. Yalimsumbua sana moyoni. Alianza kufikiri.

'Huyu John ni nani? Wanasema kwamba mimi kilema! Nimekosa nini? Walikuwa wanamaanisha nini waliposema kwamba mimi kilema. Wanasema baba mkali. Kuna ubaya gani! Si ananilinda!' Hata alipokuwa kitandani maneno haya yaliendelea kuzunguka kichwani mwake. Alikata shauri. Alikata shauri kwenda kucheza dansi.



# VI

Rekodi inawekwa na sanduku linatoa sauti. Mara moja wavulana wanaamka kwenda kuinama. Miungu wadogo wanaweka mikono yao kifuani kuonyesha kwamba wanakataa. Wengi wanakubali. Huu ni wakati wao wa umalaika. Hapa mvulana mmoja mwenye suti anaminamia msichana, msichana anakataa; lakini anapotega mgongo msichana anachukuliwa na mvulana mwingine ambaye hana hata tai. Pale unamwona mvulana mwingine, yeye amekwisha wainamia wasichana watano lakini bado anaendelea—amevaa suruali ya kaki. Ni ajabu mambo yanavyoendeshwa humo ndani. Vijana wanacheza. Wanacheza kila wimbo. Wimbo wa mapenzi, wanacheza. Wimbo wa kifo, wanacheza. Wimbo wenye huzuni, pia wanacheza. Kuna watu wengine ambao si watoto wa shule humo ndani. Wengine ambao si vijana, lakini wanacheza na kofia vichwani mwao. Wasichana wote sasa wamekwishachukuliwa, wamo uwanjani. Lakini upande mmoja kuna wavulana wawili wanabishana.

"Nakwambia ukweli Rosa leo naye amekuja. Alikuwa amekaa papa hapa! Sijui sasa yuko wapi?"

"Kweli anafahamu kucheza?"

"Wapi! Lakini anajitahidi."

"Lazima nimtafute nimwone!"

Anaangalia uwanjani. Anamwona akicheza na mtu ambaye hamfahamu. Hakuonyesha alama za uanafunzi. Kijana anakaa akisubiri rekodi nyingine.

Rosa akiwa mikononi mwa mtu huyo anacheza akitetemeka. Moyo wake unamdunda. Anataka kumwambia aondoe mikono yake kiunoni lakini anashindwa.

"Ningependa kufahamu jina lako," yule mtu anauliza kwa sauti ya chini.

Rosa anataka kuzungumza lakini tena anashindwa kufunua mdomo. Anashangaa kujiona hana nguvu. Anajiuliza kwa nini moyo wake unamdunda. Polepole anaanza kuona kwamba kuna kitu fulani anachokosa. Polepole anaanza kuona kwamba yeye peke yake hawezi kujitosheleza.

Wakati wote wa dansi Rosa anacheza na mtu mmoja tu. Hapendi kushikwashikwa na watu wengi. Polepole Rosa anaanza kumzungumzisha.

"Ulikuwa ukiuliza jina langu?"

"Ndiyo."

"Ningependa kufahamu jina lako kwanza."

"Langu Deogratias."

"Deo—nani?"

"Deogratias."

"Mimi Rosa Mistika."

"Asante."

Dansi inapokaribia mwisho Deogratias anamtoa nje kwa muda. Huko nje Deogratias anamkumbatia na kumbusu mara moja.

"Niache niende!"

"Zungumza polepole." Deogratias anamkumbatia tena.

"Kwa nini una joto sana kuliko wasichana wengine?" Deogratias anauliza. Rosa karibu fahamu zimwishie kichwani. Rosa hafahamu amekaa wapi mpaka anaposikia mtu fulani akitangaza: "Wasichana wote wa Rosary ndani ya basi!" Anapoamka anaona kwamba alikuwa amekaa juu ya magoti. Rosa anapepesuka kwenda basini. Anapofika shuleni wenziwe wanamwambia, "Shuka tumefika." Mawazo yake yalikuwa mbali.

Alipofika kitandani Rosa hakuweza kupata usingizi upesi—alianza kufikiri: 'Kama nikifanya urafiki na wavulana baba yangu atafahamu? Yeye yuko Ukerewe mimi niko Usukuma. Baba anakaa akinichunga, anafikiri yeye atanioa?'

Baada ya muda usingizi ulimchukua. Alimwona baba yake akitembea barabarani na mbwa. Mbwa huyo alikuwa amefungwa kamba shingoni. Mbwa aliona mbuzi. Alikata kamba na kukimbia. Alimrarua mbuzi vipandevipande. Rosa aliamka. Alilala, na usingizi ulimchukua tena. Aliona kijana mwembamba mwenye ndevu nyingi akimtazama kwa macho yanye huruma. Rosa alipomwona alimkimbilia na kumkumbatia akisema kwa sauti, "Lazima unioe! Ukinikataa wewe maisha yangu yamekwisha; sina tumaini tena!" Rosa alitokwa na machozi. Mvulana alimbusu na kumwambia, "Nitakujibu baadaye kwa barua; lakini unafikiri baada ya ku..." Rosa aliamka tena. Sasa usingizi ulimruka kabisa. Aliamka na kuvaa gauni lake. Alikwenda katika chumba cha Thereza. Thereza alishangaa kumwona usiku namna hiyo. Ilikuwa kama saa kumi na nusu za usiku.



**"Unaweza kunisaidia, Thereza!" Rosa alisema sauti ikimtetemeka. Thereza alikuwa bado hajaelewa Rosa alipomrukia na kumkumbatia. Waliangushana kitandani. Rosa alianza kumbusu, lakini tamaa yake haikuweza kupungua. Rosa alihitaji ule mkwaruzokwaruzo wa aina ya pekee. Mkwaruzokwaruzo wa ndevu na manyoya ya tumboni. Zaidi ya hayo moto ulikuwa ukiwaka upande wa kusini lakini wao walikuwa wakizimisha upande wa kaskazini.**

**Asubuhi macho ya Rosa yalikuwa bado mekundu. Alipomaliza kuosha uso wake alianza kutafuta zile barua alizokuwa amekwishaandikiwa na wavulana. Hakuzipata zote, lakini zile alizopata alizisoma tena. Hakuweza kufanya lolote sasa: hakufahamu wavulana hao walipokuwa; hakufahamu kama walikuwa bado na nia naye; licha ya hayo, barua hizo zote alikuwa amekwishazijibu: "Samahani kaka, mwenzio sijiwezi; jaribu mahali pengine!" Alianza kulia. Alichukua mfuko wake wa mkononi kutoa kitambaa cha kujipangusia machozi. Alikuta barua fupi mle ndani. Alikumbuka kwamba mfuko huo alikuwa nao dansini usiku. Barua yenyewe ilikuwa ya mapenzi na ilikuwa ikimwomba kidole cha pete.**

**Rosa aliona kwamba hawezi kupoteza bahati yake. Alifikiri kwamba mwanamume wa kwanza kuonyesha mapenzi ndiye yeye atakayemwoa. Rosa alikubali. Aliijibu barua hiyo kwa upole sana. Rosa sasa alianza mapenzi. Alianza mapenzi lakini aliyaendea haraka sana kama mbwa aliyekata kamba. Aliona mvulana mmoja au wawili walikuwa hawamtoshi kwa urafiki. Mwaka huohuo aliwakubalia wavulana watano. Thereza aiipomtembelea siku moja alishangaa kuona faili zima la picha na faili jingine la barua.**

"Unafahamu, Thereza, siku hizi ninawachezea wavulana kama mtu aendeshaye punda. Vuta kamba mkono wa kulia na punda atakata kona: vuta mkono wa kushoto, pia atakata. Punda hafahamu aendapo isipokuwa mwendeshaji tu. Ndivyo hivyo ninavyowachezea wavulana siku hizi. Vijana hawa hawafahamu mwisho wao. Angalia: huyu hapa ana makengeza lakini bado ananinyemelea. Juzijuzi alinitumia shilingi hamsini. Ujinga wake, mimi sikumwomba. Huyu hapa mwenye miwani ni mzuri lakini ana vidole sita mkononi. Anapoteza muda wake. Huyu hapa ni mrefu sana. Mimi ninakomea kiunoni tu ninaposimama naye. Hata kama akinioa nitakuwa nikiona haya kutembea naye. Huyu hapa mzuri sana lakini hafahamu mapenzi. Huyu anaona wivu sana. Mimi sipendi wanaume wa namna hiyo."

Mwishowe aliifikia ile picha aliyokuwa akiipenda. "Huyu hapa mwenye kofia kichwani jina lake Deogratias; anasoma shule ya wavulana ya Bwiru. Tulikuwa naye siku ile ya dansi. Huyu ndiye anaweza kunioa, natumaini."

Thereza aliangalia kwa mshangao. Rafiki yake aliyekuwa akimwona mjinga zamani, katia fora. Lakini kwa kuwa aliona kwamba alikuwa akitishwa alianza kusema.

"Mbona kama mimi ningalikuwa nataka ningekuwa na arobaini sasa; lakini wengine nimewakataa nimebakiza wawili tu," Thereza alikuwa akitaka kumtishia rafiki yake. Lakini alikuwa akisema ukweli. Alikuwa amekwisha jifunza mengi kuhusu wavulana. Thereza aliendelea kuzungumza.

"Sijui mavulana mengine yakoje! Kuna mvulana mmoja nimekwishamjibu vikali kwamba simtaki! Kwamba sitampenda hata kwa mizinga! Lakini yeye anajibu: 'Aksante sana kwa barua yako: hiyo ni alama ya mapenzi.' Mimi nimekwishachukizwa."

"Hivi kijana mwenyewe anatoka wapi?" Rosa aliuliza.

"Wanasema sijui ni jitu la wapi—lina miguu mirefu kama mbuni!"

"He he he he!" Walicheka pamoja.

"Ajabu kama hadithi ya kinyonga! Unafahamu hadithi hiyo Thereza?"

"Sifahamu."

"Kinyonga alikuwa akimchumbia msichana. Baba alikataa na kumwambia kinyonga: 'Kinyonga nenda zako, huyu binti huwezi kumwoa!' Kinyonga hakuamini. Alikwenda akitazama nyuma hata mwishowe macho yake yakaweza kupinduliwa pande zote."

Walicheka tena wote pamoja.

"Wavulana wengi ni kama kinyonga," Thereza alisema.

Thereza aliona kitambaa juu ya meza.

"Hiki kitambaa unamfumia nani?" aliuliza.

"Ninamfumia *boy* wangu D," Rosa alijibu kwa fahari.

"Umekwishamwona *boy* wa somo yako?" Thereza aliuliza tena.

"Sijamwona!"

"Ni mzee! Hakika unaweza kudhani ni baba yake!"

"Sijui kwa nini somo anampenda."

"Wanasema kwa sababu huyo mzee ana motokaa."

"Sijui masichana mengine yakoje!" Rosa alishangaa.

"Umekwishamwona Mary anatembea?" Rosa aliendelea.



"Ukimwona anatembea utashangaa—anatembea ameacha kiuno chake nyuma, utafikiri eropleni inataka kutua."

"Mimi ninamjua fulani, anatembea anachezesha kiuno chake. Sijui labda anataka wavulana wamtamani zaidi!"

Mazungumzo yao yalikatishwa na kengele ya kuingia madarasani kujifunza.

Wakati huu wasichana walikuwa wameshamshangilia sana Rosa. Aligeuka kupindukia. Katika mtihani wa kuingia darasa la kumi na mbili alikuwa wa ishirini. Alianza kupoteza muda wake mwingi siyo tu kwa kufuma na kushona vitambaa, lakini sasa alianza mara zingine kuwa analala mjini. Masista walishangaa kumwona Rosa anatelemka sana katika mitihani yake. Lakini Sista John alikuwa amekwishavumbua. Alikuwa amekwishasikia juu ya tabia na matendo yake nje. Siku moja alipoletwa kutoka mjini kwa gari la mtu aliyeonekana kuwa mwenye cheo, Rosa alishangaa kumkuta Sista John akimngojea. Alikuwa amepigiwa simu.

"Utaniona kesho asubuhi ofisini," Sista John alisema kwa ukali. Usiku mzima Rosa alilala akifikiri atakwenda kusema nini mbele ya Sista.

Asubuhi Rosa alipoingia ofisini alikuwa anatetemeka kwa hofu. Sista John siku hiyo hakucheka wala hakuwa na haja ya kumzungumzisha maneno mengi.

"Rosa," Sista aliita.

"Sista."

"Nani aliyekuleta kwa gari?"

"Rafiki yangu. Anafanya kazi benkini."

"Una rafiki mwingine?"

"Ndiyo."

"Nani?"

"Deogratias"

"Deogratias! Deogratias! Rosa, tumekusudia kukupeleka nyumbani. Utarudi tu kufanya mtihani wako wa Cambridge."

Rosa alilia. Lakini Sista John akisema amesema. Alikuwa akifanya kazi yake.

Rosa alikwenda nyumbani. Alipofika nyumbani aliwambia wazazi wake kwamba akili zilimzidi kichwani, kwa hiyo aliambiwa kwenda nyumbani kupumzisha kichwa. Wazazi wake walishangaa kumwona Rosa anapumzika muda wa miezi miwili bila kurudi shuleni. Wasichana wenzake walipokuja likizo waliwatolea wazazi hadithi yote ya Rosa.

Wazazi walisikitika sana: walitegemea kwamba Rosa atawachukua katika maisha yao ya siku za usoni. Regina alisikitika zaidi.

Mwenendo wa Rosa ulimfanya Zakaria ajitahidi zaidi katika kazi ya kuwachunga binti zake. Flora alikuwa sasa shule ya wasichana ya Mwanza. Alikuwa darasa la kumi. Alipokuwa anakuja likizo alikaripiwa kwa maneno ya kuogopesha na matusi. Honorata sasa alichungwa vikali na alizuiwa kuzungumza na mvulana yeyote. Emmanuel alibembelezwa na kutunzwa vizuri sana. Baada ya kupoteza mtoto mvulana kati ya Rosa na Flora, Regina aliona hawezi kumpoteza Emmanuel kwa kutomtunza vizuri.

Rosa alipofukuzwa shuleni rafiki zake hawakukawia kusikia. Wote walisikia sifa yake mbaya. Waliambiwa kwamba alikuwa akilala mjini, na kwamba alikuwa akiletwa shuleni na maafisa kwa motokaa. Wengi waliposikia walitafuta anwani yake ya nyumbani na kumwandikia barua. Walimpa pole. Rosa aliona kwamba wengine hawakumwandikia barua tena, hata baada ya miezi. Polepole Rosa alianza kuwapoteza rafiki zake. Alipoangalia faili lake la picha alikasirika na kuzichoma zote isipokuwa moja—ya Deogratias. Deogratias aliendelea kumwandikia Rosa barua karibu kila juma. Alisifia sana uzuri wake. Rosa alikaza kamba kwa kujibu barua zote alizoandikiwa na Deogratias.

Siku moja Rosa alipata barua ndefu sana kutoka kwa Deogratias. Rosa alipoisoma alifurahi sana: aliona maisha yake kwa vyovyote yatatengamaa. Ndani ya barua Deogratias alimwambia asiwe na shaka. Alikuwa tayari kumwoa wakati wowote. Alimtumia shilingi mia tano za kumsaidia wakati akiwa nyumbani. Alimjulisha pia kwamba alikuwa tayari kuwaona wazazi wake kwa jambo la ndoa. Rosa alipomaliza kuisoma barua hiyo aliibusu na kuiweka ndani ya faili. Chumba alichokuwa akilala pamoja na dada zake kilikuwa kimejaa picha za Deogratias. Mbili zilikuwa ukutani juu kwenye kichwa cha kitanda; moja ilikuwa kwenye miguu ya kitanda, ukutani; na moja ilikuwa chini ya mto. Rosa alimpenda kweli mchumba wake.

Alipokuwa nyumbani alipata muda wa kusoma asubuhi tu—jioni alimtembelea Bigeyo. Kwa hiyo barua ilipofika kutoka shuleni ikimjulisha tarehe ya kuanza mtihani, Rosa alijiona ana machache sana kichwani. Hata hivyo alikusudia kujaribu. Alipofika shuleni Thereza alimpokea kwa furaha sana. Thereza alianza kumsimulia rafiki yake juu ya masomo.

"Unafahamu Rosa, mwalimu wa historia alivumbua baadaye kwamba alikuwa akitufundisha mambo ambayo yalikuwa hayahitajiki sana katika



mtihani!" Thereza aliendelea kumsimulia juu ya masomo yote. Alimletea madaftari yake ili ajifunze kwa muda wa majuma matatu yaliyokuwa yamebaki.

Mtihani wa historia ulipofika Rosa aligeuzageuza karatasi lakini hakuona swali lolote aliloweza kuandika zaidi ya ukurasa mmoja. Mwishowe alichagua maswali manne. Alianza kuandika kitu fulani kama historia. Siyo historia tu iliyokuwa ngumu. Rosa aliona masomo yote magumu isipokuwa Kiswahili.

Majibu ya mtihani yalipokuja Rosa alijikuta ameshinda masomo matatu—Swahili, Needle Work na English. Alipewa cheti cha kundi la tatu. Thereza alipata cheti cha kundi la pili. Rosa alifurahi kuona amewazidi wengine waliokuwa pale shuleni muda wote wa masomo. Thereza alichaguliwa kuendelea darasa la kumi na tatu katika shule ya wasichana ya Jangwani. Rosa alichaguliwa kwenda Morogoro TTC. Alifurahi. Zakaria na Regina walifurahi pamoja naye.

# VII

Zakaria alikuwa mkali sana katika mambo ya malezi ya binti zake lakini alipenda sana binti zake waolewe upesi iwezekanavyo. Kwa hiyo aliposikia kwamba Rosa alikuwa amekwishapata mchumba alifurahi. Alitaka kupunguziwa mzigo begani. Wakati huu alizoea kusema, "Kuzaa wasichana taabu sana! Unapata wageni wa kila aina: wageni wanaopita tu nyumbani na kuuliza—njia ya kwenda kwa fulani iko wapi? Wageni wanaopita nyumbani kunywa maji tu na kwenda." Kweli wasichana watano walikuwa wengi na vijana sasa walizoea kuita mji wake *Zoo*.

Zakaria na Regina walikuwa wakimgojea mgeni kwa hamu. Walianza kufikiri, "Akija atalala wapi?" Mgeni—mkubwa na mwenye heshima namna hiyo— kulala naye ndani ya nyumba moja isiyo na vyumba vingi lilikuwa jambo la aibu. Mwishowe walikata shauri kwamba akija watamwomba alale chumba cha maongezi. Hata binti zake wengine pia walikuwa wamekwishasikia kwamba mgeni fulani atafika nyumbani—mchumba wa Rosa walisikia.

Deogratias kuingia humo. Walimaliza siku mbili humo bila kesi yao lani—alisema Deogratias. Deogratias alipofika nyumbani alitendewa mema yote. Kila siku kuku mmoja alikatwa shingo na alipewa muda mrefu kuweza kuzungumza na mchumba wake. Isipokuwa jambo moja halikuwapendeza sana wazazi wa Rosa: Deogratias alivunja sheria fulani za Kiafrika—kweli Deogratias hakuzifahamu sheria hizo. Deogratias alikula na kofia kichwani na alikuwa hatoi kofia yake kichwani hata wakati akiwasalimu wazee.

Wakiwa katika mazungumzo na mzee siku moja, Deogratias aligusia swali la mahari. Swala hilo lilizungumzwa jioni wakiwa wamekaa kuzunguka moto.

"Aaa mtoto wangu," Zakaria alisema, "Swali la mahari tumekwishalifikiria, mimi na mke wangu. Kwa sasa siwezi kukupatia jibu kamili, lakini kuna mambo mengine ambayo ninaweza kukwambia sasa



ili uanze kujitayarisha mapema. Kwa mfano—bila shaka hutashangaa sana—tunahitaji nyumba." Alionyesha nyumba yake kwa mdomo. "Ukiweza kunisaidia paa mimi mwenyewe kumalizia na kuanza sitashindwa. Pia tumeshakata shauri kwamba utatoa ng'ombe wanne, mbuzi wawili, kinu, viti vitatu, na shilingi elfu moja. Nimeongezea debe moja la pombe ya moshi kwangu mimi binafsi."

"Hilo ni jambo rahisi. Sisi kwetu tunalipa ng'ombe thelathini, hata zaidi."

"Bado! Usifikiri huo ndio mwisho," Zakaria alidakia. "Nitakutuma kwa jamaa zangu wote, pia kwa jamaa za mke wangu. Lazima ukawaombe mtoto, maana mtoto si wangu peke yangu. Wanaweza pia kuongezea mahitaji yao."

"Yote hayo ni sawa tu, nitafanya."

Kesho yake jioni Zakaria alikusudia kumtembeza mgeni wake. Deogratias hakupinga; ilikuwa mara yake ya kwanza kufika Ukerewe. Zakaria hakumpeleka mahali pengine. Alimtembeza kule alikofahamu. Alimwingiza ndani ya chaka lililokuwa likitoka moshi—moto ulikuwa ukiwaka mle ndani—na sauti za watu ziliweza kusikika. Deogratias alifahamu. Alikuwa pia mkata maji. Alikata maji kama mtu mzima. Walikunywa mpaka usiku. Usiku ulipoingia watu walikuwa hawasikilizani tena. Walikuwa sasa wakizungumza kwa sauti ya juu kana kwamba walikuwa majumbani kwao. Deogratias alistukia watu wanakimbia ovyo kutoka chakani. Alikuwa bado akishangaa aliposikia amri inatolewa:

"Kamata! Kamata! Simama! Simama!"

Chaka lote lilikuwa limezungukwa na polisi. Deogratias alikuwa mle ndani bado pamoja na watu wengine watatu. Hawa walikuwa wamevua nguo za kifuani ili wasionekane. Wao walikuwa wamelala chini. Tochi ya polisi ilipowaka hata sisimizi aliweza kuonekana. Zakaria alikuwa hayumo. Deogratias na wale wengine walishikwa. Walivikwa pingu na sasa walionekana kama wapiga marimba. Deogratias alianza kujililia:

"Mimi mgeni mnihurumie!"

Makofi mawili yalimwangusha chini. Alizimwa kwa kiatu kifuani na tumboni. Damu ilimtoka puani palepale. Alilia kikwao.

"Washenzi, ninyi ndio mnatuharibia nchi. Mnatufanya tutembee usiku! Utakuwa mgeni wetu leo!"

Wale wote walioshikwa walishurutishwa kutembea kwa miguu mpaka bomani—umbali wa maili sita. Kwa kuwa Deogratias alionekana kuwa mtu safi aliambiwa kubeba debe la moshi kichwani mpaka bomani.

Walipofika huko walilazwa gerezani. Ilikuwa mara ya kwanza kwa Deogratias kuingia humo. Walimaliza siku mbili humo bila kesi yao kusikilizwa. Mwanzoni Deogratias alikuwa akitema kila wakati. Aliomba aonane na mkuu wa wilaya, lakini askari jela hawakusikiliza ombi lake. Nyumba ya gereza ilikuwa na chumba kimoja kidogo sana pamoja na dirisha moja. Humo ndani kulikuwa na watu wengine. Pembeni kulikua na ndoo moja kubwa, nayo ilikuwa imejaa. Ilikuwa imeandikwa "W.C." Upande mwingine kulikuwa na blanketi moja kubwa, nalo lilikuwa na madoadoa mengi meusi. Blanketi hilo lilikuwa kavu kama kuni. Mwanzoni Deogratias hakupenda kulitumia ili kujifunika. Baada ya siku moja ndiye alikuwa wa kwanza kuvuta blanketi hilo na kujifunika ingawa lilikuwa likimkwaruzakwaruza. Mtu mmoja alimwuliza Deogratias. Alimtambua. Alikuwa amekwishamwona siku moja Mwanza.

"Hivi wewe "staff" umeletewa nini humu?"

"Tulishikwa tunakunywa pombe ya moshi," Deogratias alijibu "tena mimi nilikuwa mgeni. Nilikuja kuonana na mchumba wangu."

"Hilo ndilo kosa la kukuleta humu! Ha ha ha! Utakuta mchumba wako amekwishaolewa. Mimi niliiba shilingi elfu ishirini na baada ya kifungo changu nitazikuta tu. Ha ha ha! 'Mimi nilikuwa mgeni.' Umepata kilichokuleta huku. Kweli wewe ulikuwa bado kuoa?"

"Bado." Deogratias alijibu.

Watu walimcheka kiasi cha kushikilia mbavu. Deogratias sasa hakuwa na kofia. Nywele nyeupe—ingawa hazikuwa nyingi—ziliweza kuonekana. Siku tatu alizokaa mle ndani zilimfanya Deogratias akonde. Alipoletwa mbele ya hakimu kuhukumiwa alionekana kuwa mzee zaidi. Siku hiyo Rosa na wazazi wake walihudhuria. Deogratias alijulikana. Alihukumiwa kufungwa miaka miwili. Wengine walihukumiwa mwaka mmoja tu.

Rosa hakupata kufahamu zaidi juu ya Deogratias mpaka siku aliyofunga safari kwenda Morogoro TTC. Hapo ndipo alipokata shauri kuchoma barua na picha zote za Deogratias. Akiwa botini kwenda Mwanza alisikia wanawake wawili wakizungumza.

"Huyu ndiye Rosa aliyemfanya Deogratias akafungwa."

"Yule Bwana Maendeleo wa Mwanza!"

"Ndiyo, huyohuyo."

"Mbona yeye mzee wa miaka arobaini?"

"Si ameoa, ana wanawake wawili, wote wasichana."

"Nasikia alikuwa amekwishawapa mimba watoto wawili wa shule?"



"Ndiyo, lakini aliwapa shilingi wasimseme. Walitaja vijana wengine waliokuwa wakisoma nao."

Rosa alisikia mengi zaidi alipofika mjini Mwanza. Hadithi yote ya Deogratias aliisikia. Deogratias alikuwa mmoja kati ya wale wazee wanaojifikiria bado vijana. Wazee wanaopendelea kutembea na vitoto vidogo—hata vile vinavyoanza kuota maziwa. Watoto wao wa kuzaa. Wazee wasioona aibu. Wazee wanaomezea mate matiti ya mtoto mdogo. Wale wazee wanaopoteza bado muda wao katika mambo ya anasa kama dansi badala ya kukaa nyumbani na kuangalia watoto wao. Wazee wanaopenda kukaa katika makundi ya vijana. Akiwa na umri wa miaka arobaini na miwili alikuwa bado akiwaandikia wasichana barua akisema, "Ninakupenda kama almasi ya Mwadui." Alikuwa kati ya wale wazee wanaochukiwa na vijana. Utasikia mara nyingi vijana wakisema, "Wazee hawa wanatufujia!" Huyu ndiye alikuwa Deogratias: Bwana Maendeleo, mchumba wa Rosa.

Zaidi ya hayo, Deogratias alikuwa mmoja kati ya wale watu watumiao vyeo vyao na pesa kwa kupata chochote wapendacho. Utawasikia mara nyingi wakipiga kelele juu ya jukwaa, utafikiri mwisho wa dunia. "Watoto wa siku hizi mmetuchosha! Mnatembea ovyo! Tangu leo mvulana yeyote akionekana anatembea na mtoto wa shule atawekwa nguvuni! Atawekwa nguvuni! Mtu yeyote akimpatia msichana mimba atazidi kujililia mwenyewe!"

Wakishuka kutoka jukwaani utaona baadaye benzi zao zikipeleka watoto "beach." Wazee wa mabinti hawa hawana la kusema. Watasema nini hali mkubwa amekwishapenda? Mpiga ngumi ukuta hujiumiza mwenyewe. Kijana gani atawazungumzia wasichana hao? Nzi hatui juu ya damu ya simba. Habari zilivuma kwamba Deogratias aliwahamisha wazee wawili kutoka Mwanza kwa sababu ya kupinga asiwachukue binti zao. Vijana wengi walitafutiwa sababu za kuwekwa jela.

Deogratias alipenda sana dansi, hasa zile za watoto wa shule. Alizoea kwenda na kofia. Hivyo ndivyo alivyohimiza maendeleo—dansi pia ni aina fulani ya maendeleo. Hivyo ndivyo alivyowatafuta wale wenye joto bado. Kwa wakati huu alikuwa akihitaji mwanamke wa tatu na bahati alikuwa amekwishaipata. Ilikuwa siku ya kwanza Rosa kushikwa mikononi mwa mwanamume yeyote. 'Malezi mema' yalimfanya apende yule mwanamume wa kwanza kuonana naye.

Deogratias alikuwa amekatazwa na wake zake asiende Ukerewe kumwona mchumba wake, lakini baada ya kubishana nao na kuwaambia kwamba atarudi upesi alikata shauri kwenda kisiwani licha ya man-

ung'uniko yao kwamba walikuwa hawahitaji Mkerewe ndani ya nyumba. "Wakerewe wagomvi," walisema. Deogratias alifika Ukerewe na alikipata alichokitafuta.

Mjini Mwanza Rosa alikaa siku tatu. Baada ya kusikia hadithi ya Deogratias alikusudia kwenda kujifurahisha kidogo ili asahau msiba alioupata. Alikuwa akijituliza moyoni mwake kwamba wanaume wamejaa. Rosa aliingia *bar* moja iitwayo "Green Bar." Humo ndani aliona mengi: ujanja wa wanawake na ujinga wa wanaume; unyonyaji wa wanawake na unyonywaji wa wanaume.

Rosa alipata meza yake peke yake pembeni kabisa. Hapo alikaa akinywa chupa yake ya Kilimanjaro kwa raha. Karibu na meza yake walikuwa wamekaa vijana wawili. Mmoja alikuwa amekwishalewa sana: alikuwa ameweka kichwa chake juu ya meza. Mwingine alikuwa hajalewa kiasi hicho. Mwanamke mmoja, kijana mfanyakazi wa humo, alikuwa amekaa juu ya magoti yake; alikuwa akimpapasapapasa kiuno na maziwa—lakini wanawake hawa wamezoea vile kwamba hawasikii lolote. Kuzunguka meza hiyohiyo tu kulikuwa na wanawake wengine sita—nao pia wafanyakazi wa humo. Chupa zilikuwa zimejaa hapo. Martini na Cinzano pia zilikuwapo. Baada ya muda kitambo yule kijana alimwamsha mwenzake ili waende, watoke ndani ya *bar*. Rosa alisikia vijana hao wakisema:

"Lakini msitudanganye! Kesho tutakuja kuwachukua."

"Sisi ni mali yenu tu!" walijibu pamoja, msemo wao wa kawaida. Wale vijana waliyumbayumba kwenda zao kulala. Hapo ndipo Rosa alipoona wale wanawake wakipeana mikono hali wakicheka.

"Heko mwenzangu! Tumewatengeneza! Tumetumia zaidi ya shilingi mia ishirini! Kesho watamparamia nani!"

Baada ya kisa hiki kijana mmoja alikwenda kukaa meza moja na Rosa.

"Unatumia nini dada yangu!"

Tusker, Rosa alijibu bila kuchelewa.

"Tusker" moja iliagizwa kwa ajili yake. Rosa alikunywa chupa tatu. Alimwambia kijana aje kumchukua kesho yake namba mbili "Banda Street."

"Fika kesho tu kaka yangu. Utaona ninavyonoga!"

Rosa alifunzwa na wale wanawake. Rosa alifahamu siku yake ya kuondoka kwenda Morogoro. Kesho yake aliondoka. Rosa alifahamu mengi, kweli alifahamu mengi—alifahamu mapenzi na unyonyaji. Mapenzi ya mwanamke mara nyingi huenda pamoja na unyonyaji. Yule kijana alifika "Banda Street" namba mbili. Hata kiwiliwili chake kilimcheka!



# SEHEMU YA PILI

# VIII

Morogoro TTC ilikuwa shule yenye majengo mazuri sana wakati Rosa alipoingia. Wanafunzi walikuwa wachache. Kila mwanafunzi alikuwa na chumba chake. Wasichana walikuwa wachache zaidi ya wavulana. Rosa alipotika hakuwa na nia tena ya kutafuta mchumba. Kitu kimoja kilimwangusha Rosa—alipenda kupendeza kila mvulana. Kati ya wasichana, Rosa ndiye alikuwa wa kwanza kujulikana. "Msichana huyu mpole na mchangamfu sana!" Utasikia wavulana wakisema. Aisifuye mvua imemnyea. Rosa alijulikana kwa kila mvulana. Alipokuwa akitoka katika chumba cha mvulana, kila mara nguo nyeupe ya ndani ilionekana chini ya gauni, na yeye mwenyewe akijitazamatazama.

Rosa alikuwa wa kwanza kujulikana. Sasa alikuwa wa kwanza pia kupenda chumvi nyingi ndani ya mboga na kula vitu vya ajabuajabu. Wasichana ndio walikuwa wa kwanza kumtambua, halafu wavulana. Hayawi hayawi huwa—Rosa alilazwa hospitali mahututi kwa kutoa mimba ya miezi miwili. Wengine waliokuwa maskini katika mambo haya walianza kusema, "Labda bwana, inawezekana alikuwa na mimba, eti bwana!" Rosa alikaa hospitali muda wa majuma mawili. Wavulana walimwombea apone upesi.

Rosa alipona. Aliendelea na mchezo wake. Katika majuma mawili yaliyofuata Rosa alikonda sana. vijana walikuwa wakimzungumzia yeye katika vikundivikundi; hata yeye mwenyewe alifahamu. Alianza kuwa anaviziavizia vikundi hivyo ili afahamu wanasema nini juu yake. Siku hazikupita alipokuta vijana wakiangalia gazetini. Alijificha. Alisikia maneno waliyokuwa wakisema.

"Staili hii bado sijaitumia."

"Kwa nini bwana usiende *Lab.*"

"*Lab* kwenyewe ni wapi?"

Rosa alisikiliza mpaka mwisho wa mazungumzo yao. Kufuatana na mazungumzo hayo, Rosa aliweza kuelewa kwamba walikuwa wamembandika jila la "Laboratory," yaani nyumba ya kufanyizia majaribio. Ukichanganya dawa hii na dawa hii unapata matokeo haya; ukiweka

dawa nyingi unapata matokeo mengine. Rosa aliitwa "Lab" kwa kifupi. Rosa hakujali. Jina hili halikumsumbua hata kidogo. *"Kama Mola hapendi ni kazi bure, watasema watachoka!"* Rosa sasa alizoea kuimba.

Pale Morogoro, Rosa alikuwa hapati barua nyingi zenye *stamp*. Kama alipata barua yenye *stamp* alifahamu ilitoka kwa Thereza. Barua yenye *stamp* aliyoipata ilimshangaza; ilimfanya aifungue upesiupesi: ilikuwa imeandikwa "Kwa Roja" juu ya bahasha. Ndani, mwandiko ulikuwa hausomeki vizuri. Ilikuwa kana kwamba iliandikwa na mtu aliyesoma chini ya mti katika shule ya wazee.

*Namagondo*
*P. O. Box —*
*NANSIO (Bukerebe)*

*Kwa mtoto wangu Rosa,*

*Nimesikiya kwamba ulikuwa musibitali umejifungua mtoto wa kiume. Mimi Regina pamoja na mlevi wangu tunamshukuru Mungu. Sisi benyewe hatukujaliwa batoto bengi ba kiume. Wewe umejifungua mutoto wa kiume, tunafurahisha sana. Tunakwishafutafuta jina la mutoto huyo. Utamwita Bagaile. Muntu huyu alikuwa ni baba yake mudogo. Alijama na mtumbwi gwake wakati akisafili kwenda Mwanza. Manueli mjima, siku hiji si mweupe kama jamani.*

*Mimi,*
*Regina Mama Yako.*

Rosa aliikunjakunja na kuitupa ndani ya kapu la taka.

Mama yake, baada ya kusoma chini ya mti katika masomo ya watu wazima, alijitahidi kumwandikia mtoto wake barua. Alitumia muda mrefu sana kuandika barua hiyo baada ya kuambiwa na mtu mmoja kutoka Dar es Salaam kwamba Rosa alikuwa amekwishajifungua. Mtu huyo alipita Morogoro ndani ya basi akielekea Ukerewe. Kwa kuwa basi halikukaa Morogoro muda mrefu hakuweza kusikia habari kamili. Juma moja baadaye Rosa alipata barua ingine kutoka kwa dada yake, Flora. Flora alimpa pole dada yake. Flora naye—huko shule ya wasichana ya Jela (hili lilikuwa jina la utani la shule ya wasichana huko Mwanza iliyokuwa inalindwa na polisi) alikuwa amekwishatoa mimba. "Mimba tu haiwezi kunifanya nikajiharibia maisha yangu kwa kuacha shule," Flora alimalizia barua yake.



Maisha ya binadamu ni kama mti. Mti unahitaji maji, hewa na mwanga. Kama mti ukinyimwa mwanga wa kutosha na miti mingine, utarefuka. Utajaribu kupita miti yote ili upate mwanga. Zakaria aliwanyima binti zake mwanga wakati ule walipokuwa wakiuhitaji sana. Aliwapiga; aliwakataza kuzungumza na mvulana yeyote. Nao, kama mti walijaribu kujirefusha ili wapate mwanga, na walirefuka kweli; kiasi cha kutoweza kuonywa na mtu yeyote. Kama ni watoto wasichana, mara nyingi utakuta mama anajenga baba anabomoa; kama wavulana, baba anajenga mama anabomoa. Haya yote hutokea kwa sababu ya kutofahamu wapi mama atawale zaidi, na wapi baba atawale zaidi. Dunia imegeuka, nasi ndio twaigeuza. Tukubali kwamba wakati wa kumtunza binti ndani ya nyumba na kumpaka mafuta umekwisha. Huu si ulimwengu wa kuambiwa, "Ulimwengu uko hivi na hivi." Huu ni ulimwengu wa kutoka nje; ona, amua, na tenda.

Rosa alitoa tena mimba alipoingia katika mwaka wake wa pili. Wengine walisema kwamba ilikuwa mimba ya tatu; wengine walisema kwamba ilikuwa ya nne.

Rosa sasa alikuwa amekwishajulikana Morogoro nzima, hata mjini. Mwishowe sifa yake iliwafikia mapadri wa pale. Padri mmoja alitumwa kwenda kumwonyesha tena mwanga wa wokovu. Padri alipofika pale shuleni aliuliza chumba cha Rosa. Alisikia kijana mmoja akisema kutoka dirishani, "Anauliza nini huyo! Lab? Mpeleke bwana!" Padri hakuweza kuelewa. Aliongozwa mpaka chumba cha Rosa. Rosa alikuwa akisoma daftari lake aliposikia hodi mlangoni. Rosa alifungua mlango na Padri aliingia, Biblia yake mkononi. Rosa alifunga mlango.

"Samahani kwa kukupotezea muda wako," Padri alisema hali ameweka mkono wake kifuani. Aliangalia mezani. "Oo! Ulikuwa ukisoma!"

Daftari la Rosa lilikuwa bado mezani. Lilikuwa limefunuliwa. Padri alilichukua; alianza kupitisha macho yake akisoma vichwa tu vya maneno. Humo ndani alikuta mambo ya ajabu. Rosa alikuwa ameandika habari nyingi kuhusu watu: "Wanawake wafupi... wanawake warefu... Jinsi ya... Namna ya kufahamu kwamba mvulana anakupenda... Namna ya kuweza kuzaa mtoto wa kiume au wa kike... Staili zifaazo..." Vichwa hivi vyote vilikuwa vimeelezwa kinaganaga. Mwishowe Padri alifikia ukurasa aliokuwa akisoma Rosa wakati alipoingia. Padri alisoma ukurasa huu.

"Je, utumiaji wa vidonge vya mimba hauwezi kupunguza tamaa ya mwanamke? Ndiyo, unaweza. Mara nyingi kwa wanawake wengi tamaa ya kujuliana na wanaume hupungua. Lakini uzuri wa vidonge hivi ni kwamba ile hofu inayowasumbua wanawake—hofu ya kupata mimba isiyohitajika—inaondolewa kabisa. Na kwa kuwa tamaa ya mwili inaletwa hasa na moyo wa kuhitaji jambo fulani kuliko joto la damu, mwanamke hana haja ya kuogopa, kwani moyo wake utakuwa umetulizana, bila hofu. Kusema kweli, kwa wachumba wengi au wale ambao wamekwishaoana, vidonge hivi vya dawa vimewaletea usalama ambao umewaongezea furaha ya mwili. Watu wanaweza kutumia staili nyingi, lakini mapenzi yao yatapungua. Vidonge vya dawa havitapunguza mapenzi kamwe. Hakuna sababu ya mwanadamu mwenye akili kuamini kwamba utumiaji wa vidonge vya kuzuia mimba unaingilia utaratibu wa ulimwengu kuliko mimba zitokeazo, mimba baada ya mimba—mimba zisizotakika."

Padri alikomea hapo kusoma. Alisoma sentensi ya mwisho mara tatu. Alitingisha kichwa chake kwa huzuni. Rosa alikuwa amepiga mistari chini ya maneno yaliyokuwa ya maana zaidi kwake; mambo aliyokuwa anahitaji wakati huu; na mambo mengine yaliyokuwa yakimsumbua sana moyoni mwake: tamaa ya mwili; hofu ya kupata mimba; inaondolewa kabisa; furaha ya mwili; staili; na mimba baada ya mimba.

Kama Padri angalizungumza juu ya mambo haya labda angaliweza kumsaidia. Lakini yeye alianza kumzungumzia juu ya wokovu. Kwa hiyo Padri alipoanza kuzungumza, Rosa aliona anapoteza muda wake.

"Rosa, maneno uliyoandika uliyatoa wapi?" Padri aliuliza kwa unyenyekevu.

"Nimeyatoa kwa wenzangu."

"Ninakuomba uyachome yote."

Padri alinyamaza kwa muda. Alizungumza tena.

"Rosa, nimekuja kukusaidia; nimekuja kukuonyesha tena mwanga wa wokovu."

"Umekuja kunisaidia! Mimi maskini?"

"Ndiyo, wewe maskini wa roho."

"Umejuaje, wewe Mungu?"

"Mwovu huonekana kwa matendo."

"Umeyafahamuje matendo yangu?"

"Dalili ya moto ni moshi. Hujapata mimba wewe hata mara moja?"

"Ya·nani?"

"Si lazima nifahamu ya nani."



"Utaona kama nitapata mimba tena."

"Mimi mtumishi wa Mungu. Nimekuletea habari njema, Rosa."

Padri alifungua Biblia yake, pale alipokuwa ameweka picha ya mtu msalabani. Rosa alijaribu kusikiliza Padri alipoanza kusoma.

"John 8: 1–10 'Walikwenda kila mtu nyumbani kwake; naye Yesu akaenda mpaka mlima wa Mizeituni. Hata asubuhi kulipokucha akaingia tena hekaluni, na watu wote wakamwendea; naye akaketi, akawa akiwafundisha. Waandishi na Mafarisayo wakamletea mwanamke aliyefumaniwa katika uzini, wakamweka katikati. Wakamwambia..." Padri alisoma mpaka mwisho. Alisoma maneno ya mwisho tena. "Yesu akawambia, wala mimi sikuhukumu. Enda zako wala usitende dhambi tena."

Padri alifunga Biblia yake. Alianza kumhubiria Rosa: "Usikate tamaa. Rosa usikate tamaa. Kukata tamaa ni dhambi isiyoweza kuondolewa hapa duniani. Yesu bado yu nawe. Katika mfano huu tunamwona akimwondolea dhambi mwanamke asherati. Wokovu uko bado machoni mwako."

Rosa alianza kutapika maneno, na matapishi hayamezwi tena. "Wokovu maana yake nini? Wokovu! Wokovu gani! Kama kuna moto basi nitakwenda!"

"Rosa, usihamaki."

"Hapana; hufahamu taabu zilizonipata."

"Kila mtu anapata taabu humu duniani."

"Padri, maisha yangu yamekwishaharibika, na sijali! Kwanini wewe ujali roho yangu kuliko mimi mwenyewe?"

Padri alimwangalia, alishangaa. Alisimama na kufungua mlango. Kabla ya kutoka nje alisema:

"Lusifa! Lusifa amekwishafanya roho yako kiti chake." Padri alionekana akitoka nje kasi sana na Biblia yake kwapani. Rosa alifunga mlango. Hakuzidi tena kumwona Padri huyo kwa siku zilizofuata.

Wakati huu Rosa alikuwa amekwishapata tabia ile ya kutojali watu wanasema nini. Yeye alijifahamu mwenyewe kuliko mtu yeyote. Mara kwa mara alitenda mambo yaleyale waliyokuwa wakimzungumza mbele ya haohao watu ili awakasirishe zaidi. Tangu siku hiyo mvulana yeyote aliyekuwa akiingia ndani ya chumba chake alitoka nje akipiga miayo moja kwa moja. Rosa alitenda hivi kwa sababu alikuwa na hasira.

"Sijali!" Alizoea sasa kusema. Pia alitenda hivi kwa sababu ya dawa za kuzuia mimba ambazo alikuwa amekwishanunua.

# IX

Mvua ilikuwa ikinyesha na Rosa alikuwa chumbani mwake akiwa amejikunyata kwa baridi. Alikuwa amejifunika kanga mabegani. Rosa alikuwa amekaa kwa raha akingojea muda wake ufike. Alikuwa amekaribishwa. Kwa kawaida siku mvua ikinyesha wanafunzi hawakuwa na raha pale shuleni maana mvua ilipunguza sana uhuru wao wa kutembea. Ni Rosa peke yake aliyekuwa na furaha siku hiyo.

Baridi ilikuwa nyingi, na wanafunzi walikuwa vyumbani mwao. Nje hapakuonekana mtu—hata ndege hakuonekana angani isipokuwa wafungwa waliokuwa wakitembea kuelekea jela ya Kiguruwia; askari jela wakiwa nyuma yao na bunduki zao mkononi. Wafungwa walikuwa na mizigo ya kuni vichwani; kila mmoja mzigo wake. Nguo zao zilikuwa zimetota kwa mvua. Mvua ilikuwa bado ikinyesha. Barabarani gari lililokuwa likisafirisha mafuta lilikuwa limepinduka, magurudumu juu. Kama isingalikuwa hao wafungwa dreva angalikufa. Dreva wa gari hilo alipelekwa hadi hospitalini mjini.

Mvua ilikwisha saa sita. Baada ya kula wanafunzi walikwenda kuangalia gari lililopinduka kwani shule haikuwa mbali na barabara. Siku za Jumamosi wanafunzi waliruhusiwa kwenda kutembea. Wengi walikwenda kuangalia gari hilo walipitiliza mpaka mjini. Rosa alikuwa na mambo mengine ya kufanya; mambo ya maana zaidi.

Baada ya kula Rosa alikwenda chumbani mwake. Alikaa juu ya kitanda chake. Aliangalia saa yake ya mkononi. Aliona muda bado—saa ilisema saa saba. Moyo wake ulikuwa ukimdunda. Alichukua daftari lake aliloambiwa kuchoma na kuanza kusoma. Alifunua ukurasa ule aliokutwa na Padri akisoma. Mara Rosa alikumbuka jinsi alivyomjibu Padri siku ile: "Mapadri watu wa ajabu!" Alisema kwa sauti. Rosa alijitambua. Aliinuka kuchungulia nje ili kuhakikisha kwamba hakuna mtu aliyemsikia. Alikaa tena kitandani. Alikaa akitazama chini hali akikisaidia kichwa chake kwa mikono miwili. Alifikiri kwa muda. Alistukia akipiga mwayo mrefu, "Haauu, maisha! isha! isha!" Aliinuka na kujinyoosha mikono, "Uu, u, u! Aaaa!" Aliangalia tena saa yake. Aliona muda umekaribia. Alisoma tena ile barua kuhakikisha ule muda alioambiwa afike. Barua ilisema saa kumi; saa yake sasa ilisema saa nane. Alianza kujitayarisha.

Sabuni ya kuogea ya aina ya *Butone* ilitafutwa. Alipofika chumba cha kuogea alianza kujiangalia na kujipapasapapasa. Alitumia muda wa saa moja kwa kuoga. Alipomaliza kuoga alifungua sanduku kuchagua nguo ya kuvaa. Nyeusi aliona haifai: ataonekana kama mtu aliyefiwa. Nyeupe aliona ni rahisi kuchafuka. Alitoa nguo zote sandukuni. Alikaa kufikiri. Mwishowe alikata shauri kuvaa gauni lenye rangi nyeupe na mistari mieusi kuelekea juu shingoni. Alilivaa. Aliona linamkaa. Kioo kilitafutwa—fika umwone umpendaye. Rosa alianza kutabasamu alipojiangalia. Alitoa meno kidogo; aliyaona ni safi. Alitoa ulimi aliona ni safi. Aliashama. Aliona kila kitu ni safi, isipokuwa nywele. Nywele zilitimuliwa siku hiyo. Rosa alionekana mtu mwingine kabisa. Mwanamke hasahau mafuta ya nywele kama mwanamume asivyosahau wembe wa kunyolea ndevu. Mafuta yaliwekwa. Na sasa muda wa kuchagua viatu vya kuvaa ulifika.

Viatu vyenye visigino virefu viliwekwa miguuni. Alipotembea alifanana na mtu anayejaribu kuchukua kitu fulani mahali ambapo hapafikii. Alipojaribu kutembea chumbani mwake mwendo wa madaha ulikuja kwa urahisi. Rosa alipoangalia saa yake aliona ni saa kumi na moja. Aliiiangalia kiooni mara ya mwisho. Alikuta poda ndani ya masikio. Aliyapangusa vizuri kwa kitambaa. Alichukua mfuko wake wa mikononi na kuondoka kwa haraka. Alifunga chumba chake.

Rosa hakuwa anaenda mbali. Alikuwa amekaribishwa na mwalimu mmoja, mwalimu wa chuo hichohicho, Mwalimu Mkuu wa Chuo. Rosa alipofika alikuta Mwalimu Mkuu amemngojea kwa hamu sana.

"Karibu! Karibu! Nilifikiri hutafika!"

"Ahadi ni deni."

"Asante."

Rosa alikalia kochi moja, na kabla hajasema zaidi aliulizwa, "Unatumia nini, Martini au VAT 69?

"Martini," Rosa alijibu akijipulizia upepo kwa kitambaa.

Chupa moja ya Martini ililetwa. Rosa alianza kunywa. Aliangalia chumba kila upande. Upande mmoja ulikuwa umejaa picha za magazetini. Upande mwingine kulikuwa kumetundikwa vyeti na shahada mbalimbali. Upande mwingine kulikuwa kumetundikwa picha kubwa

sana, ilikuwa ya siku ya arusi, yeye na mkewe. Upande wa nne ulikuwa umewekwa sanamu zinazochongwa na Wamakonde. Hayo yote Rosa aliyaona. Upande uliompendeza ni ule uliokuwa na picha za magazetini.

"Rosa," Mwalimu Mkuu alianza kusema baada ya kunywa bilauri moja ya mvinyo. "Rosa, unafahamu jinsi walimu wengine wanavyokuchukia? Juzi tulikuwa na mkutano wa walimu. Walimu wote walikata shauri ufukuzwe shule, eti kwa sababu ulitoa mimba. Mimi nikiwa kama mwalimu mkuu wa shule hii ninakuhakikishia kwamba hutafukuzwa!"

"Nitashukuru," Rosa alisema akirembua macho.

"Nitaona pia kwamba lazima upate cheti chako cha ualimu."

"Asante."

Chupa ilipobakia nusu, redio ilifunguliwa na dansi ya watu wawili ilianza. Mapazia ya madirisha yalivutwa. Chupa ya kwanza ilipokwisha Rosa alikuwa amekwishaanza kukaa mapaja yake nje.

Jua lilitua. Giza likaingia. Mwezi ulitokeza. Mwalimu alipotoka chumba cha kulala—saa tano—kuja kufungua mlango uliokuwa umeachwa wazi, alishangaa kuona mwezi mkubwa ukimwangalia mlangoni. Mwezi ulikuwa mwekundu sana kana kwamba ulitokeza kuja kumhukumu. Alifunga mlango na kurudi ndani upesi.

Humo chumbani mwalimu mkuu wa chuo—Thomas—alimwomba Rosa avue nguo wakalale, kwani saa zilikuwa zimekwenda. Rosa alimwomba Thomas atazame pembeni ili avue. Thomas hakukataa. Aligeuka kuelekea ukutani. Thomas aliweza kuona kivuli cha Rosa ukutani kikivua nguo. Alipata shida. Moyo wake ulikuwa ukimdundadunda. Rosa alivaa taulo.

"Ndala ziko wapi? Ninataka kuoga kwanza."

"Chini ya kitanda."

"Nimekwishaziona. Bafu wapi?"

Thomas aligeuka. Alimwelekeza. Rosa alimfuata nyuma.

"Hii hapa."

Alipomaliza kuoga alimkuta Thomas amemngojea chumbani. Rosa alikuwa amevaa kanga moja. Thomas aliangalia kila kitendo alichotenda. Rosa alijikausha kwa taulo polepole sana. Kisha alichana nywele zake. Thomas aliona anapoteza muda. Aliamka. Alimshika Rosa; alimbana na kumbusu. Walikaa kitandani. Walisimama tena. Walibusiana. Thomas alikuwa akiyachezea matiti ya Rosa kwa mkono mmoja kama mtu anayechukua mayai mawili mkono mmoja. Walikaa kitandani tena. Kila mmoja moyo ulikuwa ukimdunda. Walibusiana tena na tena. Thomas



alikishika kidevu cha Rosa kwa mkono mmoja, mkono mwingine ulikuwa ukipapasapapasa kiuno chake. **Polepole aliuinua uso** wa Rosa. Walitazamana machoni.

"Rosa, tunaweza kuendelea hivi mpaka kesho," Thomas alisema. "Tuzime taa tulale."

"Ngoja kidogo."

Rosa alijipaka mafuta kidogo. Baada ya muda mfupi taa ilizimishwa. Giza liliingia. Rosa alikaa juu ya kitanda. Thomas alisikia kitanda kinalia: Rosa alikuwa kitandani. Thomas, akiwa na shauku kubwa, alimtupia mkono. Aliona kwamba Rosa hakuwa na nguo hata moja. Thomas alimvuta ili amsogeze karibu. Mara moja mkono wake ulishikwa na kurudishwa kwa nguvu.

"Si kawaida yangu," Rosa alisema.

"Kwa nini?"

"Huwa sipendi. Si leo siku ya kwanza."

"Sasa!"

"Tuzungumze tu."

"Mpaka lini?"

"Mpaka mimi nipende."

"Utapenda lini"

"Vumilia kidogo."

"Haiwezekani."

"Kwa nini huwezi?"

"Mwenzio sijiwezi."

"Lakini kwa nini hupendi?"

"Hali yangu hairuhusu."

"Hali gani?"

"Mimi mwanafunzi wako."

"Sahau uanafunzi."

Thomas alimtupia mkono tena. Rosa aliurudisha.

"Basi mimi ninakwenda kulala kitanda kingine."

Thomas aliamka. Alikuwa bado hajatoka kitandani Rosa alipomshika na kumrudisha. Rosa alimkumbatia Thomas. Thomas alikusanywa. Alivutwa. Aligusa mwili wa Rosa.

Wakati huo Thomas alikuwa hafahamu yuko wapi. Alikuwa amekwisha kazi. Alisema maneno mengi. Aliapa yamini kwamba Rosa hatafukuzwa shule kamwe. Rosa aliona kwamba ameshinda. Sasa alikuwa akimpangusa jasho Mwalimu Mkuu wa Chuo: baada ya kujenga

nchi mwananchi alitoka jasho. Usiku huo Thomas alikuwa kama kifaranga cha kuku chini ya ubawa. Alikusanywa wala hakusikia kitu tena. Hata kama mtu angalitembea juu ya paa Thomas asingesikia.

Ndege walikuwa wamekwisha anza kulia. Ingawa kulikuwa kumekucha sauti ilikuwa bado ikisikika ndani ya nyumba: *"Kiss me slowly; you are hurting me dear!"* Nje, mzigo ulikuwa mlangoni na mtu fulani alikuwa akiwasikiliza dirishani. Mtu huyo alipandwa na mori aliposikia sauti ya mlio wa furaha. Alitosheka. Aliondoka kwenda nyumba iliyokuwa karibu nao.

Aliporudi, alikuwa kama mtu mwenye kichaa. Alianza kupasua mlango kwa shoka. Siku za mwizi ni arobaini. Mle ndani wote wawili walishangaa kusikia mlango ukigongwa kwa ghadhabu.

Mwalimu Mkuu wa Chuo alitambua kwamba huyo alikuwa ni mke wake, kwani hiyo haikuwa mara yake ya kwanza. Rosa pombe ilimtoka; alianza kukimbia huku na huko kama samaki ndani ya sanduku la kioo. Sasa mlango wa chumba ulikuwa ukipasuliwa. Ulipasuka. Mara moja mke wa mwalimu aliingia na shoka lake mkononi limeinuliwa juu tayari kumwangukia Rosa kichwani. Mwalimu alilidaka hewani.

"Leo utanitambua! Unataka kuniletea hapa umalaya wako!"

Rosa alijaribu kukimbia. Alishikwa na yule mwanamke. Rosa aliangushwa chini. Yule mwanamke alimwinamia. Rosa alitiwa jino. Palepale uso wa Rosa ulienea damu. Yule mwanamke alionekana akitema kitu fulani chini. Rosa alilia. Mwalimu alimtoa mke wake juu ya Rosa. Rosa alikimbia. Kabla hajawahi kutoka nje redio ilimpata mgongoni. Ilianguka chini na kupasuka. Rosa huyoo! Chumbani mwake.

Ndani ya chumba Mwalimu Mkuu wa Chuo alibaki akifokewa kama mtoto mdogo.

"Ulifikiri nimekwenda nyumbani! Nilitaka kuwashika. Nimechoka na huyo msichana! Kama unataka kumwoa afadhali umwoe upesi!" Alichukua tena shoka lake na kuanza kupasua kabati pamoja na meza za mle ndani.

"Sijui kwa nini Serikali ilikupatia ukubwa! Ulipata cheo hiki kwa sababu ya ukabila tu. Mimi ninafahamu! Na sasa ninaweza kukutobolea. Kama hungalikuwa na kikazi hiki, usingalinioa! Mweusi kama chungu!"

Mwalimu Mkuu, Thomas, alikuwa mtu ambaye alielewa kwamba ndoa ni maisha ya watu wawili, mume na mke, mpaka siku watakayokifiana;



siyo mpaka kufa! Huyo aliyekwenda alikuwa mke wake wa tatu. Thomas alikuwa amefanya hila ili amfukuze mke wake bila kumwambia kinaganaga. Siku aliyoandika barua kwa Rosa alijifanya kuisahau mezani na kwenda kufundisha—baada ya mke wake kumwambia kwamba siku fulani atakwenda kuwasalimu wazee wake nyumbani.

Rosa alipofika shuleni aliingia upesi chumbani mwake. Hata hivyo kulikuwa na wasichana wengine waliomwona. Alipofika chumbani alijifungia humohumo kwa ufunguo. Alikimbilia kioo. Alipojiangalia ndani ya kioo hakuweza kuamini kwamba hiyo ilikuwa kweli sura yake. Alilia kwa sauti. Alililia sikio lake. Yule mwanamke alimwuma sikio na kutoa sikio lote la nje. Alianza kusikia maumivu makali. Saa tatu mwalimu alikuja kumchukua kwa motokaa mpaka hospitalini baada ya kuona kipande cha sikio ndani ya nyumba yake. Sikio lilipona. Rosa sasa alikuwa na sikio moja. Alipopona kitambaa hakikumtoka kichwani.

Wanafunzi walijiuliza mara nyingi kwa nini Rosa hakufukuzwa shule. Matendo yake yalikuwa yamekwishajulikana kwa walimu wote. Baada ya kitendo hiki kilichovuma siku hiyo mpaka Dar es Salaam, Rosa alijulikana kama mke wa Mwalimu Mkuu. Ilionekana wazi kwamba ilikuwa vigumu kumfukuza shule. Wanafunzi walianza kumchukia kwa sababu yeyote aliyekuwa akikutwa na Mwalimu Mkuu amesimama akizungumza naye alipewa adhabu kali. Siku moja alipopitia kikundi cha wavulana pale shuleni alisikia mvulana mmoja akitema mate chini. "Amekwisha kazi huyu! Amekwisha kazi."

Rosa aliangalia nyuma. Vijana walinyamaza. Rosa alifunua mdomo wake lakini maneno yalikataa kutoka mdomoni kwa sababu ya hasira. Aliona afadhali avumilie. Aliendelea na safari yake kwenda chumbani mwake. Rosa alikuwa hajitambui mpaka alipopitia kundi la wasichana. Alisikia mmoja wao akisema: "Maskini! Maskini hajitambui!" Rosa alijiangangalia nyuma. Alikuta nguo yake imeingia matakoni. Wale vijana waliona kinyaa walipomwona; ndiyo maana mmoja wao alitema mate chini. Rosa alipofika chumbani mwake alifika kujitupa kitandani. Mambo mengi yalimzunguka kichwani mwake. "Rosa," alisikia sauti moyoni mwake ikimwita. Ilikuwa sauti kama ya mtu anayetaka kufa. Ilikuwa sauti hafifu sana. Rosa peke yake aliweza kuisikia. Rosa peke yake aliweza kuitambua.

"Rosa, Rosa, Rosa, mtoto wangu. Mimi ninakufa. Njoo karibu nikuguse; njoo nikupe baraka yangu ya mwisho."

Hiyo ilikuwa sauti ya mama yake. Ilimsumbua sana Rosa. Akiwa Morogoro, Rosa hakupata kwenda nyumbani wakati wa likizo. Livu moja alikwenda Dar es Salaam; livu nyingine alikwenda Moshi; na livu iliyopita alikuwa Tanga. Wakati ule alikuwa bado akipendwa sana na wavulana; sasa vijana walitema mate walipomwona. Wakati ule hata wasichana wenziwe walimvulia kofia kwa jinsi alivyoendesha maisha; sasa walimhurumia kiasi cha kumwita "maskini." Wakati ule alikuwa na masikio mawili; sasa alikuwa na sikio moja. Rosa aliona maisha yanamghilibu.

Alianza kumkumbuka mama yake. Alikumbuka pia maneno yake. Alianza kuwakumbuka kina Flora, Honorata, Stella, Sperantia na Emmanuel. Alikumbuka jinsi Stella alivyokuwa akiwachekesha. Alikumbuka hadithi walizokuwa wakisimuliana usiku. Rosa alitokwa machozi. Alijipangusa kwa kitambaa. Alisikitika zaidi alipokumbuka kwamba alikuwa amekwishapata barua tatu kutoka kwa mama yake zikimjulisha ugonjwa wake. Mama yake alikuwa mgonjwa. Alimwomba afike nyumbani livu moja. Wakati ule Rosa hakuzijali. Sasa aliona uchungu. Rosa alikata shauri kwenda nyumbani.

Akikata shauri Rosa, amekata. Alikwenda nyumbani livu iliyofuata. Alipofika nyumbani alimkuta mama yake mzima. Alikuwa amekwishakonda kwa mawazo lakini alikuwa mzima. Regina alimwazia mtoto wake. rosa alipokelewa kwa mikono miwili.

"Mtoto wangu! Njoo ukae juu ya magoti yangu!" Rosa hakukataa alikaa juu ya magoti ya mama yake. Wote wawili walitokwa na machozi walipokumbatiana.

"Rosa, mbona umekonda namna hii! Ulikuwa unakula nini?"
Rosa hakumjibu. Aliposhuka chini mama yake alikwenda kumtayarishia chakula.

Dada zake walipotoka shuleni jioni walifurahi sana kumwona Rosa; Rosa pia alifurahi. Stella alikuwa wa kwanza kuzungumza.

"Mimi siku hizi niko darasa la sita. Honorata amekwishashindwa. Siku hizi anakaa nyumbani tu sisi tunasoma."

"Flora amekwishakuja nyumbani?" Rosa aliuliza.

"Ndiyo tulikuwa naye hapa livu iliyopita."

"Nasikia siku hizi ni mweupe kunizidi."

"Mmmn! Nani alikwambia. Mnalingana tu kwa weupe."

"Honorata amekwenda wapi?"

"Alikuwa amesema anakwenda kusukwa nywele. Labda ndiko amekwenda."



"Sperantia yumo darasa gani?"

"La tatu. Alikua wa pili mtihani uliopita."

Wakati Stella alipokuwa akihojiwa Sperantia alikuwa amekwishabadili nguo. Stella pia alikwenda kuvua nguo za shule na kuvaa za nyumbani. Regina aliwaletea chakula alichobakiza Rosa. Rosa alisikia Stella akizungumza na chakula mdomoni, "Honorata huyo anakuja" Honorata alirudi jioni kutoka kwa rafiki yake kusukwa. Alimsalimu Rosa. Alianza kumwuliza habari za Morogoro, jinsi watu na nchi ya huko ilivyo. Rosa alieleza sura za Waluguru, nguo wanazovaa, chakula chao, na kazi wafanyazo. Alieleza juu ya milima ya Morogoro.

Zakaria alifika nyumbani usiku kama kawaida yake. Alipofika, Regina ndiye alikuwa wa kwanza kumjulisha kwamba Rosa alikuwa ndani. Zakaria aliguna tu na kusema, "Rosa ndiye nani? Malaya hajawa mgeni wangu wala mtoto wangu."

Maneno haya aliyasema kwa sauti kubwa. Rosa aliyasikia. Maneno haya yalimsumbua sana Rosa moyoni. Rosa hakujali kusikia hayo maneno yakisemwa na watu wengine. Lakini kusemwa na baba yake! Hili lilikuwa jambo kubwa sana. Wakati huu Rosa alikuwa kama mtoto mpotevu. Alihitaji kupokelewa mikono miwili na kuonywa kwa upole. Wakati huu Rosa alihitaji watu wa kumtuliza. Fikira tu ya kwamba kulikuwa na watu waliomjali ilitosha kumtuliza na kumpa furaha. Kati ya makosa makubwa aliyotendewa na baba yake hili ndilo lilikuwa la pili.

Rosa alilia. Alianza kusita kama kweli Zakaria alikuwa baba yake. Alijifikiria kwamba hakuwa mtoto wake halali. Lakini Rosa hakuwa mtoto sasa. Alikuwa mtu mzima. Alijipangusa kwa kitambaa na kusema moyoni, "Ya Mungu mengi. Mungu ndiye anafahamu mkosefu ni nani. Nisingezaliwa hapa labda ningekuwa mtu mwingine." Rosa sasa alikata shauri. Kwa sasa alikaa kimya. Moyoni alikuwa amevurugika kama mtu aliyetaka kutapika. Kwa sasa hapakuwa na mwingine aliyefahamu mawazo yake.

Rosa alipokuwa nyumbani mama yake alimjali sana. Kila siku alipewa maziwa mengi zaidi kuliko watoto wake wengine. Baada ya majuma mawili Rosa alinenepa. Kila mtu nyumbani alimwonea huruma sana Rosa isipokuwa baba yake. Alipoeleza kisa cha kukatwa sikio walimsikiliza hali wameshika mashavu yao. Hakuna aliyemcheka. Lakini Rosa hakutoa hadithi yote. Alieleza jinsi alivyoonewa na yule mwanamke bila kosa lolote.

Haukupita muda mrefu kabla Rosa hajagombana na baba yake. Katika matembezi yake Rosa alipata kufahamiana na Mkuu wa Wilaya, hasa kwa sababu alikuwa kaka yake Thereza. Siku moja mkuu huyo wa wilaya alikuja kumchukua Rosa kwa gari kwenda ufuko wa Rubya, kule kwenye mchanga mweupe kama sukari. Motakaa ya Mkuu wa Wilaya ilipofika Zakaria alikuwa amelala. Aliposikia mlio wa motakaa nyumbani kwake aliamka. Rosa alikuwa amekwishavaa tayari kwa safari. Zakaria alipotoka nje alimfokea sana Mkuu wa Wilaya.

"Rudi na motakaa yako! Unafikiri hapa kuna wasichana wengi wa kuchukua kwa gari. Toka hapa! Masikio makubwa mithili ya punda! Na wewe Rosa usitoe pua yako nje! Nisikuone unatoka hapa! Unafikiri uko Morogoro!"

Rosa alikuwa amekwishakata shauri juu ya jambo hili. Alingoja kuchokozwa. Kweli Zakaria alichokoza mzinga wa nyuki. Rosa alitoka nje ghafla. Alikwenda mpaka karibu ya baba yake. Alitapika maneno. Maneno haya alikuwa ameyatunza moyoni mwake kwa muda mrefu.

"Kila wakati unatuchunga. Unafikiri utatuoa wewe!" Rosa mwishowe aliyasema yale maneno. Maneno aliyopaswa kusema siku ile aliyopigwa angali msichana. Zakaria aliyapata yote: maneno aliyopaswa kuambiwa siku ile. Maneno hayo yalimchoma moyo Zakaria. Alisimama pale kwa muda bila kusema neno. Rosa sasa alitembea huku na huko kwa maringo hali ameinua mabega yake juu. Rosa alishinda. Mbele yake pandikizi la mtu aliloshinda lilikuwa limesimama bila damu. Damu ilikuwa imeliganda. Mkuu wa Wilaya alikuwa pale kushuhudia.

Zakaria, kutunza heshima yake, alifunua mdomo. Maneno fulani yalitoka mdomoni mwake.

"Rosa, tangu leo wewe si mtoto wangu."

"Tangu leo wewe si baba yangu." Rosa alidakia bila kukawia. Aliingia mara moja ndani ya motokaa na kwenda zake *Beach*. Siku hiyo Rosa hakurudi nyumbani.

Jioni Ndalo alifika kuongea na jirani yake. Alimkuta Zakaria amekaa kwenye ukumbi wa nyumba yake. Walipomaliza kusalimiana Zakaria alitikisa kichwa na kusema.

"Ndalo, ulimwengu umegeuka."

"Kwa nini?"

"Leo hii hii binti yangu kaniasi. Amenikataa. Amesema kwamba tangu leo mimi si baba yake!"

"Sema kweli!"



"Hivi hivi! Tena kaniambia mbele ya Mkuu wa Wilaya. Macho kwa macho."

"Sema kweli!"

"Aaah! Wewe unafikiri uongo!"

"Kwa kweli, hata mimi mwenyewe ninashangaa. Wewe si mtu wa kwanza kutendewa jambo kama hili. Juzijuzi mzee fulani kaambiwa vivi hivi na binti yake, eti kwa sababu alimzuia kuvaa nguo zao hizi za siku hizi zinazowafanya wafanane na mafunza. Sijui zinaitwaje...eh nimesahau jina. Sijui zinaitwaje. Kama 'teti'...'tahiti'...'taiti' ee ndiyo, 'taiti'.

"Watoto wa siku hizi waliosoma wote ni namna moja. Mzee mwingine nimemsikia huko Bulamba. Yeye alijichoma ulimi kwa sababu ya kulazimishwa na watoto wake kutumia uma. Labda ingefaa kama tusingaliwapeleka watoto wetu shuleni."

Waliendelea na mazungumzo yao kwa muda mrefu. Ilikuwa kama kwamba vipofu wawili walijaribu kuongozana njia. Hawakutizama upande mwingine wa kamari na kuangalia nani kaliwa. Hawakufikiri kwamba kuna vijana wengi wanaowateta vilevile.

"Wazee wa siku hizi wanatushusha sana," hawa vijana nao walisema. "Wakija kukutembelea wanakataa kutumia vyoo. Wanang'ang'ania vichaka tu." Katika jambo moja tu, wazee na vijana wanakubaliana—kwamba ulimwengu umegeuka. Zamani senti tano iliweza kununua nguo; siku hizi hata kitumbua hainunui. Zamani ilikuwa marufuku mwanamke kula nyama ya kuku; siku hizi bwana, bibi, na watoto wanakula meza moja. Mapatanisho yanaweza kuletwa kama kundi moja likipiga hatua moja mbele na kundi jingine hatua moja nyuma.

Rosa alingoja hasira ya baba yake ipungue. Alirudi nyumbani baada ya siku mbili. Kwa bahati alipofika nyumbani hakumkuta baba yake. Alimkuta mama pamoja na dada zake. Stella alimweleza jinsi Zakaria alivyonoa panga kumkata vipandevipande kama angalirudi nyumbani siku ile. Rosa alipofika nyumbani mama yake alimwonya afunge mizigo aondoke upesi kabla ya Zakaria kurudi nyumbani. Mama alimwambia aende kukaa kwa mama yake wa ubatizo. Rosa hakukataa. Alifunga mizigo na kwenda kijiji cha Kameya; maili tano hivi kutoka Namagondo. Huko ndiko alikuwa anaishi mama yake wa ubatizo.

# X

Kameya, Rosa hakukaa zaidi ya majuma mawili. Livu yake ilikuwa imekaribia mwisho. Mkuu wa Wilaya alifika na motakaa yake kumsindikiza mpaka mjini Nansio. Rosa aliingia botini. Boti ilipokitega mgongo kisiwa cha Ukerewe, Rosa aligeuka kukiangalia. Aliona watu bado wanapunga mikono kuwaaga. Rosa naye aliweka mkono wake juu, lakini moyoni mwake alikuwa akiwafikiria dada zake na mama yake. Rosa alitumainia kukiona tena kisiwa cha Ukerewe: alikuwa anakwenda kumaliza kipindi cha mwisho. Rosa alijiona mwalimu.

Meli ilipofika Mwanza jioni, Rosa alishangaa: Leo meli hii imekimbiaje? Lakini mwendo wake ulikuwa uleule. Na ilitumia muda uleule wa saa tatu majini. Rosa alishangaa kwa sababu meli ilipokuwa ikitembea mawazo yake yalikuwa mbali. Humo melini Rosa alipata kukaa karibu na mwanamke mmoja aliyekuwa amepakata mtoto miguuni. Mtoto huyo alikuwa mzuri sana hata Rosa aliona wivu. Mtoto alimwangalia Rosa. Alishika mkanda wake wa saa. Mtoto alimchekea Rosa, alinyoosha mikono yake. Rosa alitamani kumbeba.

"Mtoto, njoo."

Yule mtoto aliinua mikono juu. Mama yake alimwachilia. Mama alifurahi sana kusaidiwa. Mtoto alipokuwa mikononi mwa Rosa hakuonyesha alama yoyote ya kulia. Alianza kumpapasapapasa kifuani. Rosa alifahamu anatafuta nini. Alimwonyesha mkanda wake wa saa ili kumpotezea mawazo. Alianza kuchezacheza nao. Wakati huo wote Rosa alikuwa akifikiri kama naye pia atazaa mtoto mzuri kama huyo siku moja. Alianza kujuta alipokumbuka mimba alizokuwa amekwishatoa. Lakini Rosa hakuwa mzee: alikuwa bado kijana. Alikuwa bado na uwezo wa kuzaa. Hiki ndicho kilikuwa kitulizo chake kwa wakati huu. Maneno ya mama yake hayakuwa na nguvu.

Mawazo haya yalipokuwa yakimzunguka kichwani mwake, mtoto alikuwa amekwishapatwa na usingizi. Alilala hali amekaa juu ya miguu ya Rosa, kichwa chake kikitazama juu. Mtoto alilala mdomo wazi. Rosa



alianza kazi ya kufukuza inzi wasije tua juu ya mdomo na kuingia ndani. Rosa hakusikia uchovu wowote. Alisikia moyo wa mtoto ukipiga upesiupesi. Alisikia mtoto akivuta pumzi upesiupesi. Yote haya Rosa aliyaona ya ajabu. Rosa alimwangalia mtoto. Aliona mtoto amefumba macho. Rosa alikuwa haoni mtoto tena isipokuwa malaika mdogo.

"Kuna wanawake wengine wenye dawa," yule mama alianza kusema. "Mtoto huyu huwa hapendi watu lakini leo amebebwa hata akalala. Dada, mtoto wangu amekupenda."

"Labda alikuwa amepatwa na usingizi tangu zamani," Rosa alijibu akitabasamu kwa sifa aliyopewa.

Kwa hiyo meli ilipofika Mwanza, Rosa alisikitika kuachana na mtoto huyo. Mikono yake ilikuwa na joto, lakini sasa joto lake lilipotea na baridi ilianza kumwingilia. Rosa alikumbuka kwamba alikuwa na pakiti moja ya biskuti. Alimpa mtoto na kusema kwa heri.

Rosa hakuutembelea mji wa Mwanza. Kesho yake ilikuwa siku ya Jumapili, siku ambayo wasichana waliruhusiwa kupata wageni, na Rosa alitaka kwenda kumwona dada yake Flora. Alifika shuleni saa saba. Alishangaa kukuta mlango wa barabara umefungwa na polisi alikuwa akiulinda.

"Shida!" Rosa alinyamaza.

"Njoo hapa! Njoo hapa!" Polisi alimwita. Rosa alikwenda.

"Unataka kumwona nani?"

"Dada yangu."

"Saa bado mpaka saa nane."

Rosa alikaa pale juani muda wa saa moja. Wakati huu wote alikuwa akiwaza moyoni: 'Mambo haya ndiyo mimi sipendi: kuchungwachungwa kama wanyama. Wanafikiri hili ndilo jawabu. Wanafikiri hii ndiyo njia ya kuwazuia wasichana wasipate mimba! Hawa watu hawafahamu.'

"Jina lako nani?" yule polisi alimwuliza.

"Rosa."

"Rosa nani?"

"Rosa Mistika"

"Mistika ndio babako?"

"Hapana, Zakaria."

"Unataka kumwona nani?"

"Dada yangu."

"Yeye hana jina?"

"Flora."

Polisi aliandika.

"Haya! Unaweza kwenda. Lakini lazima umwone kwanza mwalimu wa zamu."

Rosa alianza kutembea kuelekea shuleni. Aliona seng'enge imezunguka shule nzima. Rosa alifikiri kwamba shule ilikuwa karibu, kumbe wapi. Ule mlango ulikuwa umewekwa mbali. Mwishowe aliyaona majengo.

Rosa alipofika shuleni alikuta mwanamke Mzungu amekalia kiti. Ilikuwa zamu yake siku hiyo. Watu wengine—vijana—walikuwa wamesimama pale wakijaribu kujitetea.

Flora alipomwona dada yake alikimbia kwenda kusimama karibu naye. Hakuweza kumchukua wala kumsalimia kabla ya kupewa ruhusa na mwalimu wa zamu.

"Unataka kumwona nani?" Mwalimu aliuliza.

"Flora."

"Nani kwako?"

"Dada yangu."

"Jina lako nani?"

"Rosa."

"Dada yako yumo darasa gani?"

"Darasa la kumi na mbili."

Sista alifunua daftari la darasa la kumi na mbili.

"Jina lake halimo humu."

"Sista, huyo ni dada yangu," Flora alisema, kumtetea dada yake.

"Kama jina lake ulisahau kuliandika basi huwezi kumwona."

"Sista!"

"Ndiyo, hii ndiyo sheria. Na sisi lazima tufuate sheria."

"Sista."

Flora alikazana sana ili aruhusiwe kuzungumza na dada yake. Mwishowe hata Sista alimwonea huruma. Rosa aliruhusiwa. Flora alimpeleka dada yake pembeni kidogo. Walikuwa hawaruhusiwi kwenda mbali. Ili kufanya watu wengi wasielewe, walizungumza Kikerewe. Flora ndiye alikuwa wa kwanza kuzungumza.

"Rosa, shule yetu hii ni ya ajabu. Tunalindwa kama watoto wadogo. Wanafikiri hata wakati wa livu watatuchunga! Wasichana wengi hapa wamekwishapata mimba na kufukuzwa wakati wakiwa hapahapa shuleni."



"Shauri lenu. Afadhali wasichana wa Rosary. Flora, unafahamu jinsi tulivyokasirishana na baba kwa sababu ya jambo kama hili—jambo la kulindwa kama watoto wadogo! Alinikataa na mimi nikamkataa. Kwani alinisaidia nini katika elimu yangu? Hata chapa hakutoa!"

"Niliambiwa na mvulana fulani nimesahau jina lake."

"Flora, hebu tuone picha za *boys* wako!"

"Tuondoke hapa."

Flora alimchukua Rosa hadi chumbani mwake. Flora alileta faili kubwa la picha. Alimpa dada yake. Flora alisimama nyuma yake na kuanza kumwonyesha kwa mkono.

"Huyu hapa urafiki nami umekwisha. Sasa ananidai pesa zake zote alizozitumia kwangu; lakini hatapata hata chapa. Mimi sikumwomba. Huyu ninampenda, lakini hajaninunulia hata chupa moja ya soda. Huyu nyumbani kwao maskini sana. Huyu hapa ndiye rafiki yangu hasa. Ni mweupe ajabu na mnene. Unafahamu Rosa, mimi sipendi mwanamume mkondefu. Huyu ni mtu wa kusini huko. Ni mtu mnene na jambazi. Jina lake John. Mimi ni John tu; John tu ndiye atanioa. Tena mimi sipendi kijana ambaye hafahamu kucheza dansi. Baada ya ndoa mtakaa nyumbani tu kama mmea ungojeao mvua shambani. Lakini John anafahamu sana. Unafahamu pia kwamba yeyote atakayeniposa lazima apimwe hospitali nami nipo. Wanaume wengine wanadanganya. Kijana mmoja amekwishaniambukiza magonjwa. Lakini nimekwishahakikisha kwamba John hana magonjwa."

"Flora, mimi karibu nitaolewa. Baba akikataa mimi nitajioza."

"Umekwisha mpata mchumba mwingine?"

"Ndiyo, mkuu wa chuo chetu."

"Pole sana."

Walinyamaza kwa muda. Rosa hakufahamu pole ile ilikuwa ya nini.

"Emmanuel ulimwacha mzima?" Flora alianza tena mazungumzo.

"Mimi sikupita nyumbani, lakini bila shaka alikuwa mzima."

Walinyamaza tena kwa muda.

"Nani amekuruhusu kuleta mgeni wako huku!" Sista alifoka kwa sauti. Aliwafukuza nje na kumfukuza Rosa. Rosa alimuaga dada yake. Rosa alipanda basi kurudi mjini. Humo basini alisikia kijana mmoja akizungumza kwa sauti.

"Shule hii! Hii hapa! Bure sana ingawa wanalindwa. Wanachukuliwa na wapishi wa Wahindi mjini. Kwa sababu ya kulindwalindwa wamekuwa kama wanyama. Wanapenda mtu yeyote yule apataye bahati ya kuonana nao. Wamepoteza uwezo wao wa kuchagua."

Rosa alisikiliza kwa makini. Alitaka kufunua mdomo ili amwunge mkono lakini alijizuia. Aliona sauti yake haitasikilika.

Mwishowe Rosa alifika hotelini alimokuwa amepanga. Alikuwa na nia ya kuutembelea mji wa Mwanza usiku, lakini alipomaliza kula chakula cha jioni aliona afadhali apumzike kwanza. Alifika kulala kitandani akifikiri ataamka mapema. Picha ya yule mtoto mdogo ilimjia kichwani na usingizi ulimchukua. Alipoamka ilikuwa saa sita. Rosa alikata shauri kulala.

Kesho yake Rosa alipanda basi kuelekea Morogoro. Alipofika shuleni, kabla ya kupanga vitu vyake vizuri chumbani mwake, alikwenda mara moja kumwona mkuu wa chuo. Rosa alipofika nyumbani kwa mkuu wa shule alikuta watoto tu.

"Ninaweza kumwona mkuu wa shule?"

"Anaoga," mtoto mmoja alijibu.

Rosa alikalia kochi moja, lakini alishangaa kuona mkuu wa chuo amenunua makochi mapya, meza mpya, kabati kubwa mbili, na mambo mengine mengi. Zaidi ya hayo alishangaa kuona watoto wawili pale. Mkuu wa chuo alipomaliza kuoga alikuja kumwona mgeni. Rosa aliinuka.

"Samahani, labda nimekosea. Ninamtafuta mkuu wa chuo. Amehama nyumba hii?

"Mkuu wa chuo ni mimi hapa. Una shida?"

"Hapana siyo wewe. Bwana Thomas?"

"Unamtafuta Bwana Thomas?"

"Ndiyo."

"Wewe mwanafunzi?"

"Ndiyo."

"Jina lako nani?"

"Rosa Mistika."

"Jina moja."

"Ndiyo."

"Ninaweza kukuona ofisini."

"Kufanya nini?"

"Bw. Thomas aliniachia ujumbe wako."

"Ujumbe wangu?"

"Ndiyo."

"Ndiyo kusema hayuko tena hapa shuleni."

"Nitakueleza."



Rosa alinyamaza kwa muda mfupi.

"Labda unataka nikupe ujumbe wako humu ndani?"

"Itakuwa vizuri zaidi."

"Kaa kidogo nije."

Rosa alikaa. Hakufahamu mtu huyu alikuwa nani. Alimfikiria kuwa mwalimu mgeni. Yule mwalimu alirudi.

"Mimi ni Bwana Albert. Nimeletwa hapa kuja kushika nafasi ya Bwana Thomas. Ninakuomba ukae kama mwanafunzi na uzungumze nami kwa adabu! Unasikia!"

Rosa alianza kutetemeka.

"Ninasikitika kukwambia kwamba Bwana Thomas amefutwa kazi. Sasa yuko Tabora na mke wake."

Rosa alitokwa machozi. Alitoa kitambaa kujipangusa.

"Rosa, ulipata barua yangu?" Bw. Albert aliuliza. Rosa alilia sana kwa sauti. Bwana Albert alipozidi kumzungumzia Rosa alilia zaidi na zaidi.

Albert alimtoa nje na kufunga mlango. Rosa alikwenda chumbani mwake hali akilia. Kwa bahati nzuri wanafunzi hawakumwona: wengi walikuwa hawajafika. Rosa alifika na kukaa juu ya kiti karibu na meza. Aliweka mikono yake mezani, na aliinamisha kichwa kukiweka juu ya mikono. Rosa alisikitika. Moyoni mwake alikuwa amekwishakata shauri kuolewa na Thomas. Alikuwa akifikiri juu ya Thomas aliposikia mtu fulani anabisha mlango. Rosa aliamka polepole kwenda kufungua mlango.

"Samahani Rosa, hii barua yako kutoka kwa mkuu wa shule." Msichana alimpatia barua na kwenda zake. Yule msichana alionekana kufahamu kulikuwa na maneno gani humo ndani. Rosa alifunga mlango. Alifungua barua polepole sana. Barua ilikuwa imepigwa chapa. Rosa aliisoma.

Rosa alilala kitandani. Machozi yalimtoka kiasi cha kuweza kujaza kikombe cha chai. Kichwa kilimwanga. Wakati Rosa alipokuwa chumbani mwake alifikiri jinsi Mungu alivyomtesa. Bwana Albert alikuwa akizungumza na wanafunzi akieleza jinsi utawala wake mpya utakavyokuwa. Rosa, akiwa chumbani mwake, alisikia makofi yakipigwa. Moyoni mwake alifikiri kwamba wanafunzi walikuwa wakishangilia kufukuzwa kwake. Baada ya mkutano huo alisikia wanafunzi wakipita karibu na chumba chake wakisema, "Lab sasa itafungwa!" Aliudhika zaidi aliposikia vijana wengine wakipita pale na kutema mate chini.



30

Akiwa chumbani mwake Rosa hakuweza kuona ulimwengu. Alitafuta kamba akakosa. Alichukua mkanda wa gauni lake, aliona haufai. Mwishowe alikumbuka kwamba alikuwa na kisu kidogo sandukuni. Alifungua sanduku upesiupesi ili akomeshe taabu zake kabla ya hasira yake kushuka. Alikitoa. Alikikunjua. Rosa alipasua gauni lake tumboni apate mahali pa kupitishia kisu. Alifumba macho aliposikia kisu kinagusa tumbo lake. Rosa alianza kukisukuma polepole ili kiingie tumboni mwake. Ngozi ya juu ilikuwa imekwishakwaruzwa alipostukia mkono wake unashikwa. Rosa alikuwa mikononi mwa Albert.

"Rosa, usifanye jambo la kijinga namna hii! Huwezi kufaidika" Aliambiwa na Albert ambaye alikuwa amemshika.

Baada ya mkutano wake na wanafunzi, Bwana Albert alikuwa amekuja kumwambia Rosa apange vitu vyake sandukuni; kwamba amefukuzwa kabisa. Kwa namna fulani alimwonea huruma; lakini alipaswa kufuata sheria. Rosa alichukuliwa na kwenda kufungiwa ndani ya chumba kidogo baada ya kuhakikisha kwamba hapakuwa na chombo chochote cha kuweza kujiumizia.

Jioni Rosa aliletewa chakula. Alikuwa kama mfungwa. Humo ndani Rosa alifikiri mengi. Alifikiri maneno ya kumwambia mama yake. Alifikiri atasema nini kwa dada zake. Mwishowe alifikiria ujanja wa kufanya ili asiende nyumbani. Aliona vigumu: mkuu mpya wa shule alionekana kuwa mtu asiyependa mizaha. Muda wote aliokuwa naye kule nyumbani kwake hakuonyesha alama yoyote ya kucheka wala kufurahia mazungumzo. Rosa aliona maisha yake yanaharibika wakati mbaya. Alikuwa kama mkimbiaji atanguliaye wakimbiaji wote na kuanguka chini hatua moja kabla ya kufikia kamba.

Bwana Albert alikuwa bado kijana. Alipopata shahada katika ualimu huko Makerere alipelekwa mara moja kuwa mkuu wa TTC ya Mpwapwa. Bwana Albert alijulikana sana kwa ukali na ugumu wa moyo wake. Wakati huu alikuwa bado hajaoa, lakini alikuwa akiwatunza watoto wawili wa kaka yake. "Hakuna msichana wa kujichekeshachekesha mbele yake," utawasikia wavulana wa pale Mpwapwa wakimsifu. Sifa yake hii—kama inaweza kuitwa sifa—ilimfanya ajulikane. Mwishowe hata serikali ilimtambua kama mtu awezaye kuendesha shule vizuri. Na kweli Albert alifanya kazi yake vizuri: alipokuwa Mpwapwa wanafunzi walimpenda sana. Hapakuwa na hata msichana mmoja aliyepata mimba. Kwa hiyo Bwana Albert alipofika Morogoro aliendelea kutawala kwa ukali na vitisho kama alivyofanya huko Mpwapwa.



Asubuhi kabisa Albert alichukua gari lake kumpeleka Rosa mjini pamoja na vitu vyake. Bwana Albert alipohakikisha kwamba Rosa ameingia basini na kwamba basi limeng'oka kuanza safari, alirudi shuleni. Rosa alisikia uchungu wa kufukuzwa shule.

Bw. Albert aliondoa shina la mgogoro. Alifurahi kuona kwamba alifaulu bila shida au matata yoyote. Siku hiyo yote wanafunzi walikuwa wakizungumza juu ya Rosa: wengine walisema kwamba alikuwa punguani; wengine walisema alikuwa mwehu; wengine walisema kwamba malezi yake yalikuwa mabaya; na kadhalika. Lakini wengi walimsifu kwa kusema kwamba hapakuwa na msichana mwingine aliyeweza kuendesha maisha kama yeye. Yawayo yawe, Rosa alikuwa amekwishafukuzwa.

Bwana Albert hakuzungumza tena juu ya Rosa. Jioni alikwenda nyumbani akifikiri jambo gani atafanya ili kurudisha sifa ya shule juu. Alipofika nyumbani alijifungia chumbani mwake ili watoto wasije wakampandapanda mgongoni na kupoteza mawazo yake.

Giza liliingia. Upande wa mashariki alama za mvua au dhoruba zilikuwa zikionekana. Baada ya muda mfupi mawingu mazitomazito meusi yalianza kufunika sehemu yote ya Morogoro. Giza lilikuwa kubwa sana. Albert alipofungua dirisha kutazama nje, alilifunga upesiupesi kwani umeme uliompofusha macho. Matone ya mvua yalianza kusikika juu ya paa la nyumba. Ilikuwa dhoruba kubwa sana, hata wale wenye nyumba za mabati waliogopa kwamba mapaa ya nyumba yatachukuliwa na upepo. Kila mtu alitegemea kusikia kesho yake kwamba nyumba ya fulani imechukuliwa au kuanguka. Kila radi iliyopiga, watu walifikiri ilipiga yadi tatu–nne kutoka nyumba zao. Watu walijikunja vitandani. Wenye dhambi walikiri makosa yao. Wasio waovu walifikiri wezi ndio walioteleteza dhoruba hiyo.

Mawazo kama haya hayakumjia Albert kichwani mwake. Albert alikuwa mtu mwenye bidii. Dhoruba hii haikumtisha sana. Alipofunga madirisha yote aliendelea na kazi yake ya kupanga vipindi vya walimu. Kama mvulana aliyepewa ahadi na msichana, Albert hakupatwa na usingizi. Albert alikuwa akifanya kazi hali akipika chakula cha jioni. Alitumia umeme. Albert alikuwa akichorachora mistari alipoona kitu kama nyoka kikipita juu ya sakafu kuelekea kwenye friji. Kiliingia ndani. Palepale taa za nyumba zilizimika. Albert alifahamu. Alimshukuru Mungu kwamba yule nyoka hakugusa mguu wake. Alikwenda kuwasha taa ya mafuta. Alipowasha alikwenda kuchukua soda mbili kabatini na kuanza kunywa pamoja na mkate.

Bwana Albert alikuwa amemaliza chupa moja ya soda na mkate ulikuwa umebaki nusu aliposikia mlango unagongwa. Albert alisikiliza. Alikuwa amekwishasikia mengi kuhusu wachawi. Alisikiliza kwa makini. Hakusikia lolote tena. Alisema moyoni, 'Labda ni upepo tu.' Alisikia tena mlango ukigongwa, mara hii kwa nguvu zaidi. Albert aliinuka polepole sana. Alichukua panga lake—silaha yake pekee ndani ya nyumba—na kwenda kusimama mlangoni. Moyoni mwake alikuwa bado na hofu. Akiwa na panga lake mkononi, alijibanza karibu na mlango, tayari kukata chochote kitakachoanza kutokeza. Hakuna aliyefungua mlango. Alingoja kwa muda. Alisikia tena mlango unagongwa. Mara hii alisikia sauti ya mtu ikisema, "Mwalimu, hodi." Mara moja wazo lilimjia kichwani kwamba hao walikuwa ni wanafunzi, 'Labda wamepatwa na maafa fulani huko shuleni—radi kaua mtu labda' alisema moyoni. "*Wait!*" Alisema mwishowe kwa sauti. Alikwenda kuficha panga lake.

Albert alifungua mlango polepole sana: alikuwa bado na hofu kidogo. Alipofungua mlango mtu aliingia ndani. Alionekana kuwa maskini sana—kikongwe. Alikua amejifunika kichwa na Albert hakuweza kuona uso wake vizuri. Nguo zake zilikuwa zimetota na sasa zilikuwa zimegandamana na mwili wake. Alikuwa akitetemeka kwa baridi.

"Wewe nani?" Albert aliuliza.

Yule mtu alinyamaza tu.

"Wewe nani? Huelewi Kiswahili!"

Yule mtu hakujibu. Alinyamaza tu.

"Wewe mchawi?"

Albert alijaribu kumfunua ili aone uso wake vizuri. Yule mtu alikataa kufunuliwa. Albert alimsikia akilia. Palepale yule mtu alianza kufunua uso wake. Aliweza kutambulikana sasa. Alifunua mdomo. Albert alikuwa na hamu sana ya kusikia atasema nini. Kwa hiyo alipofunua mdomo wake polepole sana Albert alionyesha alama za kusikiliza kwa makini. Mwishowe yule mtu alianza kuzungumza.

"Albert. Albert," machozi yalimtoka. Aliendelea "Albert, Albert. Hivi nilikukosea nini?"

Albert alinyamaza. alipigwa na bumbuazi.

"Albert, Albert, haiwezekani." Alilia sasa kwa sauti.

Albert alimshika, alimkumbatia; hakujali tena kwamba nguo zake zilikuwa zimetota. Mwanamke machozi yalimtoka, yalitiririka juu ya mkono wa Albert. Albert aliuinua uso wa mwanamke. Walitazamana machoni.



"Rosa, mimi siwezi kukusaidia."

Rosa alilia sana. Albert alimhurumia. Moyo wake ulikuwa bado haujapatwa na pigo la huruma kama siku hiyo. Albert karibu atokwe machozi. Alijikaza. Aliona si kawaida kwa mwanamume kutokwa na machozi.

"Rosa, imekwendakwendaje hata ukarudi?"

"Nilirudia njiani—nilichukua basi jingine kurudi pale karibu na Dodoma. Niliona nikienda nyumbani baba na mama watasikitika sana."

Albert alimchukua kwa gari lake mpaka chumbani kwake. Kesho yake asubuhi aliitisha mkutano wa walimu. Aliwaeleza walimu hali ya Rosa. Aliwaeleza jinsi alivyokuwa karibu kujiua kwa kisu. Albert aliwambia walimu kwamba halikuwa jambo gumu kumrudisha Rosa: alikuwa bado hajaijulisha Wizara ya Elimu juu ya kufukuzwa kwake. Walimu hawakubisha. Walikubali. Walimwonea huruma Rosa. Lakini walisema lazima aache mwenendo wake wa zamani.

Rosa alipokubaliwa kumaliza mwaka wake alijifunza kufa na kupona ili kuwaonyesha wale waliokuwa wakimchukia kwamba akili zake zilikuwa timamu. Mitihani ilikuwa imekaribia. Baada ya majuma mawili mitihani ilianza. Rosa nusura ashindwe, lakini hata hivyo alitosheka na ushindi wake. Katika pendekezo lake, Rosa alikuwa amechagua kwenda kufundisha mkoa wa Mwanza. Hili ndilo lilikuwa pendekezo lake la kwanza. Hakutaka tena kuwa mbali na wilaya yake; hakutaka kuwa mbali na mama yake.

Majibu yalipotangazwa Rosa alichaguliwa kwenda shule ya msingi ya Nyakabungo, Mwanza. Huko, Rosa alitegemea kuanza maisha mapya.

# XI

Ukimwuliza mtu wa shamba habari kuhusu maisha yake atakwambia: "Maisha ya shamba ndugu yangu, ni mazuri. Huwa ni baridi. Ubaridi huu unakifanya kichwa kifikiri vizuri. Huko shamba mtu anapata nafasi ya kufikiri bila kelele. Hakuna vumbi. Majani kila mahali na miti yenye maua mazuri hupendeza macho. Maua haya hunukia. Harufu nzuri huingia puani na kupanda mpaka kinywani. Huko shamba ndugu yangu utaona kila kitu kikuavyo—mwanzo na mwisho wa kila kitu. Kama mvua ikikosekana kwa muda mrefu utawasikia watu wakilia 'Mwaka huu kuna njaa.' Utawasikia watu wakilitaja jina la Mungu kwa heshima kwa sababu kila kitu cha shamba hutegemea mvua. Mtu wa shamba huishi pamoja na mifugo. Kwa hiyo uhusiano uliopo kati ya mwanadamu na mnyama, mtu wa shamba anaufahamu. Ukimwona mtu wa shamba anakamua ng'ombe maziwa, utamwona vilevile mtoto mdogo amechutama pembeni akingojea sehemu yake. Ng'ombe au mbuzi akifa huombolezwa. Mtu wa shamba hutokwa na machozi. Mbolea ya ng'ombe, ndugu yangu, ikikauka moto hukokwa. Lo! mji mzima hunukia. Ubani gani uwezao kupita huu! Huku mkojo wa ng'ombe, huko mkojo wa mbuzi, na kule wa beberu—mji mzima hunukia. Marashi gani yapitayo haya! Nikwambie ndugu yangu, huko shamba utawasikia ndege wakiimba asubuhi na mapema. Muziki gani upitao huu!"

"Mimi huwa sili mboga bila mafuta ya samli ndani yake!" Utamsikia mtu wa shamba akisema. "Mtu wa shamba akitoka kutembea mbwa humlaki afikapo nyumbani.Utamwona mbwa anapigapiga mkia wake na kulialia. Wakati akila utamwona mbwa amelala pembeni karibu naye—haingilii. Utamwona vilevile paka amelala upande mwingine. Akimaliza kula mbwa, na paka huingia kula mifupa. Mtoto wa shamba huambiwa asibung'ae wakati wa kula. Yule anayebung'aa utamwona kuku akikimbia na samaki mdomoni na mtoto akimfuata. Mtoto hukata tamaa; hurudi kumwomba mama. Utasikia akikemewa. Tangu awali mtoto wa



shamba hufunzwa kuishi na wanyama, vilevile na ndege. Hafunzwi kuishi na watu tu. Ndugu yangu, watu wa shamba ni watoto wa jua, mwezi, nyota na mvua. Mtoto gani wa shamba asiyekumbuka wakati ule alipokimbia huko na huku uchi wakati mvua ilipokuwa ikinya? Mtu wa shamba huangalia nyota ili apate kulima zao fulani. Mtoto gani wa shamba ambaye hakujivuna kwa sababu alikuwa wa kwanza kuona mwezi! Huko shamba, nani hutoa pesa kuangalia mchezo au ngoma!"

Rosa alikuwa mtoto wa shamba, lakini mawazo haya yote yalikuwa hayamo tena kichwani mwake. Wakati alipochagua shule ya Nyakabungo kama pendekezo lake la kwanza, Rosa hakuwa na mawazo haya: shule yenyewe ilijengwa mjini Mwanza.

Rosa alipopata cheti chake cha ualimu alifurahi sana. Hicho ndicho kilichomfanya akafikiria hila ya kumpata Bwana Albert. Alipokipata kile cheti hakuwa na haja tena ya kujipendekeza kwa mwalimu. Kwa hiyo basi lilipong'oka kuondoka Morogoro kwenda Mwanza, Rosa alitazamia kugeuza maisha yake. Rosa alikuwa hapendi tena kuitwa malaya. Baada ya kufahamiana na watu wengi Rosa aliona heri apumzike. Mambo ya mapenzi yalikuwa hayamstushi tena. Mtu akimwambia "Darling", Rosa aliona ni neno la kawaida na moyo wake hutulia. 'Nikifika Nyakabungo,' Rosa alifikiri, 'hakuna mwanamume yeyote atakayekanyaga ndani ya nyumba yangu. Hakuna mwanamume atakayenichezeachezea.' Haya ndiyo yalikuwa mawazo yake sasa. Haya ndiyo yalikuwa matumaini yake. Lakini shule ya Nyakabungo ilikuwa mjini. Rosa atawaona wapi wanyama? Rosa ataiona wapi mimea? Atapata wapi hewa safi yenye kuvuma polepole na kuingia kinywani mwake ili kusafisha ubongo wake? Zaidi ya hayo, ndege wa kumwimbia kila siku asubuhi na kumnong'oneza siri ya maisha atawasikia wapi?

Rosa, akiwa na matumaini ya kugeuza maisha yake alikwenda Nyakabungo. Alifikiri kwamba atakuta nyumba za walimu. Alipoambiwa na mwalimu mkuu wa shule hiyo kwamba ilimpasa kujitafutia chumba cha kupanga mjini, alishangaa. Mjini Mwanza vyumba vya kupanga vilikuwa vikiadimika sana. Vile vichache vilivyopatikana vilikuwa na kodi ya juu sana. Baada ya siku tatu Rosa alipata chumba kimoja, mtaa wa Lumumba. Hakukaa muda mrefu ndani ya chumba hiki. Sababu aliyotoa ilikuwa kwamba ndani ya nyumba hiyo walikuwa wanakaa wanawake waliokuwa wakifikiri kwamba kila kitu kinaweza kuuzwa, hata magonjwa. Baada ya kugongewa mlango wake mara kwa mara Rosa alihama. "Sipati hata nafasi ya kutayarisha masomo yangu!" Rosa alizoea kunung'unika.

Alihamia mtaa wa Uhuru. Huko alipata chumba kizuri. Rosa alijitunza sana. Watu walifika mara nyingi usiku na kubisha mlango wake, lakini yeye hakufungua hata siku moja. Baada ya muda vijana walianza kumchukia na kumtukana, "Unaringa nini wewe!" walianza kumwambia. Rosa hakujali. Maneno haya yote aliyanyamazia, hayakufua dafu.

Siyo wanaume tu waliomchukia Rosa, bali hata wanawake. Ni hatari zaidi kuchukiwa na mwanamke kuliko mwanamume. Kwa wakati huu Rosa hakuwafahamu adui zake. Rosa hakufikiri kwamba kulikuwa na watu waliomchukia sana. Aliendelea kujitunza.

Rosa alifanya kazi yake ya ualimu vizuri. Akitoka masomoni jioni saa kumi na nusu Rosa alizoea kurudi nyumbani. Afikapo nyumbani huanza kuoga kwanza halafu hurudi chumbani mwake. Rosa alizoea kusoma na kufuma vitambaa. Baada ya mwezi mmoja chumba cheke kilikuwa kimepambwa vizuri sana. Siku moja alipokuwa akioga mwanamke mmoja aliingia chumbani mwake. Rosa hakumwona, lakini wanawake wengine walimwona. Aliingia chumbani kwa Rosa na kutoka kwa haraka sana. Hakutumia hata dakika mbili mle ndani. Alipotoka aliwambia wale wanawake waliokuwa wamekaa nje:

"Rosa akiulizia kalamu yake mwambie kwamba nimeichukua mimi. Nitamrudishia kesho shuleni."

"Wewe nani?" wale wanawake walimwuliza.

"Mwalimu wa Nyakabungo."

"Afadhali ukae. Anaoga, karibu atamaliza."

"Asante lakini nina haraka."

Rosa akiwa ndani ya bafu hakusikia hayo yote. Alipomaliza kuoga, yule mwanamke alikuwa amekwishafika mbali.

"Mgeni wako kafika. Kasema hivi, kalamu yako usiitafute. Atakurudishia kesho shuleni."

"Jina lake nani?"

"Hakutwambia. Kasema tu kwamba yeye mwalimu wa Nyakabungo."

"Mwanamume."

"Hapana, msichana hivi."

Rosa hakuweza kufahamu alikuwa nani. Pale Nyakabungo hapakuwa na mwalimu msichana. Walimu wa kike waliokuwapo walikuwa wote watu wa makamo. Alipoingia chumbani alikuta kalamu yake kweli imechukuliwa. Kalamu hiyo ilikuwa imeandikwa jina lake juu kwa mashine; nayo alipewa kama zawadi na mwalimu Albert. Rosa alikuwa akitumainia kupata kalamu yake kesho yake asubuhi.



Usiku ulipoingia Rosa alitayarisha chakula. Alichukua maji kutoka mtungini na kuweka ndani ya sufuria ili achemshe asonge ugali. Maji yalipoanza kuchemka Rosa alishangaa kuona maji yamegeuka rangi. Yalikuwa na rangi ya bluu. Alifikiri kwamba labda alichemshia kitu fulani ndani yake. Rosa aliyamwaga na kuchemsha mengine. Kabla ya kuweka maji hayo ndani ya sufuria aliyachunguza kwa makini sana. Aliyaona ni meupe na safi kama kawaida. Alipoyachemsha yaligeuka rangi tena. Rosa aliyamwaga maji hayo karibu na mlango—mbele tu ya mlango wake. Aliosha sufuria na kuteka maji mengine kutoka bombani. Alipoyachemsha aliona ni sawa. Alisonga ugali wake, akala, akashiba.

Kesho yake asubuhi Rosa alikuwa bado kitandani aliposikia watu nje wakishangaa: "Asingepona! Asingepona! Hakika huyu mtu angalikufa mara moja. Labda amekufa. Kaite polisi! Kaite polisi!" Rosa aliamka kwenda kuangalia kulikuwa na nini nje. Alipofungua mlango alishangaa kuona kwamba mlango wote ulikuwa umezibwa na kichuguu kikubwa sana. Rosa alipitia dirishani kutoka nje. Hapa ndipo aliposimuliwa na watu waliokuwa nje kwamba sumu hiyo ilikuwa kali sana. Kama watu angalikunywa yale maji angalikufa mara moja, bila hata kukohoa. Watu wengi Mwanza walikuwa wamekwishakufa kutokana na sumu ya aina hiyo. Wale waliopata bahati ya kuitupa au kuimwaga, kesho yake kichuguu kiliota pale ilipotupwa. Rosa alikuwa akitetemeka wakati alipokuwa akielezwa habari hii. Kwa wakati huu hakuweza kumfahamu yule mtu aliyeleta sumu hiyo. Alitumainia kumwona yule aliyechukua kalamu yake.

Rosa alikataa kwenda polisi kabla ya kufanya uchunguzi wake mwenyewe. Alipokwenda shuleni kufundisha aliwauliza walimu wa kike pale shuleni nani alifika kumtembelea jana jioni. Wote walikana kwamba hawakufahamu chumba chake. Alipouliza juu ya kalamu yake walikana kwamba hawakuwa na habari yoyote kuhusu hiyo kalamu. Ingawa aliendelea na uchunguzi wake, Rosa alikaa kwa muda mrefu bila kumfahamu adui wake huyo mkubwa.

Lakini siku moja Rosa alipita karibu na bar moja humo mjini. Alimwona msichana mmoja amesimama mlangoni. Yule msichana alimwangalia sana Rosa. Rosa alipita. Hakufika mbali kabla ya kusikia jina lake likitajwa. Rosa alijifanya kutosikia.

"Mwalimu huyu ninamchukia, sijui kama nini tu!"

"Yuko wapi?" Mwanamke mwingine alitoka nje kumchungulia.

"Mshenzi huyu ndiye aliyeniharibia maisha yangu! Sijui aliponaje. Angekuwa kaburini sasa."

"Alifanya nini?"

"Ndiye alifanya tukafukuzwa shule huko Rosary! Alituchongea! Kama asingalikuwa yeye kutuchongea nisingekuwa nafanya kazi humu ndani ya *bar*."

Rosa alikuwa amekwishafika mbali; hakuweza kusikia zaidi. Aliangalia nyuma kutazama sura ya huyo msichana. Yule mwanamke aliingia ndani ya nyumba upesiupesi. Rosa aliogopa kwenda kumparamia. Alikwenda nyumbani wala hakujisumbua zaidi. Alipofika nyumbani aliuliza zaidi juu ya huyo mwanamke. Aliambiwa na watu waliokuwa wakimfahamu kwamba alikuwa zamani akisoma shule ya wasichana ya Rosary. Aliambiwa jina na mtaa aliokuwa akiishi. Baadaye Rosa alikutana naye sokoni. Rosa alimwangalia kwa makini. Alimfahamu. Kweli alikuwa mmoja kati ya wale wasichana waliofukuzwa. Kwa sasa hakuweza kumsaili: watu walikuwa wengi.

Yule mwanamke alipotoka nje ya soko Rosa alimfuata. Rosa ndiye alikuwa wa kwanza kumwuliza:

"Samahani dada yangu—nafikiri nimekwishakuona mahali fulani, lakini sikumbuki ni wapi."

"Ulipokuwa mwalimu ukatusahau sisi Rosa, Asante!"

"Sura yako naikumbuka ingawa jina nimesahau."

"Maisha yangu uliyaharibu wewe. Namwomba Mola afanye maisha yako yawe kama yangu."

"Ndiyo maana ulitaka kuniua kwa sumu! Bahati nzuri kwamba Mungu hatupilii mbali kiumbe chake—bado ninaishi."

"Kama hawara zako wanataka kukuua usinisingizie mimi!" Rosa alikasirika. Alimshika. Alijaribu kumtupa chini lakini alikuta mwanamke wa *bar* matata. Watu waliokuwa wamekwishakusanyika waliwashika na kuwaachanisha kabla hawajaangushana.

"Acha wapigane!" Kijana mmoja alipiga kelele. "Wanawake wakipigana kazi yao kuvuana nguo—acha tuone! Acha tuone sinema ya bure."

Watu wengine walicheka. Lakini wengine hawakusikiliza maneno yake. Rosa aliongozwa kuelekea njia nyingine, na yule mwanamke alikwenda zake nyumbani.

Siku zilizofuata Rosa alijihadhari sana: aliogopa kufa kwa sumu. Aliendelea na hali yake ya kujitunza. Hakumkaribisha mwanamume yeyote ndani ya chumba chake. Vijana sasa walianza kumwogopa kwa vile alivyokataa kuwasikiliza.



Sifa yake ilivuma sana mjini. Mwishowe ilimfikia mwalimu aliyekuwa akifundisha shule ya msingi ya Kirumba, humohumo mjini. Mwalimu huyo alikuwa mgeni pia; naye alikuwa hajamaliza hata mwaka mmoja kazini. Kwa muda mrefu mwalimu huyu alikuwa amekwishatafuta msichana wa kuoa. Wasichana wote aliokuwa nao zamani aliwakataa kwa sababu walitembeatembea sana na vijana wengine. Alikuwa akimtafuta mwanamke mwenye sifa nzuri kama Rosa. Aliposikia sifa ya Rosa aliulizauliza nambari ya chumba chake na barabara hata mwishowe akakifahamu.

Rosa alikuwa akinyoosha nguo zake aliposikia mtu anabisha hodi mlangoni. Kwa kuwa ilikuwa mchana kama saa kumi na nusu, Rosa alifungua mlango. Alipofungua mlango kijana mwembamba mwenye ndevu nyingi aliingia. Ilikuwa kama kwamba Rosa alikuwa akiota. Yule kijana alimtazama machoni. Ndani ya macho ya kijana huyu Rosa aliweza kuona maisha yake ya mbele. Macho yake yalionekana kuwa yenye huruma. Rosa alianza kusema moyoni: 'Huyu kijana si kama wengine; nafikiri analeta habari njema. Mungu amjalie ataje lile neno—' Rosa alikuwa hamfahamu yule kijana, lakini machoni mwake aliona mchumba; alimwona bwana wake katika ndoto.

"Karibu kiti," Rosa alisema kwa upole.

"Asante lakini nina haraka."

"Karibu tuongee."

"Asante. Nina ujumbe mfupi tu."

Alitoa barua na kumpa Rosa. Rosa alipokea. Yule kijana aliaga na kwenda zake kabla Rosa hajaisoma. Rosa alipoifungua barua aliangalia jina la mwandishi kabla ya kuisoma. Alisoma jina la Charles Lusato. Rosa alikuwa amekwishasahau mahali alipoliona hili jina. Baada ya kufikiri alikumbuka kidogo kwamba jina hili alikuwa amekwishaliona ndani ya barua fulani. Rosa alikuwa amekwishaandikiwa barua nyingi vile kwamba hakukumbuka Charles Lusato alikuwa nani. Zamani Rosa alikuwa na marafiki wengi hata hakumkumbuka Charles.

Barua yenyewe ilikuwa ya mapenzi. Charles hakuficha haja yake. Alimwandikia Rosa wazi kwamba alikuwa akitafuta mwanamke wa kuoa. "Rosa, nimeona kwamba ni wewe," Charles aliandika. Aliendelea: "Nimekuona mara nyingi humu mjini ukiwa mbali; lakini nilikuwa bado sijapata ujasiri wa kuweza kuandika barua."

Rosa aliona afadhali ajaribu bahati yake mara ya mwisho. Sasa aliona kwamba kuombwa kidole cha pete na mvulana ni jambo kubwa ambalo

halitokei mara nyingi. Rosa alifikiri: 'Kijana huyu lazima anioe; nikimkataa huyu basi maisha yangu yamekwisha; sina tumaini tena.' Rosa alikata shauri kupiga mshale wake wa mwisho. 'Mshale huu ukienda pembeni, basi jitu—maisha—litaniua,' Rosa aliwaza moyoni.

Usiku mzima Rosa alimfikiria huyu kijana. Kwa ghafla alikumbuka kwamba aliwahi siku moja kusoma na mtu fulani jina lake Charles, na kwamba wakati ule alikuwa bado darasa la saba. Kadiri alivyofikiri sana ndivyo alivyozidi kupata fununu zaidi juu ya Charles. Alikumbuka hadithi yote. Alikumbuka jinsi alivyokuwa amezoea kwenda kusoma pamoja na kijana huyo; alikumbuka ile barua; alikumbuka jinsi alivyopigwa na baba yake; alikumbuka jinsi alivyopelekwa nyumbani kwa Ndalo usiku. Alimwona baba yake akimtupia Charles vishilingi vyake vitano. Kadiri alivyopata nuru ndivyo mapenzi yake yalivyoongezeka. Rosa aliona kwamba huyo ndiye alikuwa mumewe aliyeandikiwa na Mungu tangu awali.

Kesho yake jioni Charles aliporudi Rosa alikuwa amekwishakata shauri. Charles alipoingia chumbani mwake Rosa alimwangalia vizuri: aliona ni yuleyule Charles wa zamani isipokuwa ndevu. Rosa alimkaribisha ndani. Charles alipokaa, Rosa alimwambia alikuwa hawezi kumjibu kwa mdomo. Alitoa barua mezani na kumpa; lakini alimwambia asiisome wakati ule. "Utaisoma baadaye ukiwa peke yako nyumbani," Rosa alisema. Charles aliendelea kuongea bila kufahamu ndani ya barua kulikuwa na nini. Charles alijiona mjinga. 'Siwezi kuzungumza bila kufahamu kama jibu ni baya au zuri,' Charles alisema moyoni. Aliomba ruhusa kwenda kujisaidia. Rosa alimwonyesha mahali pa kwenda. Alipokuwa huko Charles alifungua ile barua. Ndani yake alikuta karatasi moja kubwa. Mikono ilikuwa ikimtetemeka. Juu ya karatasi Charles alikuta maneno machache tu.

*Mpenzi Charles,*

*Aksante sana kwa barua yako. Nichukue na unikumbatie kati ya mikono yako. Mimi ni wako wa maisha. Ninakupa moyo wangu; nakupa pumzi yangu, pumzi yangu ya maisha. Mimi ni wako katika kila jambo. Hapa ninakupa mkono wangu. Mpenzi, uchukue mkono huu na uniongoze katika bonde hili la machozi.*

*Akupendaye daima,*
*Rosa*



Charles alitosheka. Alifurahi. Alipata jibu alilokuwa akitegemea. Alirudi chumbani hali akitabasamu. Alipokaa Rosa alianza kuzungumza.

"Charles unanikumbuka?"

"Kusema haki nilikuwa nimekusahau. Lakini jana, mara tu nilipokuona ukiwa karibu nami, nilikukumbuka."

Rosa alimwangalia Charles machoni. Macho yake yalionyesha mapenzi. Charles alifahamu. Alimsogelea, alimkumbatia na kumbusu. Walikaa katika hali hii kwa muda mrefu. Waliachana, walikaa.

"Rosa," Charles alisema, "Rosa, unakumbuka siku ile?"

"Siku gani?"

"Siku ambayo mapenzi yetu yalikatwa kwa nguvu yakingali mabichi?"

"Ninakumbuka. Lakini ng'ombe hula majani na mengine huota. Moto huchoma majani na majani mazuri zaidi huchipuka."

"Rosa, unamwunga mkono baba yako. Unafikiri watu wachomao majani moto hawaingilii hali na maumbile ya vitu?"

"Charles, tendo la baba limeniumiza kuliko unavyofahamu. Ah Charles, kama tu wazazi wangalifahamu kwamba tendo lao moja linaweza kuharibu maisha ya watoto wao, wangejua ugumu wa madaraka yao na uangalifu uwapasao."

"Rosa." Charles aligeuza mazungumzo, "Ulikuwa wapi tangu wakati tulipoachana?"

Rosa alisimulia habari za Rosary na Morogoro TTC. Charles alisimulia habari za Mkwawa na Marangu TTC. Waliagana saa sita usiku.

Hivyo ndivyo Rosa alivyopata kukutana na rafiki yake wa zamani. Hivyo ndivyo alivyopata mchumba tena. Rosa aliona maisha yake yametengemaa. Na Rosa kweli alimpenda sana Charles. Kesho yake Rosa ndiye alikwenda kumtembelea Charles.

Charles alimkaribisha vizuri mgeni wake. Rosa alipomaliza kunywa chai aliona nguo fulani zimetundikwa ukutani. Alizichukua.

"Chumba cha kufulia nguo kiko wapi?" Rosa aliuliza.

Charles alimnyang'anya, "Bado ungali mgeni mheshimiwa sana," alisema kwa upole.

Rosa alianza tena maisha ya mahaba. Charles pia alimpenda sana Rosa. Mara nyingi alimchukua kwenda dansini kwenda senema, pia kwenda nje ya mji kupunga hewa. Hata mwishowe watu walikiri kwamba uchumba wao ulikuwa wa moyoni na wala si wa mdomoni tu. Wale watu ambao kazi yao ni kuharibu uchumba wa watu wengine waliona kazi bure kujaribu kutenganisha maji na chumvi.

Rosa alifika kumtembelea Charles mara nyingi zaidi. Huko nyumbani

walizoea kubusiana. Siku moja wakiwa katika hali hii, Charles alimwangusha Rosa juu ya kitanda. Charles alikuwa katika hali mbaya. Rosa alikuwa amefumba macho: alikuwa naye amekwisha. Charles alifunga milango na madirisha. Rosa alikuwa bado amelala juu ya kitanda akipumua kama njiwa. Charles alianza kumbusu; waligeuzana huku na huko juu ya kitanda. Charles alianza kuvuta gauni la Rosa juu polepole sana. Rosa alihisi mkono wa Charles ukimgusa. Ulikuwa umefika mbali mara wazo lilipomjia Rosa kichwani. Aliushika mkono huo na kuurudisha pole pole.

"Charles siyo leo."

"Mpaka lini?"

"Mpaka siku tutakayooana. Afadhali tungoje siku yenyewe."

"Haiwezekani."

"Vumilia kidogo muda umekaribia. Ninakuomba usiniharibu kabla ya muda. Charles—mimi ni bikira."

Rosa alitamka maneno ya mwisho kwa shida na kusitasita. Charles aliposikia maneno haya alikufa ganzi. Hakuwa na hamu tena ya kumpapasapapasa Rosa.

"Wewe ndiye msichana ambaye nilikuwa nikimtafuta kwa muda mrefu. Rosa, ninakupa heshima yangu yote."

Waliachana. Rosa alilisema lile neno gumu kutaja kuliko yote katika ulimwengu wa sasa. Na Charles aliamini: alikumbuka siku ile Rosa alipopigwa na baba yake; alikumbuka jinsi Rosa alivyojitahidi kutozungumza naye. Charles alimpenda zaidi na zaidi, hasa kwa sababu hii. Tangu siku hiyo alimheshimu sana mchumba wake. Aliogopa hata kumbusu. Alingojea siku ya ndoa.

Uchumba wao ulijulikana. Vijana wengi—kama ilivyo kawaida yao—walianza kuzungumza juu ya uchumba huu kana kwamba ulikuwa wao. Mwishowe kijana mmoja alijitolea kwenda kuzungumza na Charles. Alifika kumchukua Charles nyumbani kwenda kunywa pombe *bar*. Yule kijana alikuwa pia mwalimu humohumo mjini. Rosa alikuwa hajapata kumwona. Charles alipata kufahamiana na kijana huyo katika unywaji wa pombe. Walikwenda *bar* ambako watu wengi walikuwa hawanywei. Baada ya kunywa chupa mbilimbili, yule kijana alianza kumwambia:

"Charles, nimesikia umepata mchumba."

"Nani amekwambia?"

"Sisi tunasikia tu. Hatujui kama ni kweli?"

"Waliokwambia wamekudanganya."



"Charles, kama umenificha siri yako, nami sitakwambia maneno niliyotaka kukujulisha. Nina jambo kubwa sana la kukwambia."

"Jambo gani?"

"Kuhusu mchumba wako."

"Hivi nani amekwambia."

"Basi, tunywe pombe, tumalize, twende zetu."

"Huwezi kwenda kabla hujaniambia hadithi yako."

"Anza kwanza kuniambia hadithi yako."

Charles alianza kueleza ya kwake yote: maisha yake na msichana huyo walipokuwa bado watoto wadogo; jinsi walivyoachana; na jinsi walivyokutana tena mjini Mwanza. Alipomaliza hadithi yake yule kijana aliagiza chupa mbili zaidi.

"Ninakuonea huruma sana," yule kijana alianza kusema. "Huyo mwanamke si wa kuoa. Kama unaniamini afadhali umwache tangu kesho. Rosa!—siyo Rosa jina lake?" Charles alitikisa kichwa. "Sasa, unafikiri mimi nilimfahamuje. Alinikinai! Tulipokuwa Morogoro alikuwa anagawa kweli!"

"Eh?" Charles alishangaa.

"Ninakwambia ukweli mtupu. Haki ya Mungu huyo msichana mwishowe alitaniwa 'Lab'—*Laboratory*—ndilo lilikuwa jina lake.

"Tena mimi aliniambia juzijuzi kwamba yeye ni bikira bado!"

"Alikwambia kwamba yeye ni bikira! Ha! ha! ha! ha! ha! ha! Yuyu! Yuhu." Yule kijana **alicheka. Alishikilia mbavu. Charles alijiona mjinga.** Yule kijana aliendelea kumweleza uhusiano uliokuwapo kati ya Rosa na mkuu wa shule. Alimsimulia jinsi Rosa alivyochungulia kaburini kwa sababu ya kutoa mimba.

"Lakini lazima uwe macho!" Yule kijana alimwonya. "Wanawake wengine wanatembeatembea ovyo; siku ya kuolewa utasikia bwana zao wakisema ni mabikira! Wanawake kama hao hutumia dawa. Nimekwisha sikia wanawake wengi wa namna hii. Huenda Rosa pia atatumia dawa siku ya ndoa." Yule kijana alipomaliza kumpa maoni haya alimaliza glasi yake. Charles naye alimaliza yake.

Walipoachana Charles alikwenda akifikiri, lakini maneno haya alikuwa hajayaamini bado. Alifikiri kwamba yule kijana alikuwa kati ya wale vijana waliokuwa wakimwonea wivu. Baada ya siku mbili aliyaona maneno haya kuwa ya upuuzi. Lakini sentesi moja ilikuwa bado ikimsumbua: "Huenda Rosa atatumia dawa siku ya ndoa."

Rosa aliendelea kumtembelea Charles kama kawaida. Charles alien-

delea kumheshimu. Lakini yule kijana hakuwa wa kwanza na wa mwisho kumweleza Charles hasara atakayoipata kama akimwoa Rosa. Kijana mwingine alipata kumsimulia Charles hadithi za Rosa wakati alipokuwa bado Rosary. Alisimulia jinsi alivyofukuzwa shule. Alimsimulia jinsi Rosa alivyokuwa akirandaranda mjini na maafisa. Haya yote—kwa jinsi Charles alivyompenda na kumwamini Rosa—yaliingia sikioni mwake na kutoka upande mwingine. Maneno mengine aliyoyafikiria kwamba kulikuwa na ukweli ndani yake, aliyameza. Alivumilia: alikuwa amekwishakata shauri kumwoa Rosa—bikira.

Kama kweli Rosa hakuwa bikira hili halikuwa kosa lake. Yeye alisema. Alifahamu kwamba alimdanganya mchumba wake. Mwanamke ukishamwambia kwamba wewe mchumba wake, atakuheshimu sana. Hatakuruhusu. Na Rosa, hata kama angalimruhusu vilevile angalipoteza bahati yake. Rosa alikuwa akilenga shabaha. Alimlenga mnyama wake. Mwindaji akibakiwa na mshale mmoja hutafuta mti mkubwa ili mradi akimkosa apande upesi kabla mnyama hajamla. Hivyo ndivyo Rosa alivyofanya.

Na Charles je? Yeye katika maisha yake alipoteza muda wake kwa kutafuta mabikira wa kuoa. Zaidi ya hayo alizoea kuwaomba uchumba siku ya kwanza kuonana nao. Hivyo ndivyo alivyofanya hata kwa Rosa. Siku ya kwanza kabisa Charles alitaka uchumba. Alimwandikia ndani ya barua. Alimwomba kidole cha pete. Uchumba huja baada ya urafiki wa muda mrefu, na kama uchumba ukianza na baadaye urafiki, wasiwasi mwingi hutokea.

Siku zilizofuata, Rosa alimshikilia mchumba wake. Alisahau kila kitu kuhusu kina Thomas na Deogratias. Rosa hakutaka uchumba wa muda mrefu: aliogopa kumpoteza Charles. Kwa hiyo siku aliyomtembelea tena Charles, alimwuliza swali moja la maana.

"Charles," Rosa alianza, "nafikiri tumekuwa wachumba kwa muda mrefu wa kutosha."

"Hata mimi nilikuwa nikifikiria swali hilo. Nilitarajia kukuuliza leo. Mimi niko tayari wakati wowote upendao wewe.",

"Mimi ningependa tufunge ndoa baada ya miezi miwili."

"Afadhali uniongezee muda," Charles alisema. "Nipatie muda wa miezi minne. Unafahamu Rosa, wazazi wangu maskini sana. Kwa hiyo ingefaa uwapatie muda mrefu wa kuweza kujiandaa vizuri zaidi."

Wachumba hawa wawili walizungumza mengi kuhusu mpango wao wa arusi. Walikubaliana kwenda kuwaona wazazi wao nyumbani baada ya mwezi mmoja.



# XII

Siku zilizofuata baada ya kufanya mpango wao wa ndoa na kabla ya kwenda nyumbani kuwaona wazazi wao hazikuwa nzuri sana kwa upande wa Rosa. Maafa yalifuata. Maafa baada ya maafa. Kwani hazikupita siku nyingi Rosa alipokuta huko ofisini shuleni barua juu ya meza yake. Kalamu ilikuwa imewekwa juu ya barua hiyo ili isije ikiapeperusha na upepo. Rosa alifahamu kalamu yake. Alipoiona alifurahi sana. Alipoangalia ile barua aliona pia kwamba ilikuwa yake. Aliichukua. Aliifungua na kuisoma. Rosa hakuamini maneno aliyosoma. Barua hiyo ilimwomba ahame mtaa wa Uhuru upesi iwezekanavyo. "Usipohama dada yangu, utakufa baada ya siku mbili," barua hiyo ilimalizia.

"Nani ameleta barua hii?" Rosa aliwauliza walimu.

"Mtoto mmoja; hatumfahamu."

Rosa alinyamaza. Rosa siku hiyo hakufundisha. Alikwenda kupasha habari polisi. Rosa alitaja jina la adui yake. Yule mwanamke aliitwa. Aliambiwa kuandika karatasi kumi tofauti. Mwandiko wake ulikuwa tofauti kabisa na ule wa barua. Aliambiwa kutumia mkono wa kushoto, mwandiko wake pia ulionyesha tofauti kubwa. Baadaye polisi ilifanya uchunguzi zaidi lakini haikupata ushahidi wa kuweza kufanya kesi ya Rosa isimame. Rosa aliambiwa ahame na kama jambo kama hilo likitokea tena aliombwa apashe habari mapema.

Alisikiliza maoni yao. Rosa alihama. Hakuwa na mahali pengine pa kuhamia isipokuwa kwa mchumba wake. Rosa alikwenda kuishi pamoja na mchumba wake Charles. Ingawa mtaa wa Kirumba ulikuwa mbali na shule yake, Rosa aliona afadhali kuishi kuliko kufa. Aliendelea na kazi yake ya kufundisha. Wachumba hawa wawili walilala chumba kimoja, lakini hata hivyo waliweza bado kuheshimiana: kila mmoja alilala kitanda chake.

Mwezi waliokuwa wameahidiana kwenda nyumbani kuwaona wazazi wao ulikuwa umekaribia. Charles na mchumba wake walipanga siku ya kuvuka kwenda kisiwani Ukerewe. Walikwenda kuomba ruhusa kutoka

kwa mkuu wa elimu wa mkoa. Naye hakukataa. Aliwaruhusu. Aliwapa muda wa juma moja.

Rosa alimwandikia Flora barua. Alimpasha habari kwamba alikuwa amekwishahama na kwamba alikuwa sasa akiishi na mchumba wake. Ilikuwa barua ndefu sana. Rosa alijitahidi sana kumsifia Charles. "Karibu tutakwenda nyumbani. Fika kwangu Jumapili," Rosa alimwomba dada yake. Rosa alimwambia mchumba wake kwamba dada yake atafika kumtembelea.

Flora alipofika alimkuta Charles amejiandaa, tayari kumpokea. Alifika jioni saa tisa na alipaswa kurudi alikotoka kabla ya saa kumi na moja. Kwa hiyo alipomwambia Rosa juu ya muda wa kukaa aliokuwa nao, Rosa alimtayarishia chakula upesi. Wakati Rosa alipokuwa akisonga ugali Charles alikuwa akizungumza na Flora.

"Habari za huko jela," Charles alianza kumwuliza.

Flora aliona kwamba Charles alikuwa hafahamu vizuri mahali alipokuwa akiishi sasa. Hata hivyo alijibu.

"Kule kwetu jela pazuri."

"Labda wewe unaweza kuniambia: kwa nini wasichana wengi wa shule yenu wanapata mimba zaidi kuliko shule zingine?"

"Sababu yenyewe nafikiri ni kwamba hatuna uhuru wa kutosha. Tunachungwachungwa sana."

"Hapo nakubaliana nawe. Hampati uhuru wa kutosha. Hata kama mkichungwa mimi nafikiri itafaa zaidi kama uchungaji utafanyika kwa busara. Lakini wanavyofanya sasa ni kazi bure."

"Unamaanisha nini usemapo kwamba uchungaji ufanywe kwa busara?"

"Uchungaji wenye busara ni ule unaofikiria hali ya mtu ilivyo—kwamba hali ya mtu haimruhusu akae kwa muda mrefu bila kuzungumza na mtu mwingine asiyefanana naye. Uchungaji ufanywe kwa kiasi. Uchungaji wa kiasi hauwezi kumkataza msichana asizungumze na wavulana. Hawa ndio watu atakaoishi nao baadaye. Ninasema hivi kwa sababu tulikuwa na wasichana fulanifulani kutoka shule yenu na wote walionekana kuwa na mimba baada ya miezi mitatu. Ni wazi. Kama msichana amezoea kuchungwa akienda shule kama TTC—shule ambazo wavulana na wasichana wanasoma pamoja—hawezi kuishi na wavulana. Hawakuzoeana."

"Sasa wewe unafikiri serikali ingefanya nini ili kuzuia mimba?"



"Serikali haiwezi kuzuia mimba. Inaweza tu kuwazuia wasichana wasitembee. Lakini siyo kuzuia mimba. Wakienda nyumbani je?"

"Serikali inasema kwamba tukienda nyumbani tuko chini ya wazazi wetu."

"Kwa hiyo mkipata mimba nyumbani serikali haina lawama!"

"Haina, inasema."

"Baada ya kuwachunga muda mrefu shuleni! Mimi naona kwamba jambo la kupata mimba linategemea malezi ya msichana alipokuwa bado mtoto mbichi, na hali yake mwenyewe. Zaidi ya hayo ninaona kwamba watu wakubwawakubwa ndio wapatiao wasichana mimba. Wala siyo wanafunzi. Wanafunzi mara nyingi husingiziwa tu. Lakini hata kama mwanafunzi akimpatia mwenzake mimba, wanaweza bado kuoana. Wafanyakazi wakubwa, wengi wameoa."

Charles alipaswa kukatisha maneno yake: Rosa alikuwa amemaliza kuandika meza.

"Karibu mezani," Rosa alimwambia dada yake. Flora aliinuka kwenda mezani. Hakukubali kula peke yake. Charles alikula pamoja naye. Rosa alikataa. Alikaa pembeni.

"Nimesikia kwamba watu wamekufa wengi juzijuzi," Flora alianza kusema.

"Ndiyo," Rosa alijibu, "Juzi mtu mmoja aliuawa huko sehemu za Mabatini, na jana mwingine aliuawa hapa Kirumba. Wote hao wameuawa kwa sababu ya kutembeatembea na wake za watu."

"Lakini," Charles alisema, "nafikiri Flora alipouliza alikuwa akifikiria watu watano waliokufa ghafla kwa sababu ya ugonjwa wa miguu."

"Hapana. Wewe hukumwelewa. Bila shaka ni wale waliouawa." Flora, ingawa alikuwa akiulizia wale watano, alinyamaza.

"Huo ndio ubaya wa Charles. Anajidai kwamba yeye anafahamu kila kitu."

"Uwongo wako."

"Ndiyo. Jana tu uliniambia kwamba unaweza kusoma mawazo ya mtu." Charles alinyamaza. Rosa alijiona ameshinda.

"Hao watu niliowasema, polisi bado wanafanya uchunguzi. Lakini wale watano waliokufa kwa ugonjwa wa miguu hakuna anayeshughulika." Charles aliona afadhali kugeuza mazungumzo.

"Shemeji, tunakwenda kesho nyumbani. Kama una ujumbe wa kupeleka nyumbani mwambie dada yako."

"Rosa aliniandikia barua zamani. Nimemletea barua zangu ili azipeleke nyumbani. Moja ni ya mama na nyingine ya Honorata."

"Honorata ndiye nani?"

"Dada. Anayenifuata mimi. Nimemnunulia Emmanuel nguo na kimotokaa cha kuchezea. Hivyo pia Rosa atavipeleka."

Walimaliza kula. Rosa alitoa vitu mezani. Mara tu baada ya kunawa mikono, Charles alileta chupa moja ya mvinyo ya aina ya "Grenado." Charles alikunywa kidogo. Flora alikunywa lakini kiasi tu. Aliogopa asije akafokewa nyumbani. Rosa alikunywa kwa pupa. Alikuwa akijikumbusha maisha yake ya zamani. Zamani aliweza kunywa chupa saba za bia. Zamani mvinyo ulikuwa haumleweshi sana. Chupa ya kwanza ilipokwisha, Charles alileta ya pili. Hii chupa ya pili ilimalizwa karibu na Rosa peke yake. Charles alimwacha mchumba wake anywe.

"Kunywa tu. Huu ni mji wako," Charles alimwambia.

"Nikilewa nani atakupikia?"

"Mimi mwenyewe."

"Hapana—*Darling* wangu—hapana."

Rosa alikuwa amekwishaanza kupatwa. Aliweka kichwa chake juu ya kifua cha Charles.

Flora aliangalia saa yake. Aliona muda wake wa kurudi nyumbani umewadia.

"Ninataka kwenda."

"Sasa hivi!" Charles alishangaa.

"Lazima niende. Haya kwaherini."

"Unakwenda?"

"Charles, lazima niende."

"Ngoja nikusindikize."

"Mimi sifiki mbali," Rosa alisema. "Kwaheri. Ufike salama."

"Haya kwaheri. Uwasalimie nyumbani."

Charles alimsindikiza hadi kituo cha basi. Kwa bahati nzuri wakati uleule basi lilifika. Flora alipanda kwenda mjini. Flora alikwenda ametosheka. Alikuwa na haja ya kumwona mchumba wa dada yake. Alimwona. Alimwona Charles kuwa mtu mpole, mkarimu na mzungumzaji. 'Lakini hampiti John wangu,' Flora aliwaza. 'Tena Charles mkondefu kidogo.'

Alipokwisha kumwona Flora anakwenda, Charles alirudi nyumbani. Alikuwa bado akishangaa. Hakutegemea kwamba Flora atapanda basi kwenda mjini. Alimfikiria kuwa bado mtoto wa shule. Lakini Flora alikuwa amekwishamaliza darasa la kumi na mbili. Siku waliyofunga shule Flora hakwenda nyumbani. Alichukuliwa na rafiki yake, John, aliyekuwa akiishi kwa kaka yake humohumo mjini. Huko ndiko sasa



Flora alikokuwa akiishi pamoja na mchumba wake. Watu wengi walisema kwamba Flora alikuwa akiishi kama kimada. Flora hakuonyesha alama yoyote ya kupata mimba. Majibu yake ya mtihani wa Cambridge yalipokuja Flora alikuwa palepale nyumbani. Majibu hayakumstusha hata kidogo. Flora alishindwa, hata GCE hakupata. "Tutajali nini sisi hali tumekwishajikabidhi!" Huo ndio uliokuwa msemo wake wa kawaida alipokuwa akiulizwa matokeo yake ya mtihani. Watu walipomwambia, "Watakuja kukukataa karibuni," Flora aliwajibu. "Tuliyazungumza tukayamaliza."

Haya yote Charles alikuwa hajayafahamu. Alimfikiria kuwa bikira kama dada yake. Charles alipofika nyumbani alimkuta mchumba wake taabani amelala kitandani: macho yake yalikuwa yemefungwa, na pumzi yake ilikuwa haisikiki. Alionekena kama mfu. Charles alimtikisa ili kumwamsha. Rosa alifunua macho mara moja tu na kuyafunga tena. Charles alichukua kitabu na kuanza kusoma. Rosa alikuwa amelala mguu mmoja ametupa huku mwingine huko, na mapaja yake yaliyokuwa yamenawiri yalikuwa wazi. Charles alimlaza vizuri na kumfunika. Aliendelea kusoma kitabu chake.

Mambo yote yangekwenda vizuri kama Charles asingeingiliwa na shetani. Alipata tamaa mbaya. Siyo tamaa mbaya tu iliyomfanya Charles akaangusha kitabu chini wakati wa kusoma lakini hasa fikira mbaya. Charles alikumbuka maneno aliyoambiwa na yule kijana. Aliyakumbuka yote barabara:

"Lakini lazima uwe macho. Wanawake wengine wanatembeatembea ovyo; siku ya kuolewa bwana zao wanasema walikuwa mabikira. Wanawake kama hao hutumia dawa. Nimekwishasikia wanawake wengi wa namna hii. Inawezekana kwamba huenda Rosa pia atatumia dawa siku ya ndoa."

Dhamiri yake ilimsumbua. Alianza kufikiri. 'Bila shaka Rosa amelewa sana; sidhani kwamba ataweza kujitambua kesho. Sidhani kwamba yumo katika hali ya kuweza kunizuia. Nafikiri huu ndio wakati wa kuhakikisha. Labda nitafanya vibaya. Hapana. Rosa hatafahamu: amelewa sana' Charles alikwenda kitandani. Alisikia sauti moyoni mwake. 'Charles unafanya vibaya. Unatenda dhambi.' Moyo wake ulianza kumdunda. Charles alitembea bado. Alifika kitandani. Alimshika Rosa. Alishika kichwa chake kwa mikono miwili. Alikitikisa kwa nguvu. "Rosa! Rosa! Amka! Amka! Amka chakula tayari!" Rosa alikuwa amelala fofofo. Wala hakutoa sauti yoyote. Alimshika tena. Mara hii alimshika polepole. Charles alimwona amelewa sana. Aliona kwamba alikuwa amepoteza

fahamu yake yote. Alimbusu. Charles alipata shida. Alianza kuvua viatu. Alivua suruali. Alipanda kitandani. Alipandisha gauni la Rosa juu mpaka kifuani. Charles aliona kwamba mlango na dirisha vilikuwa bado wazi. Aliamka. Alikwenda kufunga mlango na dirisha. Alivuta mapazia. Alirudi tena kitandani. Rosa alifunua macho. Charles aliogopa: "Nisamehe" Charles alisema. Rosa alitoa pumzi ndefu sana. "M—mhum!" Charles aliogopa zaidi. Lakini Rosa hakufumbua macho tena. Charles alitoa nguo ya Rosa ya mwisho na Rosa sasa alikuwa uchi. Charles pia alitoa nguo yake ya mwisho. Aliona shati linaleta fujo. Alilivua. Aliona fulana inaleta fujo. Aliivua.

Baada ya muda, Charles alionekana akijipangusa jasho. Baada ya kujipangusa jasho alionekana akimbeba Rosa kutoka kitandani. Alimlaza chini, juu ya sakafu. Alimwosha. Alifanya hivi ili Rosa asije akatambua yaliyotokea baada ya kunywa. Charles alileta taulo. Alimsafisha vizuri. Alimlaza tena kitandani. Jogoo aliwika. Aliwika kabla ya muda wake wa kawaida. Charles alimsikia. Aliangalia saa yake. Aliona kwamba zilikuwa bado saa tano.

Giza lilikuwa limekwishaingia Rosa alipoharibiwa 'ubikira' wake. Giza lilikuwa limekwishaingia Charles alipohakikisha kama Rosa alikuwa kweli bikira au hapana. Sasa giza lilikuwa likitanda mbele ya wachumba hawa wawili. Charles alivumbua siri kubwa. Aliona kilichomfanya kuku kukosa maziwa. Aliona maajabu.

Kesho yake asubuhi Rosa alikuwa wa kwanza kuamka. Alijikuta amelala juu ya kitanda chake na gauni lake mwilini. charles alikuwa bado amelala. Rosa alianza kushangaa ilikwendakwendaje hata akalala na gauni lake Alikumbuka.

"Charles, Charles!"

"Mm"

"Flora alikwenda saa ngapi?"

Charles alijinyosha. Alipitisha mkono wake machoni.

"Usingizi ulikuwa bado umenipata. Unasemaje?"

"Flora alikwenda saa ngapi?"

"Nilimsindikiza saa kumi na nusu hivi."

"Pombe ilikuwa kali sana. Sijalewa maishani kama jana."

"Hukulewa sana. Tulikunywa pamoja."

"Kweli! Mimi hayo yote sikumbuki."

Siku hiyo waliendelea kulala mpaka saa tano: walikuwa bado na mavune kana kwamba walifanya kazi ngumu. Jioni walianza kutayarisha vitu vya kwenda navyo nyumbani.



# XIII

Wakati wachumba hawa wawili walipokwenda nyumbani kuwaona wazazi wao ulikuwa wakati mbaya katika sehemu ya kaskazini ya Tanzania. Maafa kila mahali yalitokea. Ugonjwa mpya ambao ulikuwa haujulikani chanzo chake ulizuka. kani chanzo chake ulizuka. Ugonjwa huu ulipewa majina mengi: Usukumani watu waliuita ugonjwa wa magunia kwa sababu watu walipougua walijaribu kufunga miguu yao kwa magunia; huko Musoma uliitwa funyafunya; Ukerewe uliitwa ugonjwa wa miguu tu. Ulikuwa ugonjwa mbaya sana. Mtu aliweza kuonekana asubuhi akizurura, lakini jioni utasikia amefariki. Nini? Utaambiwa ugonjwa wa miguu. Maumivu ya ugonjwa huu yalianzia kifuani, halafu hutelemka mgongoni mpaka magotini. Hapo ndipo mtu hukosa nguvu, huanguka chini; na kama asipofikishwa hospitali kabla ya saa mbili, hufa. Kwa siku moja watu watano au sita hivi waliweza kufa katika wilaya moja. Kwa kuwa kifo huogopwa, utafikiri watu mia walikufa. Watu walijaribu kutafuta sababu ya ugonjwa huu kwa kufikiri tu, bila kupima. Walisema: "Tumesikia siku hizi Mfaransa amelipua bomu lake huko jangwa la Sahara. Bila shaka bomu hilo ndilo limeleta ugonjwa huu." Ingawa kweli Wafaransa walikuwa wakifanya majaribio yao huko Afrika ya Kaskazini, hiki—kama madaktari walivyosema—hakikuwa chanzo cha ugonjwa huo. Ugonjwa huo ulisemekana kuwa aina fulani ya malaria. Mambo haya yote Charles na mchumba wake waliyasikia melini wakielekea Ukerewe.

Huko Ukerewe ugonjwa huu uliogopesha sana watu. Watoto wa shule waliokuwa wakisoma ng'ambo—yaani nje ya kisiwa—waliogopa kwenda likizo nyumbani kwao—waliogopa kufa. Kwa kuwa Ukerewe ni kisiwa kidogo ambapo watu wengi wanaishi, ugonjwa huu ulienea kwa urahisi na uliua watu wengi zaidi. Karibu kila kijiji watu walikuwa wakiomboleza vilio vya watu watatu au wanne kila mwezi. Ile tabia ya kwenda kilioni na kulala huko mwishowe haikufuatwa. Hadithi za watu waliokwenda mazikoni na kufia huko zilikuwa zikisimuliwa. Sababu ya ugonjwa huu

ilipovumbuliwa, kazi ya kuwatibu watu wote ilianza. Watu wote, wazima kwa wagonjwa, walipigwa sindano. Kila nyumba ilinyunyiziwa dawa ya kuua mbu na wadudu wengineo. Baada ya muda ugonjwa huo ulikwisha. Watu walianza kusema mioyoni mwao: 'Christimas ya mwaka huu nitaila.'

Charles na Rosa walipofika kisiwani ugonjwa huu ndio ulikuwa ukianza. Walipotoka Mwanza walikuwa wamesikia vifo vya watu wengi. Jamaa zao pia walikuwa wamekwishakufa. Charles alisikitika sana aliposikia juu ya kifo cha Ndalo, mjomba wake. Hata Rosa pia alisikitika kwani Ndalo alikuwa ni jirani yao. Alifahamu kwamba Regina alikuwa na masikitiko makubwa. Alifahamu kwamba Bigeyo alikuwa na masikitiko makubwa zaidi.

Charles aligeuza safari yake. Mwanzoni alikuwa amekusudia kwenda moja kwa moja hadi Itira kumwona baba yake, lakini sasa alikwenda mpaka Namagondo. Rosa alikwenda naye. Yeye alikuwa hasa akienda nyumbani kuwaona wazazi wake. Alikuwa hasa na nia ya kuwaonyesha mchumba wake. 'Bila shaka baba atafurahi kumwona mchumba wangu na atasahau makosa yote niliyomtendea zamani.' Haya ndiyo yalikuwa mawazo ya Rosa. Kwa wakati huu hakufikiri sana juu ya kifo cha Ndalo ingawa kweli kilimsikitisha.

Siku hiyo waliyofika ndiyo ilikuwa siku ambayo Ndalo alifariki. Alifariki asubuhi kwa sababu ya ugonjwa wa miguu. Alikufa ghafla. Charles alipokaribia mji alishika mfukoni mwake na kutoa barua moja. Charles alimpa Rosa barua hii; lakini alimwomba asiisome mpaka usiku. "Nimekweleza mpango wote kuhusu uchumba wetu na siku ya kufunga ndoa," Charles alisema hali akichekacheka.

Charles alipofika nyumbani karibu saa nane alikuta mazishi bado hayajafanywa. Alimwangalia Ndalo mara ya mwisho. Rosa, baada ya kupeleka vitu vyake nyumbani alikwenda naye mazikoni. Barua alikuwa bado hajaisoma. Bigeyo alikuwa amekaa karibu na maiti ya mumewe. Alikuwa akilia kwa sauti kubwa sana. Alikuwa akimpapasa maiti akisema: "Kwanini umeniacha nyuma! Kwanini hukuningoja tukaenda pamoja! Kwanini! Kwanini!" Nywele zake zilikuwa zimeenea vumbi. Maziwa yake yalikuwa hayakufunikwa.

Kaburi lilikuwa tayari na sasa maiti—baada ya kuoshwa—alitolewa nje. Bigeyo alijitupa chini; alilia kwa sauti: "Kwaheri! Kwaheri! Sitakuona tena! Sitakuona tena! *Obubwacheyo!* (wasalimu huko uendako!)". Maiti alipotelemshwa chini kaburini Bigeyo alitaka kujitupa mle



ndani ya shimo. Watu walimshika. Ndalo alizikwa. Macho yao yalikuwa mekundu. Watu wengi wa kijijini walikwenda kuwaliwaza waliofiwa. Baba yake Charles pia alikuwa amekwishafika.

"Ee, mpo mnazitazama siku zinapita. Amewaacha."

"Ee. Sisi tupo, ndiyo hali ya dunia."

"Mtafanya nini, baba! Uwezo hatuna!"

Hivyo ndivyo walivyokwenda wakiwaambia waliofiwa. Kila aliyefiwa aliambiwa maneno yaleyale. Kila aliyefiwa alijibu maneno yaleyale. Wazee waliendelea zaidi. Walianza kusimulia jinsi marehemu alivyokuwa mwema na jinsi alivyokufa; maneno aliyokuwa akisema.

Watu wengi walikuwa wakizungumza kuwasalimu waliofiwa; mji wote ulikuwa na huzuni. Wakati huohuo mtu fulani alisikika akiimba wimbo. Watu walishindwa kufahamu kama mtu huyo alikuwa akiimba au labda mlevi. Alipofika nyumbani kila mtu alimwangalia. Mji wote ulinyamaza kimya! Alikuwa Zakaria, alikuwa akiyumbayumba: alikuwa amekunywa. Alianza kupiga kelele.

"Watu wote mliopo hapa, mnatafuta nini! Mnafikiri hapa kuna arusi! Ondokeni hapa! Ndalo amekwishakufa kesho ataoza! Sitaki kusikia mtu akilia bwe! bwe! hapa!"

Watu wote walikuwa kimya. Zakaria alifanya jambo la ajabu. Kila mtu alishangaa: huu haukuwa wakati wa kusema maneno kama hayo. Zakaria alikuwa amelewa; lakini siyo tu ulevi uliomfanya asema hivi, lakini hasa kwa kuwa alikuwa amezoea mizaha. Zakaria alikuwa mtu mwenye mizaha mingi. Alifikiri kwamba alikuwa akifanya mizaha. Alipoona kwamba watu hawakufurahia mizaha yake alijaribu tena. Alikwenda akapanda juu ya kaburi la Ndalo. Kila mtu sasa alikuwa akimwangalia kwa mshangao mkubwa. Hata wanawake walitoka ndani ya nyumba kuja kumwona. Zakaria alitoa kofia yake kichwani. Akiwa amepanda juu ya kaburi alianza kusema:

"Uhuru wananchi! Wananchi uhuru!"

Hapakuwa na mtu aliyejibu. Watoto walianza kucheka. Zakaria aliposikia wakicheka aliendelea.

"Mimi, nikiwa hapa kama mwenyekiti wa walevi, ni..." Zakaria hakumaliza maneno yake kitu kama fimbo ndefu kiliposimama wima juu ya kifua chake. Zakaria alianguka chini kwa ubavu na kufa palepale. Kabla hajaanguka mwanamke mmoja alisikika akilia kwa sauti ya juu sana "Wayii!" Yule mwanamke moyo ulisimama, alilala chini maiti.

Watu walikimbia lakini wengi walibaki. Mtu mmoja sasa alisikika akijitapa kwa kutaja majina ya babu zake:

"Kwa jina la Mkaka na Kamera! Nimeua mbwa! Mtu hawezi kudharau mji wa mtu namna hii!"

Zakaria alikosa heshima. Alifanya kosa kubwa. Lakini sababu nyingine iliyomfanya aseme vile ilivumbuliwa baadaye amekwisha kufa—Zakaria alikuwa mtani wao. Na kufuatana na desturi ya Wakerewe mtani anaweza kumtania mtani wake wakati wowote na mahali popote isipokuwa mahakamani. Anaweza pia kuchukua chochote kisichozidi thamani ya mbuzi mmoja. Mtani hapaswi kuhamaki wakati huu. Na hivyo ndivyo Zakaria alivyowatania watani zake.

Lakini kwa wakati ule hii haikueleweka. Ndiyo maana sasa hata yeye alikuwa amelala juu ya kaburi la Ndalo amekufa. Mkuki ulikuwa bado umemwota kifuani. Hakuna aliyepata wazo la kwenda kung'oa mkuki huo. Katika kundi la wanawake, Regina alikuwa hapumui tena. Alikuwa kweli amekufa. Baada ya muda mfupi watu waliokuwa wamesimama pale waliingiwa tena na fahamu zao. Walimtoa mkuki. Zakaria alipotolewa mkuki, damu nyingi ilimtoka kifuani. Mji mzima ulinuka damu.

Maafa haya yalitokea saa mbili hivi baada ya mazishi. Wakati huo Rosa hakuwapo. Baada ya mazishi ya Ndalo Rosa alipatwa na wasiwasi mwingi juu ya barua aliyopewa na mchumba wake. Alikwenda nyumbani upesiupesi ili aisome barua yake. Rosa, kabla hajaisoma alianza kuibusu. Aliifungua kwa makini. Mikono yake ilikuwa ikimtetemeka. Mwishowe barua ilifunguliwa. Mle ndani kulikuwa na kipande kidogo cha karatasi ngumu, aina ya zile zitumikazo kuwekea sementi. Rosa hakuamini alichoona. Alijikaza. Aliisoma ile barua: "Ha! Rosa, kweli wewe ulikuwa bikira!. Unafikiri baada ya kufahamu kwamba ulichezewa sana huko Morogoro, na baada yangu mimi mwenyewe kuona bonde la ufa na kuliona lile sikio, unafikiri mimi ninaweza kukuoa! Ha! Dada yangu, sahau. Haiwezekani hata kwa mizinga! Hata kama ukiwa wa bure!"

Huo ndio uliokuwa mwisho wa maneno ya kile kikaratasi. Rosa alipomaliza kukisoma kichwa kilimwanga. Aliona kizunguzungu. Jasho lilimtoka. Machozi yalimtelemka mpaka kifuani. Rosa aliona ulimwengu wote ukimwonea huruma, lakini sasa aliona kama kwamba ulimwengu wote ulikuwa ukimchekelea. Kuishi aliona hawezi. Aliona ni fedheha. Alitafuta chupa. Aliona chupa moja iliyokuwa na mafuta ya nywele ndani yake. Bila shaka yalikuwa mafuta ya Sperantia. Rosa aliyamwaga chini. Alichukua ile chupa na kuisagasaga juu ya jiwe. Baada ya kuisaga aliweka ule ungaunga wa vipande vya chupa ndani ya glasi. Aliweka maji.



Rosa alifikiri kwanza kabla ya kunywa. Alitubu dhambi zake. Alitafuta karatasi nzuri sana halafu alijichanja mkononi kwa wembe. Damu ilitoka. Kwa damu hiyo aliandika maneno fulani juu ya karatasi. Alipomaliza kuandika maneno yake Rosa alivuta hasira yake. Alifikiri juu ya maisha. Mara moja alikunywa yale maji. Alilala juu ya kitanda cha Honorata. Palepale damu ilianza kumtoka mdomoni. Vile vipande vya chupa vilimkatakata kooni. Rosa alitema mate. Aliona damu. "Asante. Kifo njoo upesi," alisema. Baada ya muda mfupi Rosa alisikia maumivu makali sana tumboni. Muda mrefu haukupita Rosa alijiona anaanza kupoteza fahamu. Alianza kuona kitu kama moshi mbele ya macho yake. Alisema maneno yake ya mwisho. Hapakuwa na mtu yeyote aliyeyasikia isipokuwa manyigu yaliyokuwa yamejenga paani.

"Sasa ninakufa; ninakufa sasa. Maisha yangu yalikuwa magumu. Sasa nimeona wazi kwamba malezi yangu ndiyo yalikuwa chanzo cha taabu. Malezi. Siyo malezi ya mama, lakini malezi ya baba yangu. Kweli baba alinichunga. Nilichungwa kama wasichana wa jela. Nilipopata uhuru, nilishindwa kuutumia. Deogratias, Thomas, Charles—wote hao nimewapoteza. Kwaheri Flora, kwaheri Honorata, kwaheri Stella, kwaheri Sperantia, Emmanuel kwaheri! Baba na mama samahani kama nimefanya vibaya."

Alianza sasa kuona nyotanyota machoni. Alipiga kelele. "Padri! Ninamwona Padri! Unasoma nini! Biblia! Biblia! Padri! Padri! Usitoke nje! Ningoje! Niambie zaidi!"

Rosa hakuweza kusema zaidi. Sasa macho yake yalikuwa yamefumbwa. Honorata alipokuja kumpasha habari juu ya kifo cha wazazi wao alifikiri Rosa alikuwa amelala.

"Rosa! Rosa!"

Rosa hakujitingisha.

"Rosa! Amka baba na mama wamekufa!"

Rosa hakujitingisha.

"Rosa! Husikii?"

Rosa hakujitingisha. Honorata alitambua kwamba Rosa alikuwa hapumui. Alitambua kwamba Rosa alikuwa amekufa: mwili wake ulikuwa baridi. Honorata alianguka chini na kuzimia.

Baada ya muda maiti waliletwa nyumbani ili walazwe. Kwa siku hiyohiyo ilikuwa vigumu kuwafanyia mazishi. Watu walikuwa bado hawajafika majumbani kwao tangu asubuhi. Walikuwa wakiona njaa. Zaidi ya hayo, mazishi yalikuwa hayawezi kufanywa kabla ya jamaa za

marehemu kufika; kabla ya mtoto wao mwingine— Flora—kufika. Kulikuwa na watu wengine waliotaka mazishi yafanywe siku hiyo. Walisema: "Maadamu mtoto wao wa kwanza yupo, tunaweza kuwazika leo ili kesho tufanye kazi zetu majumbani." Walikuwa hawajafahamu Rosa alikuwa wapi, wala hapakuwa na mtu aliyekuwa amekwishamwona baada ya mazishi ya Ndalo.

Watu walikuwa bado wakibishana waliposikia Stella anatoka ndani ya nyumba hali akilia. Badala ya kulia akitaja majina ya baba na mama, yeye alilia akitaja majina ya Rosa na Honorata. Watu walikimbilia ndani ya nyumba kuona kulikuwa na nini. Juu ya kitanda alikuwa amelala Rosa. Alikuwa amekufa. Chini alikuwa amelala Honorata. Huyu alikuwa bado akipumua kidogo sana. Waliposhika mkono wake, waliona kwamba damu ilikuwa bado ikitembea. Honorata alitolewa nje ili apate hewa. Alimwagiwa maji ili azinduke upesi.

Katika kijiji cha Namagondo maafa kama haya yalikuwa bado hayajatokea hata siku moja. Watu wanne kufa siku moja! Na wote majirani! Na watatu wakiwa wa mji mmoja! Kijiji kizima kilijaa masikitiko. Wale waliokuwa na nia ya kuondoka walikaa ili kufahamu Honorata atakuwaje. Watu wengine wa kijijini waliokuwa wakiishi mbali walifika kuja kuangalia maiti. Wachungaji walipoambiwa habari hii waliacha ng'ombe zao machungani na kukimbia kwenda kuangalia ili wasije simuliwa tu. Wanawake waliokuwa wakitoka kuteka maji walipatwa na bumbuazi waliposikia habari hii. Vibuyu, mitungi na madebe yao ya maji vilianguka chini kutoka vichwani pao. "Wuuu!" Walipiga kelele pamoja kwa mshangao. Wale ng'ombe walioachwa machungani walitembea ovyo. Walikula mihogo; walikula marando; walikula mpunga; hapakuwa na watu wa kuwachunga. Watu wote walikuwa nyumbani kwa Zakaria.

Usiku Honorata alizindukana. Watu walimwona mzima. Walilaza maiti mahali pamoja msitarini na kwenda zao majumbani kwao kutafuta chochote kile ili waweke tumboni. Usiku huo ulikuwa mtulivu ajabu. Kijiji kizima kilikuwa kikiwasikitikia watoto waliobaki. Hata watoto wadogo wa kijijini walitambua kwamba kitu fulani kilitokea siku hiyo. Wao pia walisikitika. Watoto wengine waliwauliza baba zao: "Kwa nini leo watu wamenyamaza?" Hakuna aliyewajibu. Wengine waliuliza: "Hivi leo Maji—Machafu hakunywa nini! Hatujasikia anaimba!" Hakuna aliyeweza kuwajibu. Waliokuwa wakishiriki na Zakaria katika ulevi walisikitika sana. Hapakuwa na mtu wa kupiga kelele usiku huo. Zakaria alipokuwa amelewa alizoea kuimba na kupiga kelele "Hoi, Hooi!"



Karibu kijiji kizima kilizoea kusikia sauti yake. Usiku huo sauti yake haikusikika. Zakaria alikufa. Watu walishangaa, "Jamani mauti kukaa! Mauti kukaa! Maji–Machafu naye amekufa! Kweli mauti kukaa!" Hata wale ambao hawakuwa na ujamaa na Zakaria walisikitika. Usiku wa manane bundi walianza kusikika. Watoto walijikunja vitandani—watu wa kisiwa hiki wanaamini kwamba bundi akilia karibu na mji kifo hutokea humo. Kwa hiyo bundi walipolia hofu ya watu iliongezeka.

Rosa alilazwa pembeni na Zakaria pia. Regina alilazwa kati yao. Hivyo ndivyo walivyopangwa. Usiku mzima taa iliwaka. Pembeni, Stella na Sperantia walionekana wakilia. Emmanuel alikuwa naye akilia. Kwa wakati huu alikuwa akilia kwa sababu dada zake walilia. Uchungu wa kupoteza baba, mama na dada hakuweza kuupata. Watoto hawa walikesha wakilia. Walililia wazazi wao; walimlilia dada yao.

Vichwa vya maiti vilikuwa vimeachwa wazi ili watoto wawaangalie wazazi wao mara ya mwisho. Uso wa Zakaria ulionyesha wazi kwamba alikufa kwa maumivu makali. Uso wa Regina ulikuwa umepumzika. Ulikuwa umetulia. Alionekana mzima bado ingawa kweli alikuwa amekufa. Uso wa Rosa ulionekana kama wa mtu anayetabasamu. Ingawa alikufa kwa maumivu aliweza kufunga na kufumba mdomo na macho yake vizuri sana. Hizi ndizo zilikuwa nyuso tatu zilizokuwa na kitu fulani cha kuuambia ulimwengu. Nyuso hizi tatu zilikuwa na siri kubwa—siri ya maisha, siri ya upendo, siri ya malezi. Kesho yake asubuhi, yeyote yule aliyeangalia uso wa Rosa alisema:"Sijaona msichana aliyesumbuka maishani kama huyu!" Yeyote yule aliyeangalia uso wa Regina alisema: "Kweli maishani sijaona mwanamke aliyewapenda watoto wake kama huyu!" Yeyote yule aliyeangalia uso wa Zakaria alisema: "Kweli mwamba alifahamu namma ya kuyakata maji. Hakuna mtu aliyewachunga binti zake kama yeye!"

Maiti walioshwa kabla ya kuzikwa. Waosha walikuta kijikaratasi kidogo ndani ya kwapa la Rosa. Kilikuwa kimeandikwa kwa damu. Ilikuwa karatasi safi sana. Juu lilikuwa limeandikwa jina la Charles. Waliisoma: "Charles mimi nilikupenda. Ninakupenda hata sasa. Charles, ninajiua kwa ajili yako. Lakini kwa kuwa ninakupenda, ninakwambia siri moja kubwa uizingatie. Charles kuoa bikira ni bahati tu wala si kitu cha kutafuta: ukimwonja mchumba wako kabla ya ndoa si bikira tena, hata kama alikuwa." Charles alikuwa nje. Aliitwa. Alipewa barua yake. Charles alipomaliza kuisoma alimwangalia Rosa. Alitamani awe mke wake; Lakini sasa alikuwa amekufa. Alitoka nje.

Makaburi matatu yalichimbwa kwenye sehemu ya waumini. Flora alikuwa amepigiwa simu. Mazishi yalisemekana kufanywa saa saba baada ya meli kuwasili kutoka Mwanza. Walikuwa wakimngojea Flora, kwani sasa yeye ndiye aliyebaki kuwachukua wadogo zake. Flora alifika kwa ndege pamoja na mchumba wake. Flora alizimia aliposikia maafa hayo, sasa alikuwa amerudiwa fahamu. Kwa kuwa alifika saa tatu asubuhi mazishi yalifanywa saa sita. Jamaa za marehemu, wengi walikuwa wamekwishafika. Saa sita Padri alifika kufanya ibada ya mazishi. Padri alipofika maiti walikuwa wamelazwa kanisani. Alivaa nguo na kuanza ibada. Alipofika penye maiti aliwanyunyizia maji ya baraka na kusema:

"Kama ungezikumbuka dhambi, ee Bwana, nani, ee Bwana, angesimama?"

Baadaye Zaburi ilisomwa. Baada ya muda mfupi Padri alisoma sala kwa sauti.

"Twakuomba, ee Bwana, uzisamehe roho za watumishi wako, Rosa, Regina na Zakaria makosa yao, ili baada ya kufariki dunia waishi kwako. Na waliyokosa katika maisha yao kwa udhaifu wa mwili, uyafute kwa huruma na upole wako. Kwa ajili ya Kristo, Bwana wetu."

Wote walimalizia,"Amina."

Zaburi ilisomwa. Ibada ya kanisani ilimalizika. Maiti walibebwa kupelekwa kaburini. Huko watu walikuwa wengi. Charles naye alikuwa huko akingojea mazishi kamili. Walevi pia walikuwapo. Walikuwa wamekuja kumwona rafiki yao akizikwa. Walipofika kaburini Padri aliyabariki makaburi. Baada ya kuimbaimba alisoma sala nyingine, ndefu zaidi. Charles alikuwa akitetemeka: alifikiri labda jina lake pia lilikuwa limeandikwa mle ndani karibu na lile la shetani.

"Ee Mungu, viumbe vyote vinaishi kwako, na miili yetu inapokufa haipotei kwako, bali hugeuzwa kuwa bora zaidi. Basi twakuomba sana, kwa wema na huruma yako uzirehemu roho za watumishi wako na kuyafuta makosa yaliyowapata walipokosa kutimiza mapenzi yako kwa hila za shetani na kwa ubaya na udhaifu wao wenyewe. (Hapakuwa na mtu wa kuongezea—au kutokana na malezi mabaya). Uwaamuru malaika ..."

Padri hakumaliza mtu mmoja alipopiga kelele. "Nimemletea Zakaria chupa mbili za moshi, moja anywe atuage sisi walevi! Ya pili atakwenda nayo huko kwenye ufalme wa Kristo. Amina!" Kila mtu alishangaa. Wadhaifu walicheka. Watu walifikiri mchezo. Alichukua chupa moja na kuitupa kaburini. Mtu huyo alishikwa na kupelekwa nyumbani kwake.



Padri aliendelea na ibada. Maiti walitelemshwa kaburini. Kaburi la Regina lilikuwa katikati. Bwana wake alikuwa mkono wake kulia, na bintiye mkono wa kushoto. Walipotelemshwa Padri alichukua sepeto na kutupa udongo kidogo ndani ya kila kaburi. Kisha jamaa za marehemu walifanya hivyohivyo. Watu wenye nguvu walianza sasa kufukia yale makaburi kwa haraka. Makoleo yalikuwa mengi. Honorata alipoona watu wakifukia bila huruma, aliposikia udongo ukiwaporomokea wazazi na dada yake, alizimia tena. Alichukuliwa na kupelekwa nyumbani.

Makaburi yote yalijazwa udongo. Na sasa mazishi yalikuwa tayari, wanawake walianza tena kulia. Flora alilia. Alilia kwa sauti ya juu sana. Alikwenda kulala juu ya kaburi la mama yake hali akijigaragaza pale juu. Wanawake walimshika na kumsindikiza mpaka nyumbani. Alikuwa hawezi kutembea. Aliwekwa kati ya wanawake wawili. Njiani Flora alilia sana "Yoho! Yoho yoo wai! Yoho yoo wai! Haiwezekani! Haiwezekani!"

Honorata, Stella na Sperantia, macho yalikuwa mekundu sana kwa sababu ya kulia.

Watu walikuwa wengi nyumbani. Wanawake wa kijijini walifahamu shida ambayo ingewapata watoto hawa wadogo waliobaki pake yao. Karibu kila mwanamke alileta bakuli la unga jioni hiyo. Wanaume walileta kuni. John alitoa kiasi fulani cha pesa; watu walitumwa kwenda kununua samaki. Usiku ulipoingia watu walitawanyika kwenda kulala. Walibaki jamaa za marehemu tu, na watu waliokuwa na uhusiano mzuri nao. Usiku mvua ilikunya nyingi. Watu ambao huombeleza hulala nje, lakini siku hiyo walitafuta nyumba. Mtu mmoja tu alilala nje—Honorata. Mvua ilimwishia mwilini.

Siku tatu zilizofuata zilikuwa za maombolezo. Marehemu Regina alikuwa amekwishafikisha ng'ombe wanne tena. Baada ya kitoweo kukosekana jamaa waliamuru ng'ombe hawa wachinjwe ili watu wale. Ng'ombe walichinjwa. Kila siku mmoja. Ingawa maombolezi huwa ni siku tatu, watu waliendelea kukaa mpaka siku ya nne ng'ombe wa mwisho alipochinjwa. Siku mbili zilizofuata zilikuwa za unywaji. Watu walikunywa. Utafikiri hapakuwa na kilio. Nyama ilipokwisha jamaa walianza kutawanyika. Wengine hawakuaga. Jamaa wengine za marehemu walibaki ili kugawana vitu vya urithi. Ilijulikana kwamba Zakaria alikuwa bado na shilingi mia saba benki; nazo zilikuwa zimewekwa kwa jina la Emmanuel. Jamaa hawa walimlazimisha Flora aende kuzitoa zile pesa benki waje wazigawane. Flora alipokwenda benki

hakuweza kuzipata. Karibu jamaa zake wawe wehu. Walimwita mwizi, malaya na mshenzi. Jamaa hawa waliona kwamba huu ulikuwa mji wa wanawake.

Lakini Zakaria alikuwa mwalimu. Alifahamu kwamba matatizo yatatokea kuhusu urithi wa mali yake. Jamaa hawa baada ya kukosa funguo za kufungulia makufuli ya masanduku, waliyapasua kwa shoka. Mle ndani walikuta shilingi hamsini ndani ya bahasha iliyokuwa imeandikwa jina la Regina juu. Katika sanduku jingine walikuta kijibarua kidogo, nacho kilieleza habari yote kuhusu watu watakaorithi vitu. Zakaria alikiandika zamani. Wakuu wa dini walikuwapo kuangalia kwamba haki ilikuwa ikitumika. Kijikaratasi kilisema kwamba warithi walikuwa ni watoto tu. Kila mtoto alikuwa amepangiwa vitu vyake vya kurithi. Jamaa walikataa kabisa kwamba huo haukuwa mwandiko wake. Wakuu wa dini walipobisha, walichukua mapanga na kuwafukuza. Sasa walikuwa huru kutenda lolote.

Hawa jamaa walirithi. Walirithi hawa jamaa. Walirithi, walirithi. Jamaa waligawana vitu. Walirithi kila kitu kilichokuwa ndani ya nyumba. Walirithi michungwa na miembe. Walirithi migomba yote. Walirithi paka na mbwa. Walirithi majani yaliyokuwa juu ya paa, na miti yote iliyofanya nyumba isimame. Walirithi mashamba yote. Walirithi kuku; walirithi hata mbolea ya ng'ombe. Walirithi. Hawa jamaa, kweli walirithi. Lakini, hapakuwa hata na mtu mmoja aliyeweza kusema atamchukua mtoto fulani amtunze. Badala yake walimdai John alipe mahari ili pia wagawane. Vitu vya Rosa vilikwenda kuchukuliwa.

Baada ya kugawana vitu hivi, watoto walikaa pale nyumbani kwa muda wa siku moja tu. Kila kitu walichogusa waliambiwa si chao. "Pesa zenu zimo benki," walitulizwa. Flora aliwaomba Masista waliokuwa wakikaa Kagunguli wamsaidie kutunza dada zake kwa muda wa miaka miwili. Hawakukataa: waliomwonea huruma. Baada ya siku moja, Honorata, Stella, Sperantia na Emmanuel walipelekwa huko. Flora alifunga safari kurudi Mwanza pamoja na John. Maafa yalimfanya John ampende Flora. Huruma iliwafanya kweli wapendane. Wakiwa bado nyumbani John alimkubatia Flora na kumwambia: "Flora, mimi nitakutunza; baada ya muda wa miaka miwili ya kazi, nitawatunza wadogo zako."

Flora aliwambia wale watu waliojidai jamaa zake: "John hatatoa hata chapa kwa ajili yenu. Kuwatunza wadogo zangu—hakuna mahari ipitayo hiyo!" Walifunga safari mpaka Mwanza. Waliishi kama mume na mke.



Huku nyuma jamaa zake waliangusha nyumba na kutoa majani pamoja na miti. Machungwa yalipokuwa yakiiva walifika kuja kuchuma. Mashamba yalilimwa na jamaa zao. Bigeyo pia alirudi kwao. Yeye pia hakurithi kitu chochote. Kila kitu kilichukuliwa na jamaa za Ndalo. Huo ndio ulikuwa mwisho wa miji hii miwili iliyokuwa na mengi ya kuuambia ulimwengu.

Charles, baada ya kupata kile kijibarua kilichokuwa kimeandikwa kwa damu, alisumbuliwa na dhamiri yake. Aliona ukweli ndani ya maneno yale. Aliona kutegemea bahati ilikuwa kazi bure. Alikuwa hawezi kupata bikira. Lakini yeye alihitaji bikira. Baada ya siku chache, Charles alikwenda Kisubi kusomea ubruda. Alichagua maisha ya kukaa bila kuoa.

Honorata akiwa Kagunguli alitembelea siku moja kijiji cha Namagondo—umbali wa maili saba hivi. Stella na Sperantia waliambatana naye. Walifika mpaka makaburi ya Rosa na wazazi wao. Walipanda miti ya michungwa juu ya makaburi haya ili wasije wakayasahau baadaye. Miti iliota vizuri na haikukawia kukua; lakini ilipokua, mti mmoja tu ulitoa matunda mazuri—mti uliokuwa katikati. Miti miwili ya pembeni ilitoa matunda mabaya. Hata baada ya miaka kumi, matunda yalipokuwa yakiiva, watoto hawa walizoea kutoka Mwanza kuja kuchuma matunda kutoka ule mti wa katikati. Walikula damu na mwili wa mama yao. Walimkumbuka mama yao.

Baadaye walipokuwa watu wazima wote, Emmanuel aliwasimulia dada zake ndoto hii aliyoiota zamani wakati akiwa usingizini.